**13 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 13 Mei, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tisa, Kikao cha Ishirini na Tatu, leo tarehe 13 Mei, 2025.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Selemani Jafo.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake. Hayupo, kwa niaba yake, Mheshimiwa Rashid Shangazi.

Na. 289

### Kesi Inayomkabili *HRM* wa Kampuni ya *Dangote Cement* Mtwara

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia wapi kufuatilia kesi inayomkabili *Human Resources Manager* wa Kampuni ya *Dangote Cement* Mtwara?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya ukaguzi maalum katika Kiwanda cha Saruji cha Dangote kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa Sheria za Kazi, ikiwemo Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura 436. Aidha, ukaguzi huo haukuweza kupata ushahidi kuhusu uwepo wa kesi inayomkabili Meneja Rasilimali Watu, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa,

imekuwa ni kawaida kwa wageni wengi katika eneo hili la utawala *(Human Resource Management)*, kutokana na asili ya nchi zao, wanapotoka huwa hawafahamu vizuri taratibu ambazo *ILO* inazisimamia. Je, Serikali haioni kwamba ni busara sasa nafasi hii muhimu sana katika nchi yetu isiwe inatolewa kwa wageni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shangazi ametoa ushauri kwa Serikali, lakini kimsingi kwa mujibu wa sheria, ipo hivyo kwa maana ya wageni hawaruhusiwi kushika hizi nafasi za Afisa Rasilimali Watu, kwa maana wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri wa Kazi alikutana na Menejimenti ya Dangote pale ofisini, na wakajadiliana jambo hili kwa kina, na baadaye wakajiridhisha pasipokuwa na shaka kwamba, huyu mhusika ambaye ametajwa hapa kwamba ni Afisa Rasilimali Watu, hakuhusika moja kwa moja kwenye eneo hilo, na badala yake yupo Mtanzania ambaye anahudumu katika nafasi hiyo. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea. Naye hayupo, kwa niaba yake, Mheshimiwa Lupembe.

Na. 290

### Kupandisha Hadhi Shule za Sekondari za *Korogwe TC*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE K.n.y. MHE. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi Sekondari za Ngombezi, Joel Bendera na Kwamndolwa, *Korogwe TC,* kuwa za kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule za Sekondari Ngombezi, Joel Bendera na Kwamndolwa ni shule zilizo kwenye mpango wa kupandishwa hadhi na kuwa za Kidato cha Tano na Sita. Shule hizi zimejengewa baadhi ya miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita. Hivyo, shule hizi zitapandishwa hadhi pindi zitakapokidhi vigezo. Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ili kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita katika Shule za Sekondari Ngombezi, Joel Bendera na Kwamndolwa kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa, tumejenga shule za sekondari nyingi katika maeneo yetu na watoto wamekuwa wengi sana, hasa wa *form four,* ni lini Serikali itaweka mikakati kuhakikisha tunaongeza *A' Level* katika maeneo yetu hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa, Jimbo la Nsimbo napo kuna shule za sekondari nyingi na *high school* zipo shule mbili tu, na shule za sekondari zipo kama 22, ni lini Serikali itatuongezea *high schools* katika Halmahsauri yetu ya Nsimbo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya uwekezaji mkubwa sana katika kuhakikisha kwamba elimu msingi inaendelea kuimarika. Imekuwa ikifanya hivyo kwa kuboresha miundombinu na sekta nzima, kwa maana ya kupata walimu, vifaa na mazingira yote ambayo yanawezesha elimu yetu ya msingi kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba nijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja kwamba Serikali katika kipindi cha miaka minne tayari imeshajenga mabweni 738. Kama sote tunavyofahamu, shule nyingi za kidato cha tano na sita ni Shule za Kitaifa na hivyo zinakuwa ni shule za bweni. Kwa hiyo, kwa kufanikisha ujenzi wa miundombinu muhimu, ikiwemo mabweni, tayari tumeweza kupandisha hadhi shule hizi za kidato cha nne kuwa sasa zina hadhi ya kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya jitihada hizo kwa kuendelea, siyo tu kujenga Shule za Sekondari za Kata, lakini kuendelea kupandisha hadhi baadhi ya shule hizi za kata, kuzijengea miundombinu ambayo itawezesha kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Kwa muktadha huo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Jimbo la Nsimbo tutaendelea na jitihada hizo za kuendelea kuongeza shule za kidato cha tano na sita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, nimekuona.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Shule ya Sekondari Inchugu na Nyanungu zimepandishwa hadhi tangu mwaka 2024. Kuna mabweni mawili yamekamilika, madarasa zaidi ya sita yamekamilika, matundu ya vyoo yamekamilika, vitanda vimewekwa katika mabweni yote. Sasa ni lini wanafunzi watapelekwa Inchugu *High School* na Nyanungu ili watoto wasiende umbali mrefu, wakae pale pale shuleni wapate elimu nzuri? Ahsante

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Waitara kwamba kama nilivyotangulia kusema, Serikali pamoja na kwamba inaendelea kuhakikisha tunafikia kata mbalimbali nchini ambazo hazina shule za

sekondari na kuzijengea shule hizi pia, tunafanya jitihada ya kupandisha hadhi baadhi ya hizi shule ili ziweze kuchukua wanafunzi wa Kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule ambazo Mheshimiwa Waitara amezitaja, hizi mbili ambazo amekiri kwamba miundombinu ni toshelezi sasa kuweza kupandishwa hadhi na kuanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha tano na sita, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni taratibu tu, lakini tutakamilisha taratibu hizo haraka iwezekanavyo ili sasa wanafunzi wetu wa kidato cha tano na sita waweze kuanza kusoma katika hizi shule mbili ambazo amezitaja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani.

Na. 291

**Kuchelewa Kutolewa kwa Mikopo ya Wanawake**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y. MHE. KABULA E. SHITOBELO** aliuliza:-

Je, sababu zipi zinasababisha Mikopo ya Wanawake kuchelewa kutolewa kwa waliokidhi vigezo vyote, hasa Wanawake wa Mkoa wa Mwanza?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri za Mkoa wa Mwanza inaendelea kutekeleza jukumu la utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake waliokidhi vigezo kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo za Mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo hiyo hutolewa kwa utaratibu mahususi unaolenga kuhakikisha uwazi, usawa na ufanisi katika usimamizi wa fedha hizo. Kwa mujibu wa kanuni hizo, Serikali za Mitaa hushughulikia maombi ya mikopo yanayowasilishwa katika ngazi ya kata na kufuata hatua muhimu, ikiwemo uchambuzi wa vikundi, ukaguzi wa miradi, tathmini ya maombi, uhakiki wa taarifa na utoaji wa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato huu unatekelezwa ndani ya siku 60 tangu tarehe ya mwisho ya kupokea maombi, ambayo hupokelewa ndani ya siku 30 baada ya kutolewa kwa tangazo. Hali hii husababisha kuchelewa kwa utoaji wa mikopo, siyo kwa nia ya kuwanyima fursa wanawake, bali kwa madhumuni ya kuhakikisha utaratibu wa utoaji wa fedha hizi unafanywa kwa usahihi na kwa vikundi vilivyo tayari kutekeleza miradi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mchango mkubwa wa wanawake katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa kutambua hilo, imeendelea kutoa elimu, kuimarisha mifumo na taratibu za utoaji mikopo ili kupunguza ucheleweshaji usio wa lazima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng’wasi Damasi Kamani.

**MHE. NG’WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Niendelee kuipongeza Serikali kwa kuendelea kurahisisha utaratibu huu wa kutoa mikopo hii ya vikundi maalum. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; changamoto hii inayowakuta wanawake wa Mkoa wa Mwanza ya ucheleweshwaji wa kutolewa mikopo pindi wanapotimiza vigezo vyote, ndiyo hasa inawapata vijana kote nchini wanaoomba mikopo hii kupitia halmashauri zetu. Sasa, nini kauli ya Serikali kwa ajili ya kutatua changamoto hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; vijana wengi sana wamehamasika kujiajiri na wanatuma maombi mbalimbali kwenye Halmashauri kupata mikopo hii kwa ajili ya mitaji yao, lakini ni ukweli usiofichika kwamba, fedha hizi hazitoshi kuwahudumia vijana hawa. Sasa, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inaendelea kuongeza fedha katika mifuko hii ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Ng'wasi Kamani kwa swali lake lenye nia ya kuwasemea vijana wote nchini. Kuhusiana na swali lake la kwanza, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuendelea kuwasisitiza Wakurugenzi wote wa Halmashauri wafuate Kanuni za Utoaji wa Mikopo hii ya 10% inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zinataka ndani ya siku 60 mchakato mzima uwe umekamilika na wale wote wanaokidhi vigezo vya kupatiwa mikopo hii waweze kupatiwa mikopo hii. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuendelea kutoa msisitizo huo ili kuepusha ucheleweshaji wa utoaji wa mikopo, vijana wetu na wanawake waweze kupata mikopo, watu wenye ulemavu waweze kupata mikopo waende kwenye shughuli zao za uzalishaji mali waweze kujipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, naomba niendelee kuzisisitiza halmashauri zetu ziweze kuendelea kuwa bunifu kuanzisha vyanzo vya mapato kwa tafsiri ya kwamba, vyanzo vya mapato vikiongezeka, mapato ya halmashauri yakiongezeka, hata ile 10% inayotengwa kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu itaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtoe shaka Mheshimiwa Ng'wasi Kamani kwamba, ukiacha tu utaratibu wa kutoa mitaji kupitia Mfuko huu wa 10% ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri, kuna taratibu nyingine ambazo zinawawezesha kimitaji vijana pamoja na makundi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna mifuko ambayo inaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo kuna Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; kuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; na pia kuna mifuko ambayo inaratibiwa na Wizara za kisekta, kwa mfano, kwenye madini kuna Mradi unaitwa *Mining for Better Tomorrow* ambao unawawezesha vijana kupata mikopo kwa ajili ya uwekezaji katika uchimbaji mdogo. Pia, kwenye sekta ya kilimo. Wizara ya Kilimo kuna Mradi wa *Building Better Tomorrow* ambao unawawezesha vijana kuingia katika sekta ya kilimo na kuwawezesha kimtaji ili waweze kufanya shughuli hizi za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali kwa ujumla itaendelea na taratibu hizi zote za kuwawezesha vijana kupata mitaji kwa ajili ya kujitengenezea ajira. Namshauri Mheshimiwa Ng'wasi Kamani aendelee kuwahamasisha na kuwaelimisha vijana kwamba, fursa ambazo zimewekwa na Serikali yao makini ya Awamu ya Sita zipo nyingi na waweze kuzitumia fursa hizi ili kuweza kupata mitaji, kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Zaytun Swai na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha wananchi, hasa wa ngazi za chini kabisa, kwenye kata na vijiji wanapatiwa elimu hii ya mikopo na taarifa ya utoaji wa mikopo ili wengi zaidi waweze kunufaika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Zaytun Swai kwa swali lake ambalo linalenga kuendelea kuongeza uelewa au kuzungumzia umuhimu wa kuendelea kutoa uelewa zaidi kwa Watanzania kufahamu kuhusiana na fursa mbalimbali za kimitaji zilizopo, hasa katika upande huu wa halmashauri, kupitia 10% ya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kutumia nafasi hii kuwaomba hata ninyi Waheshimiwa Wabunge tendelee kuwaelimisha, kuwafahamisha na kuwahamasisha wananchi tunaowawakilisha ili wafahamu fursa nzuri ambazo zimewekwa na Serikali yao kwa ajili ya kuwawezesha kimitaji. Upande wa Serikali tunafanya hivyo, pia, tunatoa mafunzo mahususi. Katika kipindi kile cha kuvipitia hivi vikundi huwa kuna mafunzo mahususi kabisa ambayo yanaelezea taratibu na fursa zaidi ambazo wanavikundi wanaweza wakapata kutokea kwenye mikopo hii ya 10% ya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali tutaendelea kutoa hamasa na kuwajengea elimu na tunafanya hivyo. Tunapita katika vyombo vya habari kuelezea kuhusiana na fursa hizi za mikopo. Pia, nasi Waheshimiwa Wabunge naomba tuungane kwa pamoja kutoa elimu hiyo kwa jamii ili waweze kufahamu fursa mbalimbali ambazo zimewekwa na Serikali yao makini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, mikopo hii ina kanuni zake na sheria, vijana, wanawake na watu wenye ulemavu wameshahamasika na kukidhi vigezo vingi, lakini kuna baadhi ya halmashauri hawatoi mikopo hiyo. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Wakurugenzi ambao hawatimizi matakwa ya kanuni hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumpongeza kwanza Mheshimiwa Christina Mnzava kwa swali lake linalolenga kuzungumzia fursa hii ya kimitaji, ambayo inatokana na 10% ya mapato ya ndani katika halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimhakikishie kwamba hakuna halmashauri ambayo haitoi mikopo hii kwa taarifa tulizonazo kwa wakati huu. Halmashauri zote zina utaratibu kwa sababu, mikopo hii imewekwa kwa mujibu wa sheria. Halmashauri zote zina mapato ya ndani. Halmashauri zote kwenye mapato ya ndani zinatenga 10%, kwa ajili ya mikopo hii kutoa na kuwezesha vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendelee kutumia nafasi hii kuendelea kuwasisitiza Wakurugenzi wote katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa waendelee kutimiza masharti ya Kisheria na Kikanuni ya utengaji wa fedha hizi na mitaji hii kutoka kwenye mapato yao ya ndani, kwa ajili ya kuendelea kuviwezesha vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kimitaji.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge Viti Maalum.

Na. 292

**Ujenzi wa Kituo cha Afya – Kata ya Lukozi**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha kimkakati kwenye Kata ya Lukozi – Lushoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga shilingi bilioni 53.5 kupitia Bajeti ya Nyongeza ya mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 214 katika Kata za Kimkakati kote nchini ikiwemo Kata ya Lukozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto. Kata ya Lukozi imetengewa shilingi milioni 250 na tayari Serikali imeanza kupeleka fedha hizo kwa awamu ya kwanza katika majimbo 120.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Kwanza nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kupeleka fedha kwenye Kituo cha Afya Lukozi, kituo ambacho kinahudumia wananchi wengi sana takribani Tarafa nzima ya Mlalo. Naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu la nyongeza. Kituo cha Afya Pagwi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi nimeshauliza hapa mara kadhaa namna ambavyo Serikali inakichukua kama kituo cha kimkakati na kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wake ili kuokoa akina mama ambao wanapata shida ya kufuata huduma za afya katika hospitali ya halmashauri ambayo ipo mbali sana na kata hii. Je, nacho kimepata fedha hizi au Serikali ina mkakati gani wa kuweza kukiwezesha na chenyewe kupata fedha na kuweza kujenga kituo hiki? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Husna Sekiboko kwa swali lake hili linalolenga kuimarisha sekta ya afya msingi, na hususan akiwazungumzia akina mama ambao anataka wapate huduma bora zaidi za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake hili moja, naomba kumpatia taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya

Awamu ya Sita imedhamiria kabisa kuhakikisha kwamba inaendelea kuimarisha sekta ya afya msingi, ndiyo maana katika kipindi cha miaka minne utaona kwamba jumla ya vituo vya afya 367 vimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mikakati hiyo ya kuboresha miundombinu muhimu katika sekta hii ya afya msingi kwa kujenga siyo tu vituo vya afya, bali pia ni pamoja na kuhakikisha kila halmashauri inakuwa na hospitali ya halmashauri na kuendelea kujenga zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kituo hiki mahsusi alichokitaja, naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama tayari kituo hiki cha afya kwenye Kata ya Lukozi katika mwaka huu wa fedha kimepelekewa shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu muhimu kabisa, nimhakikishie kwamba Serikali itaendelea kuleta fedha katika Mkoa wa Tanga katika jimbo hili la Lushoto, kuhakikisha kwamba inaendelea kujenga vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu vituo vya afya, bali pia vituo vya kutolea huduma ya afya msingi ikiwemo kituo cha afya alichokitaja Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge Mbunge wa Kilwa Kusini, litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa..., aah, yupo mwenyewe.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo.

**MWENYEKITI:** Haya.

Na. 193

**Hitaji la Gari la Wagonjwa – Kituo cha Afya Nanjirinji**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka gari la kubeba wagonjwa katika Kituo cha Afya Nanjirinji Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali katika kuboresha huduma za afya ni magari ya wagonjwa na magari ya usimamamizi wa huduma za afya. Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilinunua magari 594 na kuyapeleka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ilipelekewa magari matatu ya kubebea wagonjwa na kupelekwa Hospitali ya Kinyonga, Kituo cha Afya Chumo na Njinjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa kwa ajili ya vituo vya afya vyenye uhitaji kote nchini, kikiwemo kituo cha afya Nanjirinji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na pia nashukuru na kuipongeza Serikali yangu kwa hatua hii ya kupeleka magari ya kubebea wagonjwa kwenye vituo vyetu vya afya. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kutokana na ukweli kwamba baadhi ya vituo vya afya kikiwemo Nanjirinji vipo mbali na ni vigumu kufikika kutoka kwenye hospitali zetu, hasa za wilaya, je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka magari ya wagonjwa kwenye vituo kama Nanjirinji kutokana na hali hii ya ugumu wa kufikika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa muktadha huo huo, je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kupeleka magari ya wagonjwa kwenye vituo vyote, ifanye *assessment* vituo vyote ambavyo ni

vigumu kufikika nchini ili magari haya yapelekwe katika maeneo yote nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Ally Kassinge kwa swali lake zuri ambalo linalenga kuendelea kuzungumzia uimarishaji wa sekta ya afya msingi. Naomba nijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja kwamba, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuwa na magari ya kubebea wagonjwa pamoja na magari ya usimamizi wa huduma za afya. Ndiyo maana katika mwaka wa bajeti 2021/2022 Serikali ilinunua magari 594 ya kubebea wagonjwa pamoja na ya usimamizi wa huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari haya yamesambazwa kote nchini katika vituo ambavyo vina mahitaji makubwa. Katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu ya msingi, magari matatu yamepelekwa kwa ajili ya kutoa huduma hizo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumuakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba kama vile Serikali ilivyoanza na jitihada ya kununua haya magari 594, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kununua magari mengine na kuyasambaza kote nchini kwa ajili ya kwenda kutoa huduma muhimu kabisa hizi za kubeba wagonjwa pamoja na usimamizi wa huduma za afya. Tutapeleka magari hayo ikiwemo katika kata zenye uhitaji, ikiwemo Kata hii ya Nanjirinji ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inatambua umuhimu, itanunua magari itayasambaza kote nchini na haitoacha kuleta katika kata ya Nanjirinji katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, nimewaona.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika haya magari 594, sisi katika Wilaya ya Chemba tuna upungufu mkubwa wa magari ya wagonjwa. Je, katika mgao unaokuja, Kituo cha Soya nacho kitapata mgao huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Fatma Toufiq kwa swali lake linalolenga kuimarisha sekta ya afya msingi. Naomba kuendelea kumhakikishia kwamba, kama Serikali ilivyotangulia kutenga fedha na kununua magari 594 ya kubebea wagonjwa, ikiwemo na magari ya usimamizi wa huduma za afya na kuyasambaza kote nchini, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa magari haya na kuyasambaza kote nchini kwa kuzingatia kipaumbele kwenye maeneo yenye mahitaji makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika kituo cha afya alichokitaja cha Soya kilichopo Chemba, Serikali itafanya tathmini na kuona uhitaji na katika maeneo ya vipaumbele ya kupeleka magari haya ya wagonjwa pamoja na magari ya usimamizi wa huduma za afya, Serikali itazingatia uhitaji alioutaja katika kituo hiki na kuleta gari hilo kwa ajili ya kuendelea kuimarisha afya msingi katika wilaya hii na katika Mkoa huu wa Dodoma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare nimewaona.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika Wilaya ya Kilwa, tuna magari mengi chakavu ambayo yanahitaji ukarabati katika vituo vyetu vya afya na hospitali yetu ya wilaya. Je, ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya ukarabati wa

magari hayo ili kuboresha huduma ya magari ya wagonjwa katika wilaya yetu ya Kilwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Francis Ndulane kwa swali lake zuri linalolenga kuimarisha sekta ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake, nichukue nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri wajibu wake wa msingi wa kusimamia utoaji wa huduma za msingi ikiwemo kwenye upande wa afya. Kwa kuwa Serikali Kuu tayari ilishanunua magari haya ya kutolea huduma ya kubeba wagonjwa pamoja na magari kwa ajili ya usimamizi wa huduma za afya na kuyasambaza kote nchini ikiwemo katika Wilaya ya Kilwa, sasa ni wajibu wa msingi wa halmashauri kupitia mapato ya ndani kuendelea kuyasimamia haya magari na kuhakikisha kwamba yapo katika mazingira mazuri, kwa kufanya ukarabati wa kila wakati kwa kadri inavyokuwa inatakiwa ili magari haya yaweze kutoa huduma za msingi kabisa kwa wananchi za kubeba wagonjwa, na huduma ya usimamizi wa huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa maelekezo haya kwa mkurugenzi kupitia mapato ya ndani aweze kukarabati magari hayo ili yaweze kutoa huduma kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Massare, nilikutaja, halafu Mheshimiwa Hhayuma utamalizia.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Katika Halmashauri ya Itigi nasi tulipata magari ambayo Serikali imetoa, lakini Kituo cha Afya Mitundu kipo mbali, tulipeleka Rungwa ambapo ni kilometa 194; na pale halmashauri tunahitaji gari kwa ajili ya kuhudumia hizi kata za karibu. Kituo cha Mitundu hakina gari kabisa. Je, Serikali ipo tayari sasa kutuletea na sisi gari

katika kituo hiki ili wananchi wa Mitundu ambako kuna *population* kubwa na uhitaji ni mkubwa katika kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Waziri ametamka kwamba magari yatakuja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Yahaya Massare kwa swali lake hili zuri linalolenga kuendelea kuimarisha sekta ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, kwamba Serikali imenunua magari 594 kwa ajili ya kubebea wagonjwa pamoja na usimamizi wa huduma za afya, magari haya yamesambazwa kote nchini, na ikiwemo pia katika halmashauri anayotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaomba niendelee kumhakikishia kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inanunua magari mengine mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba bado kuna kuna kata na vituo vya kutolea huduma ya afya msingi ambavyo vina uhitaji wa magari haya. Serikali itanunua magari haya na kuyasambaza katika vituo hivyo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba yanaweza kutoa huduma za afya nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaweka kipaumbele katika Kituo cha Afya cha Mitundu alichokitaja, na tutazingatia mahitaji aliyoyasema wakati wa kusambaza magari hayo mengine ambayo yatanunuliwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alipotembelea Hirbadaw, aliahidi kwamba tutapata gari la wagonjwa. Je, Serikali ina mpango upi wa dharura ili tupate gari la wagonjwa, kwa sababu eneo hilo lipo mbali na makao makuu ya wilaya, na tumejenga Kituo kingine cha Basotu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Hhayuma Xaday kwa swali lake hili linalolenga kuimarisha sekta ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ahadi ipo pale pale na Serikali itanunua magari kwa ajili ya kubebea wagonjwa, na vilevile itaendelea kununua magari kwa ajili ya kuimarisha sekta hii ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa ahadi ipo pale pale. Tutakapopata magari haya, yatakaponunuliwa, yatasambazwa kote nchini kwenye uhitaji na tutazingatia ahadi ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Waziri ya kuleta gari la wagonjwa katika jimbo lake Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa aulize swali lake.

Hayupo, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kwa niaba yake.

Na. 294

**Madai ya Watumishi Waliopandishwa Vyeo**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawalipa watumishi wastaafu waliopandishwa madaraja kisha hatua hizo kusitishwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa watumishi ambao walipandishwa vyeo na barua zao za kupandishwa vyeo kuingizwa kwenye Mfumo wa Taarifa za Utumishi na Mishahara na baadaye upandishwaji vyeo huo kusitishwa mwezi Juni, 2016 ili kupisha zoezi la uhakiki. Kundi hili linajumuisha pia watumishi waliostaafu kazi kabla ya Serikali kuruhusu tena upandishaji wa vyeo kuanzia mwezi Novemba, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hatua hiyo, Serikali iliridhia na kuelekeza kuwa watumishi waliostaafu kwa aina hiyo, ambao wanastahili kulipwa madai ya malimbikizo ya mishahara ya kuanzia walivyopandishwa vyeo vyao hadi tarehe walipostaafu kazi, walipwe madai yao ya malimbikizo ya mishahara. Aidha, malipo ya madai haya yamekuwa yakifanywa na Serikali kwa wastaafu hawa kupitia kwa waliokuwa waajiri wao, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili. Kwanza naipongeza Serikali kwa majibu ya Waziri. Kwa kuwa kuna baadhi ya watumishi waliokuwa wastaafu ambao tangu tamko hilo la Serikali lilipotolewa

mpaka sasa hivi bado halijatekelezwa, je, Serikali sasa inachukua hatua gani kwa wale watekelezaji ambao walitakiwa wawatekelezee hawa wastaafu na hawajafanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wapo wastaafu ambao wamestaafu muda mrefu sana, lakini mpaka sasa hivi hawajalipwa nauli zao za kwenda kwao. Je, Serikali inachukua hatua gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwa namna anavyofuatilia masuala yanayowahusu wastaafu. Nataka tu kumhakikishia kwamba Serikali ina nia ya dhati, na ndiyo maana hadi mwaka huu wa fedha tayari wastaafu walioathirika 1,200 walishalipwa fedha zao, takribani shilingi bilioni 2.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kupitia Bunge lako, nitoe rai kwa waajiri wote kuhakikisha wanaleta taarifa za hawa wastaafu wanaodai Ofisi ya Rais, Utumishi ili tuweze ku-*process* madai yao na kupeleka Hazina kwa ajili ya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wastaafu ambao wamestaafu na nauli zao hazikulipwa; mstaafu anapostaafu ana stahiki yake, na ni taratibu na sheria kwamba alipwe nauli mpaka mahali pale alipokuwa ameajiriwa, kwa maana ya *domicile place*. Sasa naomba nichukue nafasi hii pia kutoa rai kwa waajiri wote katika taasisi za umma, kwamba kama kuna wastaafu wa aina hii wahakikishe kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha wawe wamelipa wastaafu hao nauli zao kwa sababu ni haki yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, nimekuona.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wastaafu waliokuwa wakifanya kazi Jeshi la Magereza, kuna wengine wamestaafu mwaka 2015, wengine 2019 na wengine 2021,

wamekuwa wakidai madai mengi mengi kama vile nauli za safari za kikazi, nauli za uhamisho na zile za kustaafu, lakini mpaka leo hawajalipwa na wamekuwa wakifuatilia muda wote huu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba watu wanapostaafu wachukue *interval* kidogo tu waweze kulipwa? Maana wanakuwa na *database,* wanajua kwamba hawa watu wameajiriwa kwenye idara hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza niendelee kumpongeza dada yangu, Mwalimu wangu, Mheshimiwa Matiko kwa namna anavyofuatilia mambo ya askari, hasa Magereza, na amekuwa *champion* mzuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili tunalichukua kwa uzito wake. Kwenye mwaka huu wa fedha, tayari tumetenga shilingi bilioni 207 kwa ajili ya kulipa madai haya yote. Kwa hiyo, sisi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tutawasiliana na wenzetu wa mambo ya ndani, tuone namna ya ku-*compile* haya yote ili hawa wanaodai madai yao yote waweze kulipwa kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nipo Kamati ya *LAAC*, na moja ya changamoto tunazokutana nazo kwenye Kamati hii kwenye halmashauri, mbali ya madai ya wafanyakazi ni pamoja na madai ya wastaafu ambao wamestaafu, hawajalipwa malipo yao, pamoja na malipo mbalimbali ya mizigo. Je, ni lini Serikali itakapohakikisha wanaziagiza halmashauri ziwe zinalipa wastaafu kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na pia niendelee kumpongeza Mheshimiwa Ester Bulaya, amekuwa akipigania jambo hili. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema hapa kwamba tayari tarehe 30 mwezi wa Nne tulitoa Mwongozo na Waraka kuzitaka mamlaka zote za waajiri kuhakikisha madai ya wastaafu yanalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jambo la kustaafu siyo dharura, ni jambo ambalo lipo kisheria. Kwa hiyo, niendelee tena kusisitiza kupitia Bunge hili, ule Waraka na Mwongozo tuliotoa kuwakumbusha waajiri wote waweze kuuzingatia.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Deus Sangu kwa majibu hayo ya Ofisi ya Rais, Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, aulize swali lake.

Na. 295

**Utekelezaji wa Taarifa ya Wataalamu ya Ziwa Tlawi**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, ni hatua gani imefikiwa katika kutekeleza taarifa ya wataalamu kuhusu Ziwa Tlawi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya tathmini ya kina ya hali ya mazingira ya Ziwa Tlawi na kuandaa taarifa iliyobainisha changamoto mbalimbali ambazo zinatishia uhai na uwepo wa ziwa pamoja na mifumo ya ekolojia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo ni pamoja na ziwa kujaa taka kwa maana ya tope, kupungua kwa maji yanayoingia ziwani kunakotokana na uchepushwaji wa maji yote ya Mto Endayaya ambayo yanatumika kwa shughuli za majumbani na uwepo wa magugu maji ya aina mbalimbali ndani na kandokando ya ziwa, hivyo kupunguza eneo la shughuli za uvuvi pamoja na bayoanuai iliyokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali itaendelea kutenga fedha pamoja na kutafuta fedha kupitia mifuko ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo Mfuko wa Dunia wa Hifadhi ya Mazingira *(GEF)* na Mfuko wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi *(GCF)* ili kunusuru ziwa hilo na mifumo ya ikolojia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua athari ambazo zinaweza kusababishwa na uharibifu wa Ziwa Tlawi na maziwa mengine hapa nchini, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kuziagiza Halmashauri zote nchini kuendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 Kifungu Na. 51 (4), kinachozuia uendeshaji wa shughuli za kudumu za binadamu au zenye madhara kwa mazingira ndani ya mita 60 kutoka kwenye kingo za Ziwa hilo pamoja na mito na vijito vinavyoelekeza maji katika Maziwa. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maombi mawili. Ombi langu la kwanza ni kwamba, Serikali iweke muhimu mkubwa sana wa kutafuta fedha hizo ili kunusuru Ziwa Tlawi kwa kuwa bado lina mahitaji makubwa kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu pamoja na maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, je, yupo tayari kwenda kutembelea ziwa hilo ili kuweka

uzito wa jambo hili kwa umuhimu wake pamoja na hatua mbalimbali za haraka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili sikulisikia vizuri naomba alirejee kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia, swali la pili naomba ulirudie kwa uzuri.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kutembelea Ziwa Tlawi ili kuweka uzito wake kwa ajili ya jambo hili muhimu sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ingawa moja limekuja kama ni ushauri, lakini nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshaanza mchakato wa kutafuta fedha na tayari tuna jumla ya miradi takribani 11 tumeshaiandikia. Miongoni mwa miradi hiyo ni miradi ya kusafisha mito, maziwa na maeneo mengine ambayo yameathirika kutokana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo masuala ya magugu maji na kutuama kwa tope nzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa na Waheshimiwa wengine waendelee kuwa na subira, fedha zitakapopatikana, tutahakikisha kwamba tunaanzia maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nimwambie Mheshimiwa Mbunge, kutokana na umuhimu wa jambo hili na udharura wake, nipo tayari kuambatana naye kwenda katika eneo hilo ili kuona hali

ilivyo na kuona namna ambavyo tunaweza tukawasaidia wananchi, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simai Sadiki, nimekuona.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uvuvi, kilimo, ufugaji pamoja na usafirishaji na utalii zimekuwa zikitegemea sana vyanzo vya maji, lakini kiukweli kabisa kwa kipindi hiki kumekuwa na uharibifu mkubwa mno wa vyanzo vya maji. Je, ni upi msimamo wa Serikali katika kukabiliana na hali hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simai Sadiki, Mbunge na mtumishi wa wananchi wa Jimbo la Nungwi, kwamba ni kweli kumekuwa na changamoto ambayo inasababishwa na shughuli mbalimbali za kibinadamu ambazo zinaendelea kufanyika katika vyanzo mbalimbali vya maji na hasa ukiangalia katika maeneo ya bahari kwa maana ya maeneo ya ufukwe, yapo mambo yanafanyika huko zikiwemo shughuli za ulimaji wa mwani na shughuli nyingine za uvuvi usiyokuwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba msimamo wa Serikali ni kwamba, tunawaomba sana wananchi waendelee kusimamia na kufuata sheria na taratibu zilizopo hasa hii sheria ya kuzingatia sheria ya umbali wa meta 60 kutoka usawa wa maji ili lengo na madhumuni tuweze kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji hasa maeneo haya ya bahari. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul, Mbunge wa Amani.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha kwa sasa, je, ni ipi kauli ya Serikali kutokana

na uharibifu wa miundombinu, makazi na mali za wananchi wa Zanzibar? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mvua zinazoendelea, na kwa namna moja ama nyingine zimesababisha athari kubwa hasa ya maeneo ya makazi na kuharibika kwa baadhi ya miundombinu hasa kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais tutaendelea kushirikiana, kuona namna ambavyo tunaweza tukawasaidia wananchi ili waweze kuepukana na mtihani huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa naomba kutoa wito kwamba wananchi waache kujenga na kuweka makazi yao katika maeneo ambayo yanatuama maji ili waweze kuepukana na mitihani hii hasa kipindi hiki ambacho mvua nyingi zinaendelea. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 296

**Kuunganisha Gesi ya Kupikia kwa Taasisi na Wananchi Mtwara**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kuunganisha gesi kwa ajili ya kupikia kwa Taasisi na nyumba za wananchi Mkoani Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Mtwara, Serikali imeshapeleka miundombinu ya usambazaji gesi asilia katika baadhi ya maeneo ambapo jumla ya nyumba 425 na taasisi nne zimeunganishwa na mtandao wa matumizi ya gesi asilia katika maeneo ya Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali kupitia *TPDC* ipo katika mpango wa kuunganisha nyumba zaidi ya 865 katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mtwara ambapo kuna miundombinu ya bomba la gesi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, nataka kujua, ni lini hizo nyumba 865 zitakuwa zimeunganishwa, kwa sababu wananchi wanahitaji huduma hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa huduma ya gesi ya kuunganisha kwenye bomba ina gharama nafuu kuliko ya mitungi na kasi ya kuunganisha imekuwa ndogo sana. Nataka kujua, ni nini hasa mkakati wa Serikali wa kuongeza kasi ya kuunganisha ili nyumba nyingi zipate kuunganishwa wananchi wapate nafuu, hasa wale wenye kipato cha chini? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri la kutaka kufahamu mipango ya Serikali ya kuhusiana na kuunganisha gesi asilia kwa wananchi wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa zile nyumba 865 mpaka sasa tumeshafanya usanifu wa kihandisi kwa ajili sasa ya kwenda kwenye hatua ya kuunganisha. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, muda wa hivi karibuni tutaanza zoezi hilo la kuunganisha kwa sababu tumeshafanya usanifu wa kiuhandisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la mkakati wa Serikali, tayari Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, aliekeza Wakala wetu wa Nishati Vijijini *(REA)* kuhakikisha na wao wanaweka nguvu kwa kushirikiana na *TPDC* ili tuweze kuongeza kasi ya kuunganisha gesi asilia katika nyumba hizi zilizopo Mtwara pamoja na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali imeliona, tumeshaziambia taasisi zetu mbili, Wakala wa Nishati Vijijini na Shirika la Maendeleo la Petroli wafanye kazi kwa pamoja ili washirikiane kuona kwamba kasi inaongezeka ya kuunganisha wananchi hawa wa Mtwara pamoja na Lindi vilevile. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, nimekuona.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami naomba kuuliza, je, Serikali haioni iko haja sasa ya kuunganisha gesi ndani ya masoko yetu ya Stereo, Temeke, Keko na Mtoni kwa ajili ya baba lishe na mama lishe ambao wanapika ndani ya masoko hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mkakati kupitia *TPDC* wa kuendeleza miradi ya kuunganisha gesi asilia kwa maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa masoko ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge, tumeyapokea, tutaenda kuyafanyia tathmini kuona lile ambalo linawezekana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, nilikuona.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, siku za hivi karibuni Wizara za Nishati walipita kugawa mitungi ya ruzuku na kiukweli kwenye maeneo ya vijijini kulingana na jiografia watu wachache sana walipata, je, Wizara ya Nishati, haioni haja ya kutumia ushauri huu kupeleka hiyo mitungi ya ruzuku na ikaweke kwenye Ofisi za Watendaji wa Kata ili kila mwananchi ambaye anataka kupata mtungi huo, aende na kitambulisho cha *NIDA*, afike ajiandikishe kwa wakati atakaopata, kuliko vile walivyokuwa wanafika kwenye eneo, watu wachache wanapata na baadhi ya vijiji wanakosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inaonaje kuchukua wazo hilo ili hiyo mitungi ya ruzuku iwafikie Watanzania wote? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Wakati tunaanza zoezi hili la ugawaji wa ruzuku ambapo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mkakati huu, ambapo tumeweza kupata mitungi takribani 420,000 ya ruzuku kwa ajili ya wananchi, na utaratibu tulionao ni kwamba kila mwananchi anayechukua mtungi ni lazima achukue kwa namba yake ya *NIDA*, ama kitambulisho chake cha *NIDA*. Kwa hiyo, kwa hilo tumezingatia kuhakikisha mwananchi mmoja anapata mtungi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tulikuwa tumetenga mitungi takribani 3,255 katika Wilaya, na huu ndiyo mwanzo wa kuanza utekelezaji wa mkakati wetu wa nishati safi ya kupikia, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mkakati huu ni wa miaka 10. Kwa mwaka huu wa fedha na kwa kipindi hiki tulikuwa tumetenga hii mitungi 420,000. Mkakati huu ni endelevu, tutaendelea kuja na mikakati na hatua mbalimbali za kuhakikisha tunaendelea kuwafikia wananchi wengi ili na wenyewe waanze kutumia nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mwanzo tu kazi inaendelea, kwa kipindi cha miaka 10 tutakuwa tumefikia 80% ambayo ndiyo maono ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri, Wizara ya Nishati kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, aulize swali lake.

Na. 297

**Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano Kata za Vwawa**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa Serikali wa kujenga minara ya simu kwenye Kata ya Ipunga, Nyimbili na Isalalo ili kuboresha mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Nyimbili kuna minara miwili iliyojengwa kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)*. Mnara wa kwanza ni wa Kampuni ya Honora *(Yas)* ambayo ilikuwa *TIGO* na Mnara wa pili ni wa Kampuni ya *Vodacom* na minara hii yote imekamilika na inatoa huduma kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kata ya Ipunga na Isalalo bado hazijapata fursa ya kunufaika na miradi ya Serikali ya kuboresha huduma za Mawasiliano, hivyo kupitia *UCSAF,* Kata hizi zitafanyiwa tathmini ili kubaini changamoto za mawasiliano ya simu katika maeneo tajwa na kubaini mahitaji halisi na kuyaingiza katika

zabuni zitakazotangazwa kulingana na upatikanaji wa fedha hususan katika mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Serikali, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa Kata ya Ipunga na Kata ya Isalalo Serikali imedai kwamba bado hazijanufaika na upatikanaji wa huduma za simu za uhakika. Ni lini sasa utafiti huo utakamilika ili wananchi wale ambao wamesubiri kwa muda mrefu waweze kunufaika na mawasiliano ya simu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Pamoja na kwamba Kata ya Nyimbili mmejenga minara miwili ambayo kwa kweli ninaipongeza Serikali, lakini yapo maeneo kutokana na jiografia ya Kata ya Nyimbili yapo bondeni na mengine yapo, kuna milima mingi, hakuna mawasiliano ya simu kwa uhakika katika maeneo kama Hantesya, maeneo kama Shititi, Nyanyi na Namwangwa yote hayapati mawasiliano. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanafikiwa vizuri na mawasiliano yanapatikana kwa wakati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nipokee shukurani za Mheshimiwa Japhet Hasunga na wewe pia nikupongeze kwa ufuatiliaji mzuri na nikuhakikishie tu kwamba huu utafiti tutahakikisha unafanyika katika mwaka huu wa fedha ili mwaka ujao wa fedha kadri pesa inavyopatikana mapema sana wananchi hawa waweze kupelekewa huduma ya mawasiliano kwa sababu ndiyo hamu ya Mheshimiwa Rais wetu kuona kwamba vijiji vyote vinafikiwa kupata mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali katika mazingira haya yenye miinuko tayari wataalamu wetu wanaendelea kufanyia kazi, kama ni ku-*upgrade* na kuona kwamba *signals* ziwe za mfumo mzuri labda wa *3G* watafanya, lakini maeneo ambayo haiwezekani, basi minara mipya itapelekwa, na tayari tuna ongezeko la *bunch* ya minara zaidi ya 200, *TTCL* pia watakwenda kwenye maeneo haya yote ambayo siyo rafiki wa biashara lakini wananchi wetu ambao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anawahudumia wataweza kufikiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, nilikuona.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Jimbo la Karagwe, Kata ya Bweranyange, Kijiji cha Muguruka hakuna mawasiliano kabisa. Ningependa kujua ni lini Serikali itapeleka mawasiliano katika Kijiji hicho? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na maeneo haya ya Karagwe. Kadri fedha inavyopatikana, tutahakikisha maeneo haya yote uliyoyataja tutaweza kuyafikia. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Mkoa wa Njombe, Jimbo la Makambako, Kata ya Lyamkena maeneo ya Kiumba Kati, Makatani na Muungano, lini Serikali itajenga minara ili sehemu hii iweze kupatiawa mawasiliano, maana mawasiliano hakuna kabisa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya ya Njombe, Makambako Kata zote alizozitaja Mheshimiwa Neema, tayari Mheshimiwa Jerry, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, amewaagiza Wataalam, wameenda huko, wanaendelea kufanya tafiti na tafiti zitakapokamilika, Kata hizi zote zitakuwa wanufaika. Hivyo, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge katika ufuatiliaji huu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, nilikuona.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Kata ya Maroroni katika Kijiji cha Samaria na Kata ya Uwiro, Kisimiri Juu kuna changamoto kubwa sana ya mawasiliano ya simu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga minara ya mawasiliano katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Samaria na Kijiji hiki jirani ambavyo amevitaja Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, nimhakikishie kwamba mkakati wa Serikali ni kuhakikisha tunavifikia hivi vijiji vyote na kujenga minara ya mawasiliano na wananchi wote waweze kunufaika na hali nzuri ya mawasiliano, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aziza, nilikuona na Mheshimiwa Mwanakhamis.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa upo utapeli mkubwa ambao wanafanyiwa wananchi kupitia minara hii na kuwalaghai kuwa watakapotoa pesa watawekewa minara na watu hao ni matapeli, je, Serikali ina kauli gani ya kuwaelimisha wananchi ili wasizidi kutapeliwa na wananchi hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwaambia wananchi wote wa Tanzania kwamba, ujenzi wa minara unafanywa na wataalam ambao wapo, wana vibali kamili kutoka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Naomba wale wote ambao wanafika huko, huwa wanaongozana na Watendaji wetu, wataweza kuonesha vitambulisho, lakini vilevile wawatumie ninyi Waheshimiwa Wabunge kuhakiki kama kweli hao waliokwenda ni wataalamu waliopata vibali kutoka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanakhamis nilikutaja, au Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kata za Kilimarondo, Kipara Mtua, Mtua na Stesheni maeneo ya Mchangani hali ya mawasiliano ni ngumu. Je, ni lini Serikali itajenga minara kwenye Kata hizi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kwamba kata hizi alizozitaja naomba tu nimtoe hofu kwamba kadri fedha inavyopatikana mwaka ujao wa fedha 2025/2026 tutahakikisha maeneo haya na yenyewe tunayafikia na minara inajengwa na wananchi wanakwenda kunufaika na hali nzuri ya mawasiliano ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate, nimekuona.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Makao Makuu ya Wilaya ya Kyerwa kuna shida kubwa ya mtandao na

shughuli nyingi zinashindwa kufanyika. Je, ni lini Serikali itaboresha mtandao pale uweze kufanya kazi vizuri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makao Makuu ya Kyerwa, kwa sababu ni Makao Makuu, ninaamini minara ipo. Kwa hiyo, tutakachokifanya ni kuwatuma watoa huduma ambao tayari wanafanya huduma pale, wakaboreshe kama ni ku-*upgrade* kutoka *2G, 3G, 4G* ili iweze kupatikana mawasiliano ya uhakika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Maryprisca Mahundi kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, aulize swali lake.

Na. 298

**Ujenzi wa Kivuko cha Abiria – Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa kivuko cha abiria kutoka Kakukuru kwenda Gana – Ukerewe kitaanza kujengwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia wakala wa ufundi na umeme *TEMESA* katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 inaendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko

mbalimbali nchini. Aidha, baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa daraja la JPM, yaani pale Kigongo Busisi Mkoani Mwanza, vivuko vinavyotoa huduma katika eneo hilo vitagawanywa katika maeneo yenye uhitaji wa vivuko katika Mkoa wa Mwanza ikiwa ni pamoja na Kakukuru, kwenda Gana Wilayani Ukerewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali na nina maswali mawili ya nyongeza. Naipongeza Serikali kwa mpango huo na ninatambua kuna vivuko vingine vinafanyiwa maboresho kama kivuko cha MV Nyerere na kadhalika. Vivuko hivi vikishakamilika au vikihamishiwa Ukerewe kunatakiwa kuwe na magati ambayo yatasaidia vivuko hivi kutua, lakini sioni dalili zozote za maandalizi ya magati kwenye eneo la Gana, Kakukuru, Lutale wala Ilugwa. Ni nini mkakati wa Serikali kuanza maandalizi ya magati kwenye maeneo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwenye bajeti ya mwaka 2024 tulitenga pesa kwa ajili ya kujenga mabanda ya abiria kusubiri kwenye eneo la Bugolola, Bwisya pamoja na Bukimwi lakini sioni kazi yoyote inayoendelea. Ni nini mpango wa Serikali kujenga mabanda haya ya abiria kusubiri?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala haya ya vivuko na hasa katika Jimbo lake la Ukerewe ambalo linaunganisha sehemu kubwa na vivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magati, eneo hili ambalo nalisema ni sehemu ambayo kivuko kipya kinakwenda. Kwa hiyo, tunachofanya sasa hivi, ni usanifu ili kujenga magati ambayo yatahudumia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vivuko vyote ambavyo vinafanya kazi, na tunajenga vivuko vipya, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba tayari magati yanaendelea kujengwa na yapo kwenye hatua za mwisho kabisa. Kwa hiyo, sasa hivi tunachofanya katika maeneo haya ambayo ni mapya, sasa hivi tupo kwenye usanifu ili tuweze kuanza kujenga magati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika swali lake la pili kuhusu mabanda, tumetenga bajeti katika mwaka huu 2025, wakati tunaendelea na ujenzi wa vivuko vipya. Pia tuna mpango wa kujenga mabanda, na kazi hii Wizara imeipa *TBA* ambao wapo mwishoni kabisa kukamilisha usanifu wa mabanda kwa sababu haya mabanda hayafanani kati ya kituo na kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mpango huo upo na tupo hatua za mwisho za usanifu na baada ya hapo tutaanza ujenzi pia wa mabanda ili kutoa huduma katika maeneo hayo ya vivuko. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage, nimekuona.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mkoa wa Kagera baada ya kuona mafanikio ya ujenzi wa daraja la Kigongo Busisi, tumeomba Wizarani kwamba, baadhi ya vivuko vipelekwe Magarini ili kutoa huduma sehemu za Ikuza na Mazinga. Pia kivuko kingine kipelekwe Rubafu ili kuunganisha Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri katika hivyo vivuko, ni vingapi ameainisha kwamba vitapelekwa kwenye maeneo hayo mawili ambayo yana uhitaji wa vivuko?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, vivuko vilivyokuwa vinatoa huduma pale Kigongo - Busisi ndiyo vivuko vikubwa katika Ziwa Victoria na vitakapopelekwa

kwenye maeneo, maana yake, kama kulikuwa na vivuko viwili, vitahamishiwa kwenye maeneo mengine kwa sababu tulikuwa na vivuko vikubwa vitatu pale Misungwi, Sengerema na MV. Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna kivuko kilikuwa na vivuko vitatu, maana yake vitagawanywa kwenda kwenye hatua tatu. Tunachokifanya sasa hivi ni tathmini ikiwa ni pamoja na mawazo ya Mheshimiwa Mwijage, kama kutakuwa na kivuko kikubwa, hivyo chenye sifa ya kuunganisha sisi na Uganda, basi tutafanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, nilikuona.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, kivuko cha MV Ilemela kilitengenezwa kwa ajili yaku-*save* kisiwa cha *Base* pamoja na Kayenze, lakini kutokana na uhitaji, kivuko kile kilianza kufanya kazi katika Kisiwa cha Bukimwi na kwa sasa mahitaji yamekuwa ni makubwa kiasi kwamba kivuko kile kimezidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni ipo haja, aidha, kuweka vivuko viwili viwe vinapishana au kuongeza *root* ili kuweza kuondoa adha inayopatikana sasa, maana kuna magari yanaachwa, watu wanaachwa kwa sababu kivuko kimezidiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Ilemela kuhusu swali lake. Nataka nimhakikishie kwamba, bahati nzuri nilishatembelea eneo hilo la Kayenze ambapo hicho kivuko kinaanza, na tunapokuwa tunaboresha vivuko imeonekana kwamba idadi ya watu inaongezeka sana kwenye vivuko. Ndiyo maana pamoja na kukamilika kwa daraja la Kigongo - Busisi tutaongeza hivyo vivuko kwenda kwenye sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, katika Awamu hii ya Sita tunajenga vivuko vitano vipya kabisa katika Ziwa Victoria ambapo tupo kwenye zaidi ya 85% kwenda 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivyo vivuko vipya pia vitakapokamilika vitatoa nafasi ya vivuko vidogo kwenda kuhudumia kwenye sehemu nyingine. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, pia tutafanya *study* ambayo tunaendelea kuifanya kwa sababu tumeona watu wanaongezeka, magari yanabaki, tuone ama kuongeza kivuko kikubwa ama kuongeza kituo kuwa cha pili ili viwe vinapishana katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege, nimekuona.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kisiwa cha Nafuba katika Jimbo la Mwibara ni mojawapo ya sekta kubwa sana ya biashara ya samaki jimboni. Je, ni lini Serikali itajenga kivuko cha kwenda Nafuba kutoka Nasimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRII WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu maelekezo kwa Mtendaji Mkuu wa *TEMESA*, kwa sababu kazi yao ni kufanya tathmini na kufanya utafiti, aende akafanye utafiti na kuona kivuko kipi kitafaa na wapi kivuko kinaweza kujengwa ili kutoa huduma hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameiomba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, nilikuona.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, wananchi wa Kata za Kwagunda, Mnyuzi na Hari wanashindwa kuvuka kutokea Korogwe kwa sababu ya daraja ambalo limekatika kwa muda sasa. Ni upi mpango wa Serikali juu ya daraja hili la Urengera ambalo limekatika zaidi ya mwaka mmoja?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mnzava kwamba, ni kweli kwamba vivuko tunavichukulia kama ni daraja ambalo linatembea. Kwa hiyo, alichouliza ni daraja, japo tunaongelea vivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja lile lilikatika katika kipindi hiki na Wizara imelichukulia kama ni dharura. Mheshimiwa Waziri alishatoa maelekezo, na hivi tunavyoongea, sasa hivi tupo kwenye hatua za mwisho kupata mkandarasi ili aweze kulijenga pia kwa udharura wake kama ilivyotokea kwa hilo daraja la Mheshimiwa Mnzava.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Godfrey Kasekenya kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Ujenzi. Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Oran Manase Njenza, Mbunge wa Mbeya Vijijini aulize swali lake.

Na. 299

**Miradi ya Ubia Sekta ya Umma na Binafsi**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza: -

Je, Serikali imewezesha miradi mingapi kwa utaratibu wa ubia wa Serikali na Sekta Binafsi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 10A cha Sheria ya *PPP* Sura Na.103 kilianzisha Mfuko wa Uwezeshaji Ubia kwa lengo la kuziwezesha Mamlaka za Serikali kuandaa na kutekeleza miradi ya PPP. Aidha, Kifungu cha 5(1) cha Sheria hiyo imekipa Kituo cha Ubia *(PPP Centre)* jukumu la kutoa usaidizi wa kiufundi kwa Mamlaka za Serikali na Sekta Binafsi wakati wa uibuaji, maandalizi na utekelezaji wa miradi ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP)*.

Hadi Aprili, 2025 jumla ya miradi 80 imewezeshwa na Serikali, na ipo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Miradi mitatu ipo katika hatua ya utekelezaji;
(ii) Miradi minne ipo katika hatua ya majadiliano;
(iii) Miradi miwili ipo katika hatua ya ununuzi;
(iv) Miradi 26 ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu;
(v) Miradi 13 ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu wa awali; na
(vi) Miradi 32 ipo katika hatua ya andiko dhana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Manase Njenza.

**MHE. ORAN M. NJENZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali, na kwa kuwa kuna miradi mingi ya maendeleo yenye mvuto wa kutekelezwa na uwekezaji wa sekta binafsi kwa njia ya *PPP*; na kwa kuwa sheria ya bajeti kifungu 7(3) kinaelekeza Serikali kutotenga bajeti kwenye miradi ambayo ina mvuto wa *PPP*, swali namba moja: Je, imejipanga vipi Serikali kutekeleza miradi ya barabara yenye mvuto na sekta binafsi ikiwemo barabara ya Igawa, Mbeya, Tunduma pamoja na *bypass* ya Uyole Songwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali imejipanga vipi kuhamasisha sekta binafsi kuingia ubia ili iweze kutekeleza ujenzi mpya na uboreshaji wa reli ya *TAZARA* ikiwemo na uendeshaji?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Njeza kwa namna anavyofuatilia katika suala zima la uwekezaji kwa utaratibu wa *PPP*. Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi na kuwaita kabisa kuandaa miradi tofauti tofauti kwa lengo la kushiriki katika miradi ya *PPP* na miradi yao ikionekana inafaa katika utaratibu huo, basi inafanyiwa kazi na hatimaye kufika kuweka saini na utekelezaji wa miradi tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kipande cha Igawa alichokitaja Mheshimiwa Njenza, Igawa – Tunduma kwa sasa yupo mshiriki wa sekta binafsi ambaye anaandaa mradi kwa kupitia utaratibu wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, Serikali ya Tanzania na Zambia zipo kwenye majadiliano kati yake na Serikali ya China, na kwa sasa imefika hatua nzuri, wakati wowote Serikali ya Zambia na Tanzania pamoja na Serikali ya China zitaweka saini kupitia kampuni ya *CECC*, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri, Wizara ya Fedha kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 300

**Wavuvi wa Kigamboni Kupewa Vifaa vya Kisasa**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuwawezesha wavuvi wa Kigamboni kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vya uvuvi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatekeleza mradi wa kuwawezesha wananchi kupitia dirisha la *ECF/IMF* kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* tangu mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo kwa awamu ya kwanza jumla ya boti 160 zenye thamani ya shilingi bilioni 11.5 zilitolewa kwa wanufaika 3,163.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hao, idadi ya wanawake ni 1,008, na wanaume 2,155, ambapo, Kikundi cha *Bright Fisheries* chenye wananchi saba kutoka Kigamboni kilinufaika kwa kupatiwa boti ya kisasa ya uvuvi yenye ukubwa wa mita 14 na vifaa vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa bajeti wa mwaka 2025/2026, Wizara imetenga kiasi cha shilingi bilioni 9.5 kwa ajili ya kuendelea kuwezesha wavuvi kupata boti na vifaa bora vya uvuvi kwa mkopo wenye masharti nafuu wakiwemo wananchi wa Kigamboni. Aidha, utoaji wa boti hizo ni endelevu, hivyo Wizara inahamasisha wavuvi na vikundi vya wavuvi kuendelea kuomba mikopo hiyo ili waweze kunufaika na fursa hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Azan.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina swali moja la nyongeza, je, ni lini Serikali itapeleka boti kwenye Ziwa Nyasa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa Nyasa tayari Serikali imeshapeleka boti. Kuna vikundi viwili ambavyo viliomba boti na jumla ya boti tano tumeshapeleka katika Ziwa Nyasa, lakini tunaendelea kupokea maombi, tupo tayari kuendelea kuongeza boti katika eneo hilo la Ziwa Nyasa.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Mbunge. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Amina Ally Mzee, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 301

**Kujumuisha Mada ya Ukatili wa Kijinsia kwenye Masomo Nchini**

**MHE. AMINA ALI MZEE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kujumuisha Mada ya ukatili wa kijinsia kwenye Masomo kuanzia Shule za Msingi nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya maboresho ya mitaala katika ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu mwaka 2023 ili kuhakikisha kuwa mitaala yetu inaendana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mitaala iliyoboreshwa, ukatili wa kijinsia pamoja na masuala mengine mtambuka yamechopekwa katika masomo mbalimbali katika ngazi zote za elimu. Aidha, somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili ambalo ni somo la lazima kwa wanafunzi wote kuanzia elimu ya Awali mpaka Kidato cha Sita lina mada mahususi zinazolenga kujenga umahiri wa mwanafunzi katika kuelewa na kupinga ukatili wa kijinsia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa mpango mzuri wa kuboresha mitaala ya elimu. Nauliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu juu ya suala zima la kuwajengea uelewa juu ya ukatili wa kijinsia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali inahakikishaje kushirikiana na Wizara mbalimbali juu ya kutoa elimu juu ya suala zima la ukatili wa kijinsia?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu Wizara na Serikali kwa ujumla tumeendelea kutoa elimu kwa jamii pamoja na wanafunzi kwa ujumla. Naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Taasisi yetu ya Elimu Tanzania (TET) imeanzisha kituo maalum kabisa cha *TV* kinachohusiana na masuala ya kutoa elimu kwa wanafunzi pamoja na jamii kwa ujumla katika maeneo hasa hasa ya masuala ya mitaala yetu kwa maana ya shule katika masomo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *TV* hii imetusaidia kufundisha zile stadi za maisha na stadi za kazi, lakini sambamba na hilo imekuwa ni *TV* ambayo inawezesha kutoa hii elimu ya ukatili wa kijinsia kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, elimu hii inaendelea, lakini ipo katika vituo vyote vya televisheni kwa kadri unavyopata muda, basi elimu hii imekuwa ikitolewa kwa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili kuhusiana na suala la kushirikiana ama mashirikiano na sekta nyingine au Wizara nyingine, ni kweli suala hili ni suala mtambuka. Kwa hiyo, sisi Wizara ya Elimu tukishirikiana na wenzetu wa TAMISEMI, Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, na Wizara ya Mambo ya Ndani tumekuwa tukishirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba elimu hii inawafikia Watanzania wote au jamii yote kwa ujumla na hasa kwa kuanzisha madawati mbalimbali katika maeneo tofauti tofauti ambayo hususan yanahusika na masuala ya ukatili wa kijinsia. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Omari Kipanga kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale aulize swali lake.

Na. 302

**Kusambaza Maji Kata za Jimbo la Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza maji Kata za Kaboha, Shabaka, Nyang'hwale, Nyaburanda, Mwingiro, Nyugwa ili kuondoa shida ya maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji katika Wilaya ya Nyang'hwale inapatikana kwa baadhi ya maeneo ya Kata za Kaboha, Shabaka, Nyang'hwale, Nyaburanda, Mwingiro pamoja na Nyugwa kupitia visima virefu tisa, visima vya pampu za mkono saba pamoja na mtandano wa bomba. Katika kutatua changamoto hiyo, Serikali inaendelea na mpango wa muda mfupi wa kuchimba visima na kujenga miundombinu rahisi ya kutolea huduma katika baadhi ya vijiji vya kata hizo kupitia programu mbalimbali ikiwemo Programu Maalum ya Uchimbaji wa Visima 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utafutaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango wa muda mrefu wa miradi mikubwa ya kimkakati inayohusisha Upanuzi wa Mradi wa Maji *(JWPP)* kwenda vijiji vyote vya Kata ya Kaboha, pamoja na Upanuzi wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kutoka Nyijundu kwenda Nyang'hwale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali kwa baadhi ya kata ambazo amezitaja Kaboha, Shabaka,

Nyang'hwale, Nyaburanda, Mwingiro na Nyugwa kwa kuendelea kusambaza maji kupitia visima virefu tisa na visima saba vya pampu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa tumepitisha Bajeti ya Wizara ya Maji na kutengewa fedha juzi kwa ajili ya kwenda kusambaza maji kupitia Mradi wa *JWPP,* je, Serikali iko tayari kupeleka wakandarasi kwenye kila kata baada ya fedha hizo kutoka ili waweze kuifanya kazi hiyo kwa haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nataka kujua, Mfuko wa Maji mgawanyo wake ukoje kati ya mjini na vijijini? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natumia fursa hii kumpongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Hussein Nassor, Mbunge wa Nyang'hwale kwa kazi nzuri ya kuwatetea wananchi wa Nyang'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendelea kushirikiana naye kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto za huduma ya maji katika Jimbo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameshauri na tumeupokea ushauri wake. Sambamba na hilo, tutafanya tathmini ili kuona kama kutakuwa na uhitaji wa kupeleka wakandarasi wengi katika eneo hilo. Lengo ni kwamba, mradi uweze kukamilika kwa wakati. Tutafanya hivyo kwa kuzingatia mapana yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa Maji ambao unafanya kazi chini ya Sheria ya Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019, mgawanyo wa fedha hizi upo kikanuni. Tuna kanuni ambazo Mheshimiwa Waziri wa Maji alishasaini ambapo inaonesha kabisa kwamba tutakuwa na 60% ambayo itaenda kwa ajili ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa na 29% ambayo itaenda kwa ajili ya mjini na tutakuwa na 10% kwa ajili ya kulinda vyanzo vyetu vya maji. Vilevile, tutakuwa na asilimia moja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata vifaa kwa ajili ya kupima ubora wa maji ili maji yatakayowafikia wananchi yawafikie katika ubora unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji kwa majibu hayo. Tunamalizia na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 303

**Kuwagawia Wananchi Eneo la Pori la Kigosi**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwagawia Wananchi sehemu ya eneo la Pori la Kigosi ili litumike kwa shughuli za kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Misitu Sura Na. 323, inaruhusu baadhi ya shughuli za kiuchumi kufanyika kwenye maeneo ya hifadhi za misitu kwa kuzingatia mahitaji ya uhifadhi. Aidha, Serikali imetoa fursa kwa wananchi kufanya shughuli za kiuchumi katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na ufugaji wa nyuki, uchimbaji wa madini, uvuvi, utalii wa aina mbalimbali, utafiti na mafunzo ambapo hadi sasa wafugaji nyuki wapatao 3,061 kutoka katika vijiji 105 wamepewa vibali vya kuingia ndani ya hifadhi na wameweza kutundika mizinga ya nyuki ipatayo 585,713.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali kupitia Wizara ya Madini inaendelea na uratibu wa kutoa vibali kwa shughuli za madini kwa kuzingatia tafiti za madini ambapo kazi hiyo inafanyika kwa kuzingatia uhifadhi kwa mujibu wa Sheria za Misitu, Madini na Mazingira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na pia nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Iponya, Kijiji cha Sango; Kata ya Isebya, Kijiji cha Nyashinge; na Kata ya Ilolwangulu, Kijiji cha Kanangwe; nimeyataja haya maeneo, je, yuko tayari kutuma timu ya Wizara yake ije iangalie ili ione kama yanaruhusiwa ili wananchi waendelee kufanya shughuli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wilaya ya Mbogwe pamoja na wilaya ya jirani, sisi kule bado tunatumia kuni na wananchi huwa tunawapa semina kulingana na vibali kama alivyosema ikiwemo kukata mkaa lakini kumekuwa na askari ambao sio waaminifu sana, wakimwona mtu tu na mkaa wanamkimbiza, wanamfanyia fujo na kumuumiza. Je, ni maelekezo gani anayatoa kama Waziri mwenye Wizara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko tayari kutuma timu kwenda kushirikiana na uongozi wa wilaya katika maeneo haya ili kufanya hiyo tathmini na baadaye tutaleta majibu kwa Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili, uchomaji wa mkaa una taratibu na sheria ambazo unazingatiwa. Natoa maelekezo kwa wahifadhi wetu katika maeneo yote nchini

kuzingatia sheria na taratibu zinavyotaka katika kusimamia jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umefikia mwisho. Hapa nina matangazo ya wageni ambao wako Bungeni asubuhi hii.

Kuna wageni ambao wamekaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Prof. Adolf Faustine Mkenda, ambaye ni Waziri wetu wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambaye ni Ndugu Judith Kiwale, Mwenyekiti wa Washirika wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kuna mgeni wa Mheshimiwa Andrea Mathew Kundo, Naibu Waziri wa Maji ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni wapigakura wake kutoka Babati Vijijini Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni watano wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, wadau wa asasi za elimu na haki elimu kwa watu wenye ulemavu, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mtoto wake kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Viongozi wa Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko kutoka Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mshindi wa Tuzo Mbili za *Samia Kalamu Awards*. Tuzo ya kwanza ni kuhusu Mwandishi wa Habari Mahiri za Ujenzi, na tuzo ya pili ni Chombo Bora Mtandaoni cha Wazo Huru Media kwa utoaji wa taarifa zenye maudhui yenye weledi na ufanisi. Huyu ni Ndugu Mathias Canal kutoka Dodoma. Karibu sana katika Bunge letu na hongera kwa tuzo hizo. *(Makofi)*

Kuna wageni 13 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Wachungaji na Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wanamaombi wetu. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni ambao wametembelea Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Wapo viongozi saba wa Taasisi ya Kuinua Kiwango cha Elimu Nchini *(TASESO)* kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Ndugu Deus Lugaila, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 31 na Walimu sita wa Darasa la Sita na la Saba kutoka Shule ya Msingi Papango iliyopo Kata ya Mlimba, Halmashauri ya Kilombero Mkoa wa Morogoro, karibuni sana wanafunzi wa walimu wetu kutoka huko Morogoro. *(Makofi)*

Wanafunzi 80 na Walimu watano wa Shule ya Msingi *Father* Silvio Pasqual kutoka Mafinga Mkoa wa Iringa. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko Iringa. *(Makofi)*

Pia, tuna wanafunzi 100 na Walimu sita wa Shule ya Msingi Maria De Mattias ya Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu wote kwenye Bunge letu kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, ajiandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Pia nampongeza Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda kwa kazi kubwa. Nampongeza pia Naibu Waziri, Omari Qs Kipanga; Katibu Mkuu, Dada yetu Profesa Carolyne Nombo; Naibu Katibu Mkuu na timu nzima kwa kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais, na nifanye rejea ndogo ya hotuba yake ambayo aliiwasilisha hapa Bungeni Tarehe 22 Aprili, 2021 kuhusu mambo ya elimu. Naomba nisome, ninukuu, Mheshimiwa Rais alisema, "Serikali itajielekeza kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 na kufanya marekebisho kwa mitaala iliyopo ili ielekezwe kwenye kutoa elimu ujuzi. Tunataka mitaala yetu ijielekeze kwenye kutoa elimu ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na soko la ajira." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameyaishi kwa vitendo. Hivi tunavyozungumza, tunao mtaala mpya ambao pia umeanza kazi. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunayo sera mpya, Marekebisho ya Sera ya Mwaka 2023 ambayo pia yeye mwenyewe aliyazindua.

Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuishia hapo, sasa hivi tumejenga miundombinu ya shule. Tumejenga shule mpya za sekondari na msingi ili kukidhi mahitaji ya sera hii na kukidhi mahitaji ya mtaala huu. Hakuishia hapo pia, sasa hivi tunazungumza, na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema, zinajengwa shule za amali zaidi ya 103, shule 29 ni za uhandisi pamoja na shule moja iko Singida Mjini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa sana ambalo tulilizungumza na tumelizungumza kwa nguvu ni juu ya vitabu. Tumesikiliza na hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa kwamba, sasa uwiano utakuwa ni kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja. Hili ni jambo ambalo hatukulitarajia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni mafanikio ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekujanayo na yamenifanya niweze kukumbuka na kufanya rejea ndogo ya mwanasiasa nguli, Margaret Hilda Thatcher aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza ambaye pia alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza mwanamke na ndio Waziri Mkuu aliyekaa kwa muda mrefu hapo Uingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Margaret Thatcher alisema, *"If you want something said, ask a man, but if you want something done, ask a woman."* Kwa tafsiri yangu, ukitaka taarifa ya maneno mwulize mwanaume, lakini ukitaka taarifa ya vitendo mwulize mwanamke. Sifa hizi anazipata Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuishia hapo, Nelson Mandela naye alisema. Nelson Mandela aliamua kugusa kwenye eneo la elimu. Napenda pia ninukuu kwenye eneo lake ambalo Nelson

Mandela amezungumza. *"Education is the most powerful weapon which you can use to change the world."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hii ya ujuzi ambayo tumeianzisha, ndiyo elimu ambayo tunaitumia kama *tool* ya kuwafanya vijana waweze kujitegemea. Nataka niendelee kuipongeza Serikali, katika kipindi chote hiki ambacho sisi tulitaka kuwepo na mabadiliko ya elimu, iwe elimu ya ujuzi na imeweza kutekeleza jukumu hili. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kumpongeza Mheshimiwa Waziri. Nimesoma hotuba yake, nimesikiliza vizuri na nimeisoma randama vizuri, nimeona kwa kweli ameandaa hotuba nzuri na randama imeshiba. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo machache ambayo natamani kuishauri Serikali. Moja, ni uhaba wa walimu. Taarifa yetu inatueleza tunao uhaba wa walimu zaidi ya walimu 268,000, siyo jambo jepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa karibuni tumeajiri walimu 14,000. Moja ya eneo ambalo nami lilinipa masikitiko makubwa, tumeenda kuwaajiri walimu kwa kuwapa mtihani, ambapo unampa mwalimu ambaye amesoma *methodology*. Mwalimu anapaswa apimwe darasani. Hawezi kupimwa kwa mtihani ambao anapewa ili apate *marks* hizo. Eneo hili kwa kweli hata mimi sikuwa nimelipenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishauri Serikali nini? Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Juni, 2023 walitoa mwongozo wa ajira ya kujitolea, kwa watu kujitolea, lakini mwongozo huu mpaka sasa haujatekelezeka. Kwa nini hautekelezeki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia baadhi ya maeneo, la kwanza ni mkataba ambao umewekwa wa mwalimu huyo anayejitolea anaingia mkataba na nani? Kwa sababu pale kwenye mwongozo inaonesha mkuu wa shule ama mwalimu mkuu.

Pia, unaonesha Kamati ama bodi ya shule. Tayari unamweka mwalimu ana-*hang,* lakini anatakiwa alipwe posho na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake tunasema, moja ya chanzo ni mapato ya ndani ya halmashauri. Chanzo kingine tumesema wazazi, na chanzo kingine ni wadau mbalimbali. Tukiliweka hivi, tutakuwa hatuna nia njema ya kuhakikisha walimu hawa wanaojitolea wanaweza kutusaidia na kupata hicho kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishauri Serikali kwenye eneo hili. Mkataba unapaswa uingiwe na Mkurugenzi. Mwenye kutangaza ajira ya walimu kujitolea, anapaswa kutangaza Mkurugenzi kwani ndiye mwajiri wa watumishi na ndiye anayewasimamia walimu walioko huko wawe wanajitolea au hawajitolei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi ndio atangaze nafasi na ndio aingie mkataba. Ukiingia mkataba tayari unatoa fursa ya mapato ya ndani na sisi Baraza la Madiwani kujua katika bajeti yetu, tunao walimu kadhaa ambao wamejitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, rudi nenda ukarekebishe mwongozo huu wa walimu kujitolea. Msingi wa kufanya hivi, maana yake kundi hili la walimu walioko mtaani zaidi ya 200,000 wapate fursa ya kwenda kujitolea. Tupunguze hili *gap* la watumishi shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunataka kufanya hivyo? Hii itatusaidia. Leo tunayo *PEPMIS* ambayo inasaidia watumishi walioajiriwa. Mkurugenzi atatengeneza utaratibu wake wa kuwaingiza waliojitolea kwenye mfumo. Hii itawasaidia Wizara ya Utumishi, badala ya kuja kutoa mtihani kwa mwalimu ambaye ni *professional*, maana yake itakachofanya sasa ni kuangalia *performance* ya walimu waliojitolea kwenye shule na kuweza kuwaajiri kwa wepesi badala ya kutumia huu mfumo ambao tunautumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, sasa hivi tumewekeza kwenye ufundi ambalo ni jambo jema sana. Nami nataka kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Tunajenga shule 103 za amali, *VETA* zaidi ya 64 na 65 kwa maana ya *VETA* ile ya Songwe. Pia, nimeona kazi ni nzuri, ametenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 200 kwa ajili ya *VETA*. Ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha ni kwa ajili ya ufundi, uendeshaji na ni kwa ajili ya watumishi. Hili jambo ni zuri. Hata hivyo, ukifanya mchanganuo wa bajeti nzima kwenye hili eneo la ufundi ni asilimia 13 tu ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa vyuo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hii ni ndogo sana. Nataka kuiomba Serikali, kama kweli sisi tumeweka dira ya maendeleo yetu iwe kumwandaa kijana kuwa na ujuzi, ni lazima tuongeze fedha kwenye eneo hili ili liweze kutoa mwongozo, usaidie kupata walimu wa kutosha na tupate vifaa vya kutosha. Pia, fedha hii iliyopo ni lazima itoke kwa wakati. Shule zinajengwa, zinaisha, lakini mpaka sasa tunavyozungumza hakuna vifaa na hakuna walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sasa mmeenda kule Mtwara mmeona kwamba sasa tuanzishe kile chuo kiwe chuo kikuu na watu waweze kusoma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili ndiyo msingi wetu wa maendeleo. Tunataka vijana waingie darasani na waweze kupata ufundi. Sasa kama hatujajiandaa kuleta vifaa mapema, tutakuwa tumeshindwa kutekeleza wajibu huu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, sijaona *projection* ya Serikali hapa ya tunakoelekea. Mwaka 2028 tutakuwa na vijana wa *form one* ambao wametoka darasa la sita na waliotoka darasa la saba. Mikondo yote miwili inaingia *form one* 2028. Sasa ikiingia *form one* mwaka 2028, ni yapi maandalizi ya Serikali ya kuongeza miundombinu ya madarasa na kuongeza watumishi? Yako wapi maandalizi hayo ya Serikali? Hatujayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *projection* inatakiwa ifanyike leo. Tukisubiri baadaye, tutarudi kama tulikotoka huko. Tunaanza kutumia nguvu kuanzisha madarasa na shule na matokeo yake tutashindwa kufikia malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, mwaka 2025 umeisha, huu tunaenda 2026 na mwaka unaofuata tuweke maandalizi mazuri ya 2028 tunawapokeaje hao watoto waliomaliza darasa la sita na waliomaliza darasa la saba wasije wakaenda kwa wingi halafu wakakuta bado tuna tatizo lile lile la walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna walimu zaidi ya 268,000 ambao wanatakiwa waingie. Ukifika huko inawezekana walimu wakafika zaidi ya 500,000 mpaka 700,000 hawawezi kufundishika na itakuwa tumetoa elimu ambayo haina msingi wa kuwasaidia hawa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko mradi, katika hii miradi yetu mikubwa; tuna Mradi wa *BOOST,* tuna Mradi wa *SEQUIP* na tuna Mradi wa *EP4R* (Lipa Kulingana na Matokeo). Miradi hii sehemu kubwa kwenye halmashauri imefanya vizuri, lakini zipo halmashauri ambazo miradi hii haijafanya vizuri na haijafanya vizuri kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ina fedha nyingi, isipofanya vizuri, maana yake ni kwamba tunapoteza fedha nyingi za wafadhili na hii inatusaidia, kwa nini haijafanya vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mdondoko wa wanafunzi, wanafunzi ambao hawajamaliza shule. Ukichukua takwimu za 2023 – 2024, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wanaofika zaidi ya 500,000 hawajamaliza shule. Serikali inatakiwa ije ituambie ni nini sababu ya mdondoko wa wanafunzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linatuweka kwenye wakati mgumu. Nataka kuiomba Serikali ihakikishe inatuambia mdondoko wa wanafunzi unasababishwa na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia halmashauri zetu zitengeneze bajeti ambayo itahakikisha miundombinu ya shule na kujenga madarasa, itusaidie, ili kupata fedha hizi. Leo tumekosa fedha zaidi ya shilingi bilioni 124 kutoka kwa wafadhili, zingetusaidia ku-*cover* hili eneo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umewasha kipaza sauti, lakini nilikuwa nataka nimalizie. Bado nina dakika zangu kama mbili, tatu hivi za Mheshimiwa Rashid Shangazi, najua naye atachangia...

**MWENYEKITI:** Malizia sekunde zako.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja la mwisho ambalo ningependa niishauri Serikali ni kuhusiana na tulitembelea *DAT*. Hiki Chuo Kikuu kinatarajia mwakani 2026kurusha *satellite*. Moja ya eneo ambalo tulitaka kulijua sisi Wajumbe wa Kamati ni kwamba, tunarusha *satellite* ku-*collect data* gani? Wakasema wao wameshawasiliana na watu wa *TAWA* na nini? Maana yake ni kwamba wanataka ku-*collect* taarifa za wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi changamoto yetu kubwa hapa ni eneo la kilimo na eneo la mazingira. Tunataka warushe *satellite* watupatie taarifa ya maeneo ambayo tutafanya kilimo chetu kiwe bora, na sisi tukaangalia eneo la mazingira. Tusirushe *satellite* kwenda kwenye eneo dogo linalohusiana na wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, wajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa hotuba nzuri ya Waziri wa Elimu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Taasisi ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ukweli, safari hii kazi nzuri sana imefanyika, ninawapongeza kwa usimamizi wa kazi zote zilizofanywa katika taasisi. Uboreshaji na ujenzi umefanyika kama alivyosema Mheshimiwa Sima, na hasa maeneo ya vyuo vikuu, majengo mapya yamejengwa kwa ubora. *VETA* nazo zimejengwa ziko 64, lakini nawaomba sasa muiangalie ile *VETA* ya pale Mabwepande. Tulipoenda, niliona kama mwendelezo wake hauridhishi, labda mngeenda pale mwangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la mikopo. Safari hii wanafunzi wengi wamepata mikopo, malalamiko ya mikopo yamepungua. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuongeza fedha kwenye eneo la mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Taasisi hiyo ya *NECTA* kwenye mitihani, niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, sisi tuko kwenye ile Kamati ya Elimu. Sasa hivi mitihani inatungwa kwa kufuata umahiri, hakuna tena yale maswali ambayo wengi wanafikiria yalikuwepo, yale ya kuchagua *(multiple choice)*. Maswali yale yameondolewa, sasa hivi hata hesabu zinakwenda kwa kukokotoa. Kwa hiyo, hilo niwatoe wasiwasi ni kazi nzuri imefanyika kwenye *NECTA*. Sasa hivi mitihani inatungwa kwa kufuata umahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limefanyika, kwenye hii amali tunayokwenda sasa hivi, *assessment* (wanafunzi kutahiniwa) watakuwa wanafanya kama zamani, tulikuwa tunaita *continuous assessment*. Kwa hiyo, nafasi kubwa itachukuliwa kwa

kazi anazozifanya mwanafunzi akiwa pale shuleni. Tofauti na zamani, mtihani wa kuandika unachukua 60%. Sasa hivi 60% ni kazi za kila siku, *continuous assessment*. Kwa hiyo, hiyo ndiyo itafanyika katika amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa usambazaji wa vitabu. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Grace, kwamba, vitabu vimesambazwa kote. Kama alivyosema Mheshimiwa Sima, sasa hivi *ratio* ni kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu. Pia, *TET* iko katika mpango wa kuhakikisha kwamba, vitabu vitakwenda moja kwa moja katika shule, siyo tena kupitia kwenye halmashauri. Kwa hiyo, hizi taasisi sasa hivi zimejipanga vizuri na tumeiagiza *TCU* pia ichunguze na kuangalia wakati wote yanayotendeka katika vyuo vikuu yanafuata Taratibu au Miongozo ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye hii Sera mpya ya Elimu. Tunapoanzisha sera mpya au jambo lolote likiwa jipya ni lazima kunakuwa na changamoto. Ndiyo maana katika hii sera mpya, na hasa upande wa amali, tumeanza na shule chache, ili tuone tunakwenda namna gani? Kwa hiyo, shule chache zimeanza na kama nilivyosema, wakati mwingine haya mabadiliko huwa yanaleta changamoto ya uelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi kwa Wizara ya Elimu, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize. Jambo la msingi ni hii elimu ya amali haijaeleweka vizuri kwa jamii, na hasa kwa wazazi. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu jambo la kufanya ni kuwaelimisha, amali italeta faida gani kwa vijana wakishamaliza *form four*? Serikali itumie vyombo vya Habari; *television*, kuelezea manufaa ya amali, mtoto akimaliza *form four* ataweza kujiajiri, ataweza kuajiri na kuajiriwa, ndiyo hiyo isemwe. Kwa hiyo, tukisema hivyo, wazazi na jamii itaelewa kwamba, hii amali inaanza, lakini pia ili kufanya tathmini, ni lazima tujipe muda. Wazazi wanauliza, hii ina faida gani? Au imefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo kwanza tumeanza. Kwa hiyo, ni lazima waeleweshwe kwamba, baada ya miaka miwili au mitatu

ndiyo tunaweza kugundua kwamba, amali imetuletea faida gani? Kwa hiyo, ni vizuri mkashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, mjue kwamba, hii Sera ya Amali tukiifanya vizuri, hawa wanafunzi wakimaliza Kidato cha Nne, wataweza kupewa mikopo kwa sababu, tayari watakuwa na ujuzi na ni wafanyakazi. Kwa hiyo, tujipange kabisa, hawa watoto waweze kupata mikopo wakimaliza ile *form four,* kwa sababu, tayari hawa ni wajuzi na wanaweza kujitegemea. Pia tukiendelea na amali, uboreshaji utaendelea kwa sababu, wakati wote tunapotengeneza *curriculum* tunaifanyia uboreshaji au *evaluation* wakati inaendelea kutendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliseme leo kwa Mheshimiwa Waziri, ni kwamba baada ya miaka 30 watoto wetu watatucheka. Watatumia maneno ya ajabu sana kwamba, hivi Mheshimiwa Prof. Mkenda ndio alikuwa Waziri wa Elimu? Mheshimiwa Jenista ndio alikuwa Waziri wa Afya? Halafu wanahakikisha kwamba, vyuo hivi au vyuo vyetu vinavyoendesha elimu ya afya havina *teaching hospitals!* Watatushangaa na watatuita majina ya ajabu, watasema hii mijitu ilikaa inafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana, haya mambo mawili yafuatiliwe yafike mwisho. Turudishe *Teaching Hospitals* kwenye vyuo vinavyohusika; *MUHAS* pamoja na *UDOM*. Kama hamwezi kurudisha kabisa, angalau 80% imilikiwe na chuo chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwambia Mheshimiwa Waziri ile *proposal* iliandikwa na Mheshimiwa Prof. Pallangyo, ambaye ndiye mwenye *MUHAS* wakati ule, sasa wao wamekaa hapo mpaka wananyang'anywa, wamekaa, kweli! Sasa hili walishugulikie kuhakikisha kwamba, hivi vyuo vinapewa *Teaching Hospitals* zake. Narudia hii ni mara ya tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe taarifa, Madaktari wote wazuri wa Tanzania wamesoma kwenye vyuo vyenye *Teaching Hospitals;*

Norway, Sweden, Harvard, wamesoma huko. Mheshimiwa Prof. Mkenda analifahamu hilo.

**MHE. BALOZI BASHIRU A. KAKURWA:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, inatokea wapi? Mheshimiwa Balozi Bashiru.

**TAARIFA**

**MHE. BALOZI BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mchangiaji, na nilishawahi kumpa taarifa kwenye jambo hili hili. Suala hili liko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, suala hili kutotekelezwa ni kutotekelezwa kwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili. Kwa kweli, wakati mwingine inasikitisha, yaani inashangaza, huo ni Mwongozo wa Kimataifa, lakini pia, kwenye Ilani ipo. Tunaona tabu gani sisi kutoa hizi *Teaching Hospitals* kuwaachia wale na walishazianzisha?

Mheshimiwa mwenyekiti, hebu ona sasa hivi Benjamin wanafanya vizuri kwa sababu, tayari kuna ushirikiano mzuri na *UDOM*. Tufanye hicho kitu kiishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka alimalize safari hii, nimezungumza kuhusu mafao ya Wakuu wa Vyuo na leo ninalizungumza kwa mara ya mwisho kwenye Bunge hili Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi. Atakapokuja hapo, naomba aniambie, kwa maana walisema liko Mezani, liko kwenye Meza, naomba aniambie limefikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulisema, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Gwajima na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hatua waliyoichukua mara moja waliposikia wanafunzi wa vyuo vikuu wamedhalilishwa na wale sijui niwaite nani wale? Wamechukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Waziri na Taasisi zote, wale wanaojifanya wao ni mashuhuri sana, wanajifanya wao sijui ni mabalozi wa sehemu mbalimbali wa taasisi, mhakikishe kwamba, wanafukuzwa mara moja kwenye huo ubalozi, akiwemo huyo Mwijaku, watolewe huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mtu mashuhuri ufanye vitu vya maana, lakini unakuwa mashuhuri, unajiita mashuhuri, unafanya vitu vya ajabu! Waondolewe kwenye ubalozi, vijana wote au watu wote waofanya vitu vya ovyo katika jamii, waondolewe huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nimalizie, naomba sana shule zote zenye majina ya viongozi hebu tuzifuatilie.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Dakika moja nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufuatilie zile shule zenye majina ya viongozi, unakuta shule ina jina la Dkt. Thea Ntara sijui, lakini mimi sina shule; au jina la mtu yeyote mashuhuri au kiongozi wa Taifa, lakini tuangalie *discipline* ya hizo shule na elimu zao. Yaani ni namna gani wanafanya? Siyo unakuwa na jina kwenye shule, lakini ina-*perform* vibaya na nidhamu mbaya, ni aibu kwa Serikali. Kwa hiyo, nilitaka niliseme hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa leo inatosha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage. Mheshimiwa

Ng'wasi Damas Kamani na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hii Wizara muhimu katika mustakabali wa nchi hii. Nina mambo manne ya kuongea kabla sijachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya malengo makuu matano ya Dira ya Taifa 2025 ni kuwa na jamii iliyoelimika na yenye uchu wa kujifunza. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipotembelea Kagera alitupatia *blank cheque,* hundi ambayo haikujazwa tarakimu, akatuambia Wanakagera niwapatie nini mfurahi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipowauliza wananchi katika mambo matatu makubwa, ambayo Wanakagera waliyapa uzito, mojawapo ilikuwa ni ujenzi wa chuo kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kama alivyosema *Father* Kamugisha, "anayeshukuru anakumbuka." Tunakumbuka Kagera tulivyohangaika kupata chuo, lakini anayeshukuru anathamini. Tunathamini zawadi aliyotupatia Mheshimiwa Rais, tunathamini kazi mliyoifanya nyie wasaidizi wa Mheshimiwa Rais mkiongozwa na Profesa. Kipekee anayeshukuru anaomba tena. Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu wa zamani, unajua Wanakagera chuo kwao ni pamoja na ukubwa. Ukijenge kiwe kikubwa zaidi, uongeze majengo na *faculties* nyingi kusudi Wanakagera wapate chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la tatu, kwenye Hotuba ya Waziri amezungumzia Chuo cha *VETA* cha Ndolage, namshukuru ameniheshimisha. Tuliomba karakana; karakana tunayoiomba ni ya *Food and Beverages Production, Food Science* ya vitendo, na ya pili, tunaomba karakana ya upishi, mapambo na ulimbwende. Yaani dunia sasa hivi imeshakuwa dunia ya huduma. Hata mtu akifariki unakuta gharama ya mapambo inachukua fedha nyingi na

gharama ya chakula. Sasa hiyo ndiyo sekta tunayotaka kuishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne, kwenye aya ya 90 na ile ya 95 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza kuhusu kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali. Nakubaliana, lakini amesema *Tanzania Educational Authority* watawezesha upanuzi wa shule 55 za sekondari, ili ziweze kuwa Shule za Amali.

Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu, Wilaya ya Muleba, Jimbo la Muleba Kaskazini, tuna shule tatu zinazo-*qualify*. Sasa nakuomba uniwekee wepesi, shughuli ya mwaka huu unaijua, uchukue zote tatu au uchukue moja, nitakunong'oneza, uchukue zote tatu au moja iwe Shule ya Amali, iko kwenye Ibara ya 90 na 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Mpango na Bajeti ya Wizara hii, naomba nitamke kwamba, naunga mkono hoja ya Waziri. Sasa ninaanza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie dhana ya Shule ya Ufundi na Amali, na *Doctor* aliyenitangulia amelizungumzia. Dhana ya Shule ya Ufundi na Amali, niwaelezee nikiwapeleka kwenye ufundi katika Shule za Kilimo. Ufundi siyo kuchomea, ufundi siyo useremala, ufundi ni pamoja na kujenga ujuzi na uthubutu. Mmezungumzia mambo ya Ifunda na *Dar Tech* kwamba, mnataka shule za namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali katika Shule za Amali tufikirie kuanzisha Shule za Kilimo; kilimo kwa mapana yake. Kwa mfano, ile iliyokuwa Kilosa, iliyokuwa Ruvu, iliyokuwa Kibiti na kidogo ilikuwa *Nyakato Secondary*. Tunataka mwanafunzi apelekwe pale, asisomeshwe masomo mengi, Kiingereza iwe ni lazima au Lugha na Hesabu. Yaani hesabu haiepukiki, mwenye macho haambiwi tazama. Hata Baba Mtakatifu aliyeteuliwa juzi, ana *Degree* ya Hesabu; Makamu Mwenyekiti Baba Askofu Mwijage, Msaidizi wake *Vicar General* ana *Degree* ya Hesabu na *Civil Instructor Engineering*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uwafundishe hesabu hawa vijana halafu uwafundishe kilimo kwa ujumla, yaani kuanzia *crops, aquaculture, floriculture, pisciculture, mechanical atomization,* kusudi mtoto anaporudi akiwa na ujasiri na uthubutu anaweza akatumika katika hiyo *field*. Unapomwambia kwamba, ni *animal husbandry,* unapomwambia *artificial insemination,* unapomwambia *resembling,* unapomwambia *embryo planting,* mtoto wa darasa la 12 na 13 aweze kufanya hizo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie, nguvu ya kiushindani na kilinganishi ya hili Taifa iko kwenye Sekta ya Kilimo na hatutaikimbia. Hamwikimbii kwa miaka 40 ijayo. Dkt. Adesina alisema, *billionaire* anayekuja kesho yuko kwenye kilimo. Sasa sisi tunatoka kwenye kilimo tukakwenda wapi kwingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Akili Mnemba unaweza ukaitumia kwenye kuua wadudu shambani. Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba, nitakuja kukushauri, tunataka hicho kilimo, nami nina faida katika Wilaya ya Muleba. Mkoa wa Kagera tuna eneo la kutosha, nusu ya *land* yote ya *NARCO, ranch* zote, zaidi ya nusu ziko Kagera, Ziwa Viktoria *30%* iko Kagera, leta hiyo, nami nitakuwa mshauri, tuipeleke Kagera tuwaoneshe kwamba, hata kwenye kilimo, hata kwenye mifugo, hata kwenye uvuvi kuna ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kidogo kuhusu Bajeti ya Wizara. Mwanzoni nilipowaeleza kwamba, moja ya malengo ya dira ilikuwa ni kujenga jamii iliyoelimika na yenye uchu wa kujifunza. Ina maana ni uwekezaji katika Sekta ya *Human Capital*. Nimemsikia Mwenyekiti wa Kamati anazungumzia kutopatikana kwa pesa na mtiririko usioweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiambia Serikali yangu Tukufu kwamba ni lazima tuwekeze fedha nyingi katika elimu. Katika vita ya biashara ya China na Marekani, China na Marekani Mchina amempiku Mmarekani kwa sababu ana jeshi kubwa lililoelimishwa, kuanzia fundi mchundo kuja fundi mwenyewe kwenda hata wenye *Degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuwekeze kikubwa, iwe kipaumbele. Huu ni mradi wa kimkakati. Unapozungumza elimu *(education),* unamaanisha mradi wa kimkakati utangulie, mengine yafuate. Huwezi kujenga uchumi imara, huwezi kujenga maendeleo ukiwa na watu ambao hawana elimu. Huwezi kuwa na amani, huwezi kuwa na mshikamano na upendo na watu wasiokuwa na elimu. Mtu ambaye hana elimu, uwezo wake wa kutafuta na kujiongezea kipato ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo nikinukuu taarifa za Kamati. Mwanangu, Mheshimiwa Mwenyekiti aliyoyasema ni kweli. Ni lazima fedha zipatikane kikiwa kipaumbele. Fikiria wewe mtunga sera, wewe mfanya maamuzi, kama mwanao asingekuwa na uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie bodi ya elimu. Imezungumzwa kwamba tuna mahitaji ya walimu 268,000 ili tujiulize. Tujifungie tujiulize, kama tukiajiri walimu 268,000 nini kitatokea? Tuna walimu 268,000, na siyo ajabu tunao mtaani. Tukiamua kama Taifa kwamba tunakwenda kuwaajiri, tutakosa nini? Tukae kwenye vipaumbele vyetu, vingine tuache tuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria unapeleka mtoto kwenye shule ya kulipia, mtoto anarudi baada ya miaka minne anakwambia sikusoma hesabu, sikusoma *biology,* nilikuwa ninacheza, nilikuwa ninakula; anarudi amefura mashavu, haya amenenepa, lakini miaka yote hakupata walimu waliotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye maamuzi magumu kama Taifa. *Call it a project,* walimu 268 wote waende waajiriwe, tuangalie. Pesa zina tatizo, tunazitoa wapi? Kuna nchi moja sitaki kuisema, iliwahi kukopa *World Bank* kulipa mishahara ya walimu; lakini leo wanatesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwenye mkutano mmoja Vienna. Nilipohutubia, baada ya kuhutubia umati wote ukatikisika. Nikaona watoto wawili wanakuja kando yangu, walinisalimia

kikwetu. Yaani wale watoto kwa kuniangalia, wakanisalimia kikwetu, kumbe nchi yao imewaandaa. Ma-*ushers* waliokwenda kwenye mikutano ya *European Union, African Union* ma-*ushers* wote wanatoka nchi ile, na anakuangalia sura. Yaani Kiingereza changu waliponiangalia wakasema hiki kinatoka mahali fulani. Akanifuata mtoto akazungumza kikwetu. Tunataka Watanzania wawe namna hiyo. Tutengeneze Watanzania wa namna hiyo waivamie dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mimi ninapoangalia, mnatengeneza madereva, yaani masharti ya dereva eti atapewa na chakula bure. Hiyo ni kazi kweli hiyo! Mtu eti tunatafuta madereva, utapewa kazi bure na Jumapili, na siku ya sikukuu au anafanya kazi siku zote. Ni lazima tuwekeze hapo, lakini suala la msingi kwa Serikali yangu, tukiajiri walimu 268,000 tutazimia? Kipi kitakwama? *Is not a priority!* Hili ni jeshi, ni jeshi la kuikomboa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora nizungumze hilo, nami hilo ndilo la kwenye bodi ya elimu. Bodi ya elimu tumeizungumza hapa, kama siyo Bunge la Kumi na la Kumi na Moja, ni *copy from Zimbabwe*. Zimbabwe wana bodi ya elimu, ukimaliza ualimu unapewa *certificate* na unafanya mtihani. Ngoja niwaambie; mbona kuna bodi ya uhasibu hatujalalamika! Mbona kuna bodi ya mainjinia hatujalalamika! Hupewi kazi bila kuwa na *certificate* ya bodi. Waende kwenye bodi. Tunaangalia upande mmoja, kuna walimu wengine ukikutana nao darasani unasema yala! hawa watoto tunaowaleta tunawalisha sumu siyo elimu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda shule moja nikaingia darasani nikamkuta mwanamama mmoja mwalimu amefunga dera, nikasema watoto wana kazi hapa. Unafunga dera darasani? Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bodi ya elimu ni lazima, na tuna-*copy* Zimbabwe. Hatuvumbui jambo jipya, na bila bodi ya elimu hatufiki popote. Kwa sababu ya muda, nimeandika andiko zito, nitampa rafiki yangu wa siku nyingi kusudi liweze kuwaongoza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa mara ya nne. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage. Nilimtaja Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kwa kupata nafasi kuchangia katika Wizara yetu ya Elimu. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara yote kwa ujumla kwa kazi kubwa na nzuri ambayo tumeifanya ndani ya muda huu wa miaka minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu mapinduzi yaliyoshuhudiwa na sisi vijana na Watanzania kwa ujumla katika sekta hii ya elimu kwa miaka minne ni makubwa. Tunazungumzia ndani ya miaka minne ongezeko kubwa sana la bajeti ya mikopo ya elimu ya juu kwa vijana. Pia tunazungumzia ongezeko kubwa sana la fedha ambalo limekwenda kuongeza wigo wa elimu bure kuishia kidato cha nne mpaka kidato cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea ongezeko kubwa sana la bajeti ambalo limekwenda kuongeza wigo wa mikopo kuishia katika vyuo vikuu peke yake, mpaka kwenye baadhi ya vyuo vya kati. Tunazungumzia kipindi ambacho mabinti waliokuwa wamekatisha elimu zao kwa sababu za kupata ujauzito, wamerudi shuleni sana, sasa wanaendelea na elimu zao. Ni kipindi ambacho tunazungumzia mabadiliko ya Sera ya Elimu ambayo yametuletea mabadiliko makubwa sana ya mitaala ambayo yamekuwa yanapigiwa kelele na Waheshimiwa Wabunge katika Bunge hili, lakini na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu pamoja na ukinara alioonyesha katika sekta nyingine, lakini amekuwa kinara mkubwa sana wa mabadiliko katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utajikita katika mabadiliko au Sera mpya ya Elimu ya Mwaka 2023 na mabadiliko ya mitaala ambayo imekuja kutuongezea mtaala mpya wa elimu ya amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo imekuwa inapigiwa kelele na walio wengi ni kwamba vijana wengi cha kwanza wanakosa ajira kwa sababu elimu wanayoipata katika mfumo wetu wa elimu haikidhi au haimpi kijana weledi wa kutosha kufanya kazi zinazotakiwa. Pia sekta binafsi zimekuwa zinazungumza kwamba vijana wanaotemwa na vyuo vyetu vikuu hawakidhi mahitaji ya soko la ajira lililopo nje. Leo hii majibu ya changamoto hizi, yapo katika mabadiliko haya ya mtaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumzia elimu hii ya amali ni vizuri sana watu wakaelewa. Baba yetu wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kitabu alichoandika mwaka 1967 *Education for Self-Reliance* au Elimu ya Kujitegemea alizungumzia elimu ambayo leo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan chini ya Mheshimiwa Waziri na Wizara yake ya Elimu ndio wameirudisha. Kwa hiyo, tukizungumzia kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anasimamia misingi ya Taifa hili tangu linapata uhuru, hiki ndicho tunachomaanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hii ya amali inakwenda kumsaidia kijana anapoingia kuanzia *form one* mpaka *form four,* pamoja na kujifunza masomo yake ya darasani, lakini anakwenda kupewa ujuzi wa vitendo unaomsaidia. Hata akiishia *form four,* kwanza anapewa cheti chake cha elimu, lakini pia anapewa cheti au *certificate* ya ujuzi aliopokea. Kwa hiyo, kijana huyu anakuwa na uwezo wa kuchagua aidha aishie *form four,* anaweza kabisa kwenda kupambana na mazingira yake na kufanya kazi, lakini pia

hata akienda chuoni haendi kuanzia kama kule ambapo anaanzia mtu mpya, anakwenda akiwa na cheti chake cha ujuzi. Aidha, *Diploma* au *form five na six* mpaka vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wanaanza kujifunza elimu ya vitendo kuanzia *form one* na elimu hii ya amali inaendana na mazingira husika. Kwetu sisi Mwanza watu wanafanya uvuvi. Maana yake ni kwamba kijana watashuariana sasa mwanafunzi na mzazi husika, kwamba apate ujuzi upi? Je, ajifunze uvuvi kuanzia *form one* mpaka *form four?* Maana huyu kijana akitoka hapo *form four,* hata akiingia ziwani kuvua hatalingana na yule ambaye hajasoma au hatalingana na yule ambaye amekwenda chuo cha *VETA* kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamaanisha tunakwenda kuzalisha vijana watakaokwenda kulikomboa Taifa hili. Tukizungumzia suala zima la mapinduzi ya viwanda, majibu yapo katika elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niipongeze sana Serikali kwa sababu majibu ya changamoto za Taifa hili, kwangu mimi ukiniuliza ninakwambia majibu yapo kwenye mtaala huu. Tutakapoanza kupata matokeo ya mtaala huu kuanzia mwaka 2027 wote tutarudi ndani ya nyumba hii tutakubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niwaambie na kuwatia moyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Mheshimiwa Rais yote anayoyafanya washauri wakuu ni Bunge hili na ni ninyi Waheshimiwa Wabunge. Ninaamini kwa mabadiliko haya ambayo mmeyafanya, hii kazi mliyoifanya ni kwa ajili ya Watanzania wote, kwa ajili ya vizazi mnavyofuata, kwa ajili ya wote. Ninaamini wanaona kazi mliyoifanya na sina mashaka mwezi wa 11 tutakutana hapa kuapa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hii ya amali pamoja na kwenda kutengeneza *competence* ya vijana wetu tunaokwenda kuwachukua na kuwaweka kwenye jamii zetu, tuangalie nchi mbalimbali ambazo leo hii zimeendelea. Mfumo huu Wizara yetu

imeuchukua kwa kuu-*pin point* maeneo mbalimbali. Tumechukua elimu ya Ujerumani, tumechukua elimu ya India, tumechukua elimu ya China, tumechukua elimu ya Canada, tumechukua elimu ya Switzerland, zote tumezileta kupata mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongelea nchi kama China ambazo zina mapinduzi makubwa sana ya viwanda wanafanikiwa kwa sababu moja, kwamba vijana wao wana ujuzi wa muda mrefu wa vitendo wa kufanya kazi. Vitu vingi tunavyo-*import* hapa ni vitu ambavyo vimetengenezwa kwenye viwanda vidogo vidogo vinavyoendeshwa na vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mataifa mengine ya wawekezaji wenye mitaji wanakwenda kuwekeza kwenye nchi hiyo wakiamini kwamba kuna teknolojia ya kutosha ya kuzalisha vitu hivyo. Kwa hiyo, siyo tu kwamba tunakwenda kuzalisha ajira nyingi kwa vijana wetu, lakini tunakwenda kuifungua nchi yetu kwa uwekezaji mkubwa sana kwa sababu vijana watakuwa na uwezo wa kuzalisha kinachotakiwa, na vilevile tutakuwa na uwezo wa kupambana na mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyepo Njombe atafundishwa namna bora zaidi ya kulima miti. Aliyepo Geita atafundishwa namna bora zaidi ya kuwa mchimbaji madini, aliye na weledi mkubwa na wa muda mrefu. Kila kijana kwenye mazingira yake hata akiishia katika elimu yake, Taifa hili litakuwa limepunguza mzigo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, cha kwanza, pamoja na mtaala huu mzuri sasa tuliouweka, amekuwa akishauri Baba yangu Mheshimiwa Kishimba kwa muda mrefu kwamba mwanafunzi anayefundishwa na Profesa ni tofauti anayejifunza mtaani. Sasa kwenye hili tumelipatia majibu kwa sababu hawa vijana wanaenda kuanza kujifunza kwa vitendo kuanzia akiingia *form one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa, Serikali iangalie uwezekano, kuna watu ambao wameshakuwa wabobezi wa muda mrefu kwenye kazi hizi. Nitoe mfano mdogo, kwenye elimu yetu sisi

ya *Law School* tunasoma darasani, lakini tukitoka kuna wale mawakili au wanasheria nguli waliokaa muda mrefu kwenye *practice,* wanakuja kutufundisha madarasani. Kwa utambuzi wangu, nchi hii ina wazalendo wengi sana. Tuangalie, kwenye hizi amali kama kuna uwezekano wa kupata watu walio-*practise* muda mrefu wakafundishe wanafunzi wetu, kwa sababu kuna tofauti ya kufundishwa elimu ya darasani na ile ya ujuzi kutoka kwa yule aliyefanya kwa muda mrefu, basi tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, pamoja na kwamba tumeweka mfumo huu wa amali, sasa ni wakati vyuo vyetu na vyuo vikuu vianze kujiwekea tathmini ya mitaala yao ili nao watengeneze mitaala yenye malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunavyozungumza hapa, ni ukweli usiopingika kwamba nchi hii haiwezi kuajiri vijana wote. Mataifa yaliyoendelea au yanayofikiria kwa muda mrefu yanatengeneza mazingira ya kuweza kuchukua watu wake na kuwapeleka kwa ajili kuajiriwa katika mazingira au nchi za watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo hii tunahitaji vyuo vyetu, kama ambavyo tumeanzia ngazi za chini kutengeneza mitaala ambayo unakwenda kumsaidia kijana, basi vyuo vyetu na vyenyewe viangalie upya programu zake, ziwe zina malengo *international,* ya kidunia, ili kijana anayetoka kusoma katika chuo chetu aweze kwenda kufanya kazi sehemu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza hapa baba yangu Mheshimiwa Mwijage wakati anachangia kwamba, ni muhimu kwa vijana wetu, na kuna fahari ya kwenda nje ukakuta kwamba kuna Watanzania wengi wanafanya kazi kule kwa kuwa wana uelewa wa kutosha kutoka katika mifumo yetu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri. Leo hii suala hili la bajeti limepigiwa kelele siyo na Waheshimiwa Wabunge peke yake, lakini na Watanzania kwa ujumla. Tulipiga sana kelele juu ya

suala zima la mitaala, na sasa naipongeza Serikali kwa sababu imeongeza sana bajeti, kutoka shilingi trilioni 1.9 mwaka uliopita hadi 2.4 kwa mwaka huu. Ongezeko hili kubwa limekwenda kupelekwa moja kwa moja kwa sababu ya huu mtaala mpya. Yaani kwenda ku-*fund* huu mtaala mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba hii ni ajenda yetu ya Kitaifa. Tumepiga kelele kwa muda mrefu juu ya suala hili la elimu. Sasa limefika, tupo tayari kufunga mikanda kwenye vitu vingine ili tuweke fedha kwenye mtaala huu ili shule nyingi zaidi za amali ziweze kuongezwa na kwa wakati mfupi vijana wengi zaidi waendelee kupata elimu hii na kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya changamoto ya bajeti, sasa hivi tumeanzisha shule chache sana za amali, lakini mimi nafikiri tuendelee kuangalia namna ya kuongeza bajeti ili shule hizi ziwe nyingi na vijana wengi zaidi sasa waweze kupata elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani. Nilimtaja Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, na Mheshimiwa Athuman Almas Maige wajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uwekezaji mkubwa ambao ameufanya katika sekta ya elimu. Tunampongeza sana kwa maono yake na malengo mazuri ambayo ameyaona katika kulisukuma Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kupitia Mheshimiwa Waziri wake wa Elimu na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais na kuwakwamua wananchi katika sekta hii ya elimu. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote katika haya mabadiliko ya mtaala mpya ambao umekuja mbele yetu. Mtaala huu ni mkombozi mkubwa. Niungane na wenzangu wote waliotangulia kusema kwamba ujuzi ndiyo njia pekee ambayo itatutoa katika hali hii tuliyonayo sasa hivi, ya kuhangaika na bahasha kwa vijana wetu. Wanamaliza ofisi miaka inapinduka, inakwenda kwa sababu elimu ambayo waliipata, wengi wao haikuwa na ujuzi ambao ungewawezesha kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala huu wa amali ambao tunaenda kuutekeleza sasa, nina uhakika kabisa kwamba wanafunzi watakapokuwa wamemaliza watakwenda kujiajiri wao wenyewe na Serikali itapunguza ule mzigo mkubwa wa kuhangaika kuwatafutia nafasi za kazi wahitimu ambao watatoka kwenye mfumo huu wa amali. Kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kile ambacho mlikifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanamtwara ni wanufaika wakubwa wa mfumo huu mpya wa amali. Tunashukuru sana Serikali na tumeendelea kuishukuru kwa sababu wakati wa utekelezaji wa *MEM, SEDP* pamoja na *PEDP* 2002 sisi Wanamtwara tuna chuo chetu cha ualimu kawaida ambacho kilikuwa miongoni mwa vyuo vitatu ambavyo Serikali ili-*repoint* kwa ajili ya kuendeleza walimu wa sayansi ili warudi kule chini wakafundishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hatukupata bahati hiyo tangu hapo, vikaenda chuo cha ualimu cha Dar es Salaam ambayo sasa ni *DUCE* na kule *MUCE* Iringa, Mkwawa lakini Mtwara kilibakia kwenye maandishi. Nashukuru juhudi za Serikali sasa hivi kitakuwa ni

chuo ambacho na chenyewe kimechukuliwa, pamoja na kile Chuo cha Mtwara cha Ufundi ambacho sisi tunaita Mwasandube.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunashukuru sana kwamba vyuo hivi sasa vitatumika kwa ajili ya mafunzo ya amali. Ni kama *Campus* ya Chuo Kikuu cha Mbeya cha kufundishia watu kwa ajili ya mafunzo ya amali. Wanamtwara tunasema ahsante sana Serikali, kwa sababu siyo kwamba ujuzi tu ule ambao vijana wetu wataupata, kuwepo kwa vyuo hivi, Mtwara kawaida na Mtwara ufundi kama *campus* ya Chuo Kikuu cha Mbeya cha Ufundi ni kwamba itabadilisha mandhali ya Mtwara. Sura ya Mtwara itakuwa nzuri sasa kwa sababu uwekezaji mkubwa utafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wanamtwara watapata fursa nyingi kupitia uwepo wa vyuo hivi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana, sana. Tunaishukuru sana Serikali kwamba Wanamtwara na sisi sasa tumeonwa. Uwepo wa vyuo vikuu vingi katika maeneo yale utachagiza wananchi wa kule nao kupata mwamko kwa sababu wanaona vyuo vikuu vipo pale. Kwa hiyo, itakuwa ni hamasa kubwa kwa wazazi kupeleka wanafunzi wao katika shule mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali, tuna furaha sana kwa hiki ambacho wamekifanya. Nashauri sasa, kwa sababu vyuo hivi ni vya muda mrefu, vimechoka, nashukuru kwamba bajeti kwa ajili ya maboresho ya vile vyuo imetengwa. Tumesoma kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, lakini maboresho haya naomba sana Serikali isiishie tu kuboresha madarasa, iende pia hadi kwenye nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za watumishi ambazo zilikuwa zinatumika na wakufunzi wetu pale Mtwara *TTC* pamoja na Mtwara ufundi zimechoka. Naiomba Serikali kupitia bajeti yake ione namna ambavyo itaboresha mazingira mazuri kwa wale ambao watakuwa wanafanya kazi chuoni ili nao wapate sehemu nzuri ya kuishi ili wakafanye kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na ninaishauri pia Serikali kwamba uwepo wa vyuo hivi ni kitu kigeni kule, basi redio za kijamii za kule zitumike kuelimisha wananchi kuhusiana na kitakachoendelea katika maeneo yao ili nao wapate uelewa wa mambo ambayo Serikali yao inayafanya katika maeneo yao. Pia, kwa kuwa ni vyuo vipya, na mafunzo yanayoenda kutolewa pia ni mapya, naomba basi karakana zote zinazotakiwa kwa ajili ya utoaji wa mafunzo haya zikajengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia hapa Mheshimiwa Mwijage anachangia kuhusu suala la elimu kupitia kilimo. Sisi tulikuwa na shule Ndanda, tulikuwa tunalima sana, kwa hiyo, hayo mazingira yawekwe kama ni watu wa kilimo, watafutiwe eneo ambalo wataenda kujifunza kulima, watakaoenda kwenye upishi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, miundombinu yote ambayo itawafanya wanafunzi kujifunza kwa ufasaha ikajengwe na kusimikwa katika maeneo haya ili wanafunzi watakaomaliza pale wawe wameiva, sio wanafunzi ambao walikuwa hawajaiva sawasawa. Waive ili waweze kwenda ku-*implement* vizuri kile ambacho watakuwa wamekisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuongelea ni suala la uhaba wa walimu. Ili ufundishaji na ujifunzaji ufanyike vizuri, ni lazima walimu wawepo katika madarasa yetu. Kupitia taarifa ya TAMISEMI, 2024 imebainisha namna upungufu wa walimu ulivyo katika maeneo yetu Kitaifa, lakini pia hata ukienda kiwilaya. Kwa mfano, kwenye Shule za Awali kulingana na taarifa ya TAMISEMI 2024, Shule ya Awali walikuwa na mahitaji ya walimu 71,652, lakini waliyopo ni 16,559, upungufu ni 85.9%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule za Msingi mahitaji yalikuwa walimu 298,687 waliopo ni 124,826 upungufu ni 41.8%. Sekondari kadhalika. Matarajio ni kuwa na walimu 177,136 lakini waliopo ni 82,517 upungufu ni 46.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inasababisha wanafunzi kutopata vizuri masomo ambayo wameyaendea shuleni. Pia hali hii inaathiri utoaji wa elimu hata katika Jimbo la Newala Vijijini. Kwa mfano, ukienda Shule za Msingi za Jimbo la Newala Vijijini, Halmashauri ya *Newala DC*, mahitaji yalikuwa ni walimu 787, lakini waliopo ni 382 tu, sawa na 49%. Ukienda Sekondari, hali siyo nzuri kabisa. Tulihitaji walimu 482, lakini waliopo ni 185, asilimia ya upungufu ni 57. Tena ukienda kwenye masomo ya sayansi, tulihitaji walimu 203 wa sekondari; waliopo ni 81, upungufu ni 122.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii siyo tu kwamba inasababisha wakati mwingine hata ule mdondoko ambao umeoneshwa kwenye taarifa. Kuna mdondoko mkubwa. Wakati mwingine mdondoko unachagizwa na upungufu wa walimu, kwa sababu wanafunzi wanaenda shule wanatarajia wakutane na walimu, wapate elimu, lakini wanafika shuleni wanazunguka siku ya kwanza hawamwoni Mwalimu; siku ya pili, kesho, wanakata tamaa, wanakaa nyumbani, mdondoko unaanzia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali, naungana na wote ambao wamesema tuwekeze katika kuajiri walimu, tukiwekeza katika kuajiri walimu wengi hata ile *human capital* tutaipata kwa sababu tutakuwa na wajuzi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa sababu ya upungufu wa walimu, wazazi wanachangia kupata walimu wa kufundisha watoto wao. Kwa hiyo, tunawapa mzigo. Sawa, elimu inatakiwa kuchangiwa na kila mmoja wetu, lakini mzigo unazidi. Mzazi mwingine ana watoto wawili au watatu, anatakiwa achangie walimu kwa ajili ya ufundishaji wa Watoto, inakuwa ni kero kidogo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili Serikali iliangalie, nasi wananchi wa *Newala DC* tuangalieni tupate Walimu wa kutosha ili wanafunzi wetu watoke pale wakiwa wameiva na kwenda kulitumikia hili Taifa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni ombi. Kule nyuma kulikuwa na kitu kinaitwa *Teaching Allowance* kwa walimu. Walimu walikuwa wanafanya vizuri sana. Nafahamu ni suala la kibajeti, lakini sasa hivi *Teaching Allowance* imeondolewa kwa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule pamoja na Waratibu Elimu Kata wanapata posho ya Madaraka, lakini pia tuwaangalie hawa walimu ambao wanaingia madarasani, mazingira yao siyo rafiki. Basi turudishe ile *Teaching Allowance* ili walimu wetu wapate moyo, iwe kama motisha kwao, wakapate kutufundishia watoto wetu vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele yako imelia zamani.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii, naunga mkono hoja. Pia naipongeza Wizara kwamba sasa hivi mafunzo kwa vitendo kwa walimu tarajali yamerudi miezi mitatu, hongereni Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Aysharose Mattembe ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie Wizara hii ya Elimu, Wizara muhimu sana ya Sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na pongezi. Nakupongeza sana Mheshimiwa Profesa Mkenda na Wizara yake yote kwa kufanya kazi kubwa sana ya kuleta mageuzi ya Sera hii ya Elimu ili kuingiza Mtaala huu kwa Amali. Kabla ya hapo nieleze, mimi

ni mfaidika wa elimu ya amali. Nimesoma *Moshi Technical* na baadaye *Technical College*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nieleze kwamba kazi zote za kiufundi zinazofanyika hapa nchini zina mazao ya amali, kwamba aidha, walisoma *Moshi Technical, Ifunda Technical, Mtwara Technical* au *Tanga Technical.* Hawa ndio wanaoleta mageuzi katika sekta ya ujenzi, lakini ndiyo wanaoleta mageuzi katika sekta ya amali ambao wanafanya kazi za kujitegemea. Liko tatizo dogo ambalo nafikiri ni muhimu sana.

Mheshimiwa Profesa unisikilize. Tatizo kubwa neno, amali halieleweki, tutaanza kupata fundi wa amali. Halieleweki kabisa duniani kote, na hatutoki nje ya gurudumu hili, lazima kuwe na fundi mchundo, lazima kuwe na fundi sanifu na lazima kuwe na mhandisi. Elimu hii ya amali itoe hao watu watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililotokea ni zuri sana. Sasa ndani ya bahasha hii ya amali kuna makundi hayo, lakini vyuo vyote viko tofauti. Wanaofundisha msingi wa kwanza kabisa wa ufundi yaani fundi mchundo ni *VETA*, lakini kulikuwa na mvurugano watu hawaelewi *VETA* inatoa mafundi gani? Pia wanaotoa wanafunzi au wataalamu wa *Full Technician Certificate (FTC)*, hawa wanaitwa fundi sanifu, ni kutoka elimu ya sekondari ya amali halafu chuo cha ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeeleza itajenga vyuo vingi vya *VETA*, haiongelei vyuo vingi vya ufundi, tulikuwa na chuo kimoja tu cha ufundi *(Technical College)* pale Dar es Salaam ambacho sasa ni Chuo cha Elimu ya Juu, hakitoi lile kusudio lililokusudiwa la watu wa chini. Tatizo hili likiendelea tutawapoteza wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, waajiri wanapata taabu maana tutasema wametoka wanafunzi chuo cha ufundi, kumbe *VETA;* wanafunzi wametoka chuo cha ufundi, kumbe *technical college*. Kumbe anataka kuajiri fundi sanifu, yaani *full technician certificate*

*person*, anataka kuajiri mtu wa *VETA*, mambo haya ni mazuri sana kuelezwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejikita kuleta elimu ya kujitegemea, nami nina imani tulishakaa mara nyingi sana kuelezana suala hili, lakini nikisoma kwenye hizi taarifa zako, na leo nilikuwa napitia hii taarifa, wananchi wangu kijijini hawaelewi fundi amali ni nani? Waajiri wanataka kuajiri *technician* (fundi sanifu), waajiri kutoka wapi? Fundi amali! Wanataka kuajiri mtu wa kada ya chini, fundi bomba wa kuzibua bomba na kadhalika, fundi mchundo waajiri kutoka amali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimefurahi sana, taarifa ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri ya kujenga. Moja, kufufua chuo cha ufundi na pia kujenga vyuo vingine vya *VETA*. Ni sawa kwa sababu katika kila ujenzi mkubwa wa *construction* yoyote kutakuwa na Fundi Sanifu, Fundi Mchundo na Mhandisi, na hawa lazima watokane na elimu yetu ya amali. Kwa hiyo, amali hii itafsiriwe zaidi kuchambua watu hawa watatu. Tukifanya hivyo, tutakuwa na mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nilitaka niongelee mambo mengine machache kuhusu ufanisi wa mafundi ambao tunafikiri kwamba watafanya kazi vizuri na mafunzo mazuri. Tulipoanza na nina-*quote,* Mheshimiwa Profesa Mkenda alisema kwamba, "Hatuwezi kwenda wakati mmoja pote paa, tukaenea. Tutaanza." Ninavyoona anataka kuacha lile wazo lake zuri kwamba tuanze taratibu, anataka kuanza pamoja, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa *Moshi Technical,* nikitembelea *Ifunda Technical* tulikuwa na sekta zote za ufundi; ufundi magari, ufundi *machenical, electronic*, ufundi umeme lakini ufundi wa ujenzi kwenye shule moja, na kulikuwa na karakana zote. Hatuwezi Vyuo vya *VETA* 200 *low carder,* lakini shule nyingine zile za amali zikawa na vifaa vyote hivyo, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipange kwa Kanda. Kanda hii tuna shule kumi za amali, zina kila kitu ndani yake; Kanda hii ina shule kumi za amali, ukiingia ndani ya shule ile kuna karakana ya *machenical*, kuna karakana ya umeme, kuna karakana ya *civil,* kuna karakana ya *electronics*. Zimekamilika. La sivyo, tutaenda kutoa watu wa nadharia *(theories),* hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimeenda *Moshi Technical* zile karakana hazipo na ndiyo ilikuwa shule kubwa kabisa ya ufundi. Hakuna *Lance Machines* upande wa *mechanical,* upande wa umeme vitu havipo, lakini inaitwa shule ya ufundi. Hii tutapiga pancha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa alikuwa na wazo zuri kwamba bora tuanze, lakini nashauri sana, aoneshe kwa vitendo anaanza, siyo anaenea kila mahali, haiwezekani. Nami nakuamini na hata Mheshimiwa Rais hakutegemea atafanya makubwa namna hii. Bajeti yake inajenga shule 200, itapata wapi vifaa vya kujaza kwenye hizo shule? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, darasa moja la Shule ya Ufundi; *Moshi Technical* au Ifunda au Tanga, inagharimu bilioni za pesa, sasa 200 zitapatikana wapi? Kwa hiyo, nashauri arudi kwenye wazo lake la kwanza alipotushawishi Wabunge tumuunge mkono kwamba anaomba tuanze, aanze na shule chache za amali au shule za ufundi na neno la ufundi litumike sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, asiache kanuni kwamba ufundi lazima uanze kwa hatua, lakini watu pia wafafanuliwe mtoto wa *VETA* anapata nini? Mtoto wa *form one* mpaka *Form Four Secondary School* anapata nini? Anapokwenda *Technical College* anapata nini? Tukiweka vizuri haya, pongezi sana. Hongera sana Profesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naunga mkono sana hotuba yake, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Athuman Almas Maige. Nilimtaja Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Aysharose wajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia kwa Rais wake wa Awamu ya Sita Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kufanya maboresho makubwa sana katika sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba toka tumeingia humu ndani tatizo letu kubwa lilikuwa ni namna gani mitaala yetu inabadilishwa? Nilizungumza kwamba kule Mwanza kulikuwa na kongamano la vijana. Siku hiyo Waziri, Mheshimiwa Prof. Mkenda pamoja na Mheshimiwa Rais walikuwepo. Katika Kongamano la Vijana niliwaambia vijana someni mkitambua mnasoma ili mwelimike na mkielimika mjiajiri wenyewe. Hii ndiyo *message* niliyoipeleka mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka Waziri, Mheshimiwa Prof. Mkenda akaniambia umesema mambo makubwa sana yanatakiwa kufanyiwa kazi. Tuna vijana zaidi ya milioni 23 sasa hivi, na katika hao vijana milioni 23 na wao wanahitaji waje kuwa na maisha kama sisi baba zao, kama sisi wazazi wao, lakini ni lazima wafanye kazi ili waishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo moja ambalo linasumbua katika nchi yetu ilikuwa ni namna gani hawa wanafunzi wanaotoka katika vyuo vyetu wawe na uwezo wa kufanya kazi bila kutegemea kufanyishwa kazi. Kwa hiyo, yeye mwenyewe anajengeka kwamba natakiwa kuwajibika. Nifanye nini leo? Anapanga kazi zake za kufanya. Hawezi kupanga kazi zake za kufanya kama hajaandaliwa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaandaa hizi shule za elimu ya amali na biashara, lilikuwa kosa kubwa sana katika nchi yetu kuliacha hili somo la amali. Kama mtangulizi hapa alivyosema, hivi vyuo *Tanga Technical, Moshi Technical, Arusha Technical,* na *Ifunda Technical,* hizi sekondari zilikuwa zina maana kubwa sana. Wakati Baba wa Taifa anazianzisha katika nchi yetu, sasa tunaingia katika hii elimu ya amali kwa kasi kwamba tunaonesha tumechelewa na katika kuonesha tumechelewa tunatakiwa twende kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Waziri, mimi ninakuamini kabisa na katika maboresho makubwa haya unayoyafanya, tunakutana, tunazungumza na unatusikiliza, lakini inataka utusikilize katika *angle* moja hii ya kwanza. Ni kwamba hawa walimu wa hizi shule za amali na walimu wa shule za biashara, huu mtaala wa biashara ambao tunaoupeleka ni kwamba lazima upelekwe kwa shule zote, kuanzia shule za *O-level* na *Advance*, yaani uhakikishe walimu wa masomo ya biashara wapo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili hizi shule kwa ajili wa amali, je, umewaandaaje walimu wake? Ni kwamba lazima hawa walimu uwaandae, wapelekwe nje wakasome ili tuendane na hali inavyokuwa ya dunia. Hatuwezi kujifungia ndani hapa Tanzania tukaona kwamba tuna uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama sasa hivi, tuna hizi treni za mwendokasi, hawa walimu huwezi ukawafundisha hapa. Niambie una chuo gani Tanzania cha kuwafundisha? Sasa ni lazima tuwapeleke watu wakasome halafu waje hapa kufundisha tupate madereva wengi wa kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa mfano tu, leo kuna *pump* hizi za *petrol station*, sasa hivi hizi *pump* za *petrol station* niambie una chuo gani kinachotoa *course* za kuwafundisha mafundi wanaokwenda kuweka *pump* za *petrol station,* au kutengeneza hizi *pump* za *petrol station?* Hawapo. Watu wa vipimo hawana hawa

mafundi, hao ma-*technician* hawapo, kwa sababu hatuna huo mtaala hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajenga majengo marefu, tunatakiwa tupate mafundi, ma-*technician* ambao watakuwa wanazi-*run* hizi *lift*. Unaweza ukakaa kwenye *lift* masaa mawili, wanatafuta mafundi. Unaweza ukakuta Mkoa mzima wa Dodoma fundi wa *lift* yupo mmoja tu. Sasa inaonesha kwamba tuko nyuma kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tupeleke mafundi wakasome nje. Mheshimiwa Waziri, hili najua kabisa liko ndani ya uwezo wako na tunavyopeleka hawa wataalamu warudi kuja kufanya kazi na mwaandalie malipo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kupeleka hawa tu peke yao bila Kitengo cha Mdhibiti Ubora. Huwezi kuwa na elimu ya amali bila kuwa na kitengo cha mdhibiti ubora. Hauko kwenye udhibiti ubora. Hawa wataalamu wakafundishwe kwa sababu huwezi kuweka Mdhibiti Ubora wa Wilaya ambaye anaenda kukagua hizi shule. zimekuja na mtaala mpya, wakati yeye haujui ule mtaala mpya. Hili ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Waratibu wetu wa Kata. Hawa Waratibu Elimu Kata ni lazima wapate mafunzo, huwezi kuwa na kitengo cha elimu ya amali unampeleka Mratibu wa Kata kule, yeye ni mwalimu, huyo mwalimu aliyepelekwa kule amesoma *art* na kule kwenye Kata yake kuna shule mbili za amali. Anaenda kufanya nini na amesoma masomo ya *arts?* Sasa kuna kazi kubwa sana. Kwa hiyo, haya ni mawazo ambayo nimeona nimshauri Waziri wa Elimu katika Kitengo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Mdhibiti Ubora. Hakuna mahali ambapo wadhibiti ubora wanaishi kimaskini na wako kwenye kitengo nyeti kabisa. Mdhibiti Ubora ni sawasawa na *CAG* wa elimu katika nchi yetu. *CAG* katika bajeti ya nchi anapewa siyo chini ya

asilimia kumi au asilimia tano ya bajeti ya nchi ili aweze kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matokeo yake, mdhibiti ubora wetu, bajeti yako sasa hivi hapa 39% inategemea pesa kutoka nje. Haya, huyu Mdhibiti Ubora unakuja kumweka wapi? Unampa kwenye bajeti yako asilimia ngapi? Unaipeleka katika Kitengo cha Udhibiti Ubora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la udhibiti ubora ni kwamba unavyobadilisha mitaala, na hawa watu wa udhibiti ubora lazima nao waingie kwenye mafunzo, na kule kwenye udhibiti ubora mwaandalie vifaa vya kufanyia kazi. Unakuta katika wilaya, mdhibiti ubora ana gari, lakini hilo gari lina miaka 15. Mdhibiti ubora atakwenda kukagua shule ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye jimbo langu tu nina shule karibu mia moja ishirini na kitu, lakini Mdhibiti Ubora gari halina tairi. Wewe Mbunge usipomnunulia Mdhibiti Ubora, basi inamaanisha kwamba hawezi kukagua shule, lakini lazima uje na makadirio kwamba Bwana Mdhibiti Ubora wa Kanda au wa Wilaya anatakiwa akague shule zote 120. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huku kwenye ukaguzi wa hizi shule, huwezi kufanya mabadiliko ya elimu katika nchi hii. Kama Mdhibiti Ubora hana vifaa, na wala hawezi kwenda kuzifikia hizo shule, akikagua shule Mdhibiti Ubora wa Wilaya atakagua shule zilizoko pale pale Makao Makuu ya Wilaya tu, lakini kumfanya aende kilomita 160 akakague shule, Mdhibiti Ubora atapata wapi bajeti ya kumpeleka kule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikuta Mkurugenzi ambaye anakiona kile kitengo kiko kushoto, siyo cha kwake, hawezi kabisa kutoa bajeti yoyote kwenda kule kwa Mdhibiti Ubora. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anakuja hapa kufanya majumuisho yake atueleze wadhibiti ubora anakujaje kukiimarisha hiki Kitengo cha Udhibiti Ubora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo nataka kushauri Mheshimiwa Waziri ni sehemu ndogo sana. Limezungumzwa hapa hili suala la walimu wa kujitolea na walimu kufanyiwa mitihani. Mimi ni mdau wa elimu, nilikwenda Ukerewe katika ziara zangu za kawaida nikamkuta Mwalimu anafundisha *tuition* ya *English*. Yule Mwalimu nikamuuliza unafanya kazi gani? Akasema anafanya kazi ya uvuvi, ni mkokozi tu hapa, nafanya kazi ya uvuvi naloa, basi napata riziki yangu, lakini ni Mwalimu wa *English*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikampa na nauli aje Sengerema. Alipokuja Sengerema, kitengo changu mimi pale shuleni nikamwambia mfanyieni mtihani kama anaweza kufaulu huyu aje kama Mwalimu wa *English* hapa. Nimemkuta anafundisha wanafunzi Ukerewe. Baadaye naletewa matokeo naambiwa yule Mwalimu hana uwezo kabisa, tumempa mtihani amefeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu amepigwa jua kijijini, amekwenda kuloa, mtu analima bustani, mwalimu amesoma miaka mitano anatafuta kazi, unakuja kumpa mtihani wa *form* four. Nikawauliza, mmempa mtihani gani amefeli? Tumempa mtihani wa *form four* wa mwaka juzi. Nikawaambia haya ndiyo matatizo makubwa waliyonayo watu wetu. Nikasema aajiriwe hivyo hivyo. Baada ya miezi sita wananiambia bwana huyu Mwalimu ni bingwa, mwalimu ni mzuri sana, bahati nzuri amepata kazi nzuri Serikalini yuko Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hiki cha kuja kuwapa mitihani walimu ambao wamechomwa jua miaka mitano, miaka sita, miaka saba amekata tamaa bado unakuja unampa mtihani, basi tukifute hiki kitengo na hii kozi ya ualimu ifutwe katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna shida ya walimu kwenye maeneo yetu. Nchi nzima ina shida ya walimu, halafu unakuja kuwaajiri, unakwenda kuwafanyia mtihani. Ukamfanyie mtihani, anataka kufaulu aende wapi? Kwa sababu yeye ni Mwalimu, anatakiwa kuja kufundisha darasa la kwanza na darasa la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie tu jambo moja la msingi sana. Kuna vyuo vyetu vya ufundi na vyuo hivi ambavyo vilikuwa vya maendeleo ya jamii. Hivi vyuo vimetengwa katika wilaya. Hebu tujaribu kubadilisha sera yetu ya nchi. Ni kwamba hawa-*appear* mahali popote katika wilaya. Wewe Mbunge usipokumbuka kwamba kuna chuo kwenye wilaya yako, upite kwenda kumtembelea yule Mwalimu ha-*appear* halmashauri, siyo kwa Mkuu wa Wilaya, hebu angalieni sasa nao waanze kupeleka taarifa mwaweke karibu na halmashauri ili matatizo yao yaende katika halmashauri, yapite kule kwenye Kamati za Elimu, Afya na Maji ili nao kila *quarter* watoe taarifa zao na matatizo yao yaweze kujulikana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam Mwagao. Nilimtaja Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Aysharose, ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu. Awali ya yote, nitangulie kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uwekezaji mkubwa ambao ameufanya katika Sekta hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tangu alipoingia madarakani mwezi Machi, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Profesa Mkenda pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Kipanga kwa kazi kubwa wanayofanya ya kusimamia miradi yote, lakini pia kusimamia mageuzi makubwa ambayo yamefanyika katika Wizara hii ya Elimu. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa, wamefanya mapinduzi makubwa katika sekta hii ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu mingi tumeona imeboreshwa kwa kushirikiana na Wizara rafiki au iliyo jirani nao ya

TAMISEMI tumeona shule nyingi zimejengwa, madarasa, vyuo vya kati vimejengwa vingi ikiwemo vyuo vya *VETA*, na sisi wana Kilwa kwa kweli tunashukuru kwa sababu ni miongoni mwa maeneo ambayo yamenufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kilwa kuna shule tano ambazo zilikuwa shule shikizi. Kutokana na uwekezaji mkubwa ambao umefanyika katika shule zetu za Namandugutungu, Kitope, Mbelenje pamoja na Masaninga sasa zimegeuka kuwa shule kamili za msingi na zimesajiliwa, sasa zinatoa elimu ya msingi, tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye miradi ya *SEQUIP* wameisimamia vizuri kwa kushirikiana na TAMISEMI kiasi kwamba tumeweza kujengewa shule tano katika Wilaya ya Kilwa. Kuna Shule ya Sekondari ya Ngome, Mavuji, Somanga, Namandugutungu na sasa tuko katika hatua za umaliziaji katika Shule ya Sekondari ya Mtekimwaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunayo shule ya amali katika kata ya Rihimaliyao katika Kijiji cha Kisongo, iko katika hatua ya awali ya utekelezaji wa ule mradi. Kwa ujumla, *SEQUIP plus,* mradi huu wa Shule ya Amali tayari tumeshaletewa zaidi ya shilingi bilioni tatu. Kwa hiyo, yote hayo yanatufanya tuishukuru sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa ambayo imefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumejengewa shule kamili kule Kinywanywa. Baada ya kuwa shule yetu iko katika hali mbaya, Serikali ililiona hilo tulipowasilisha hoja yetu kwao na ile shule imeshakamilika, na sasa inafundisha wanafunzi zaidi ya 300 pale, shule yenye *equipments* zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme, tuna chuo cha *VETA,* nasi ni miongoni mwa wanufaika wa vyuo 64 vya *VETA* vinavyojengwa hapa nchini. *Progress* yake ni nzuri, na kinaendelea kujengwa. Ni matumaini yetu katika msimu ujao wa masomo, basi kitaanza kudahili wanafunzi kwa ajili ya masomo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba *branch* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inajengwa pale Lindi Mjini. Ni matumaini yetu kwamba ndani ya muda mfupi ujao kitakamilika na tutaweza kupata manufaa ya kuwepo katika chuo kikuu cha kwanza katika Mkoa wetu wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunawapongeza, kwani mtaala mlivyoubadilisha unakwenda na wakati. Hivyo, nilikuwa na mambo yafuatayo ambayo nafikiri nikiishauri Serikali, basi yataweza kusaidia kuboresha zaidi sekta yetu ya elimu. Kwanza ningependa muendelee kuangalia namna ambavyo tutaboresha hii mitaala ili iwe bora zaidi na iendane na wakati na siyo tu kwa elimu ya msingi na sekondari, basi pia tuangalie hata kule kwenye elimu zetu za vyuo vya kati na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kuna mambo ambayo yanahitajika, kwa mfano teknolojia na kadhalika. Teknolojia inabadilika kila siku, inahitaji kufundishwa katika hivyo vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la ajira. Kumekuwa na utitiri kila siku wa kuanzisha kozi mpya katika vyuo vyetu vikuu na baadhi ya kozi ambazo zinaanzishwa zinaonekana hazina tija kwenye soko la ajira. Vijana wengi wamekuwa wakihitimu, lakini mwisho wa siku wanaishia mtaani, ajira za kujiajiri hazipatikani, ajira za kuajiriwa na Serikali au taasisi binafsi hazipatikani, ajira za kuajiriwa na Serikali au taasisi binafsi hazipatikani kutokana na *nature* ya zile kozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningefikiri hapa Serikali ijaribu kuona kama inaweza ikaunda Tume ya kuchunguza hizi kozi zisiwe zinaundwa tu na vyuo bila kuzingatia mamlaka ya kiserikali na soko la ajira. Hii Tume ishirikiane na waajiri katika kubaini taaluma au kozi nzuri zinazoweza kutolewa ambazo zinaendana na ajira kulingana na mazingira tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ningeomba vyuo vyetu vya *VETA* uwekezaji uendelee ili yale matunda tuliyokuwa tunayakusudia ya vijana wetu kupata elimu ya ufundi stadi ikiwemo Wilaya yetu ya Kilwa pale Njianne basi vianze kazi mapema na hivyo viwe na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tuko katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa hivi vyuo, na hapa katikati vilisimama simama, basi Serikali iongeze msisitizo wa kupeleka fedha ikiwezekana msimu ujao wa masomo kozi zianze kutolewa, na zitolewe katika ubora na yale majengo ya hatua ya awali ambayo yanagarimu shilingi bilioni 3.8 yaweze kukamilika na nchi nzima kwa kweli tuweze kukombolewa katika hili eneo na vijana wetu kuweza kupata hizo taaluma za ufundi stadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba tuone ajira zetu ambazo Serikali kwa miaka mfululizo imetoa, na hivi karibuni ilitangaza ajira 14,000. Tunaomba ajira ziendelee kutolewa, lakini katika eneo hili kwa sababu tuna malaki hapa, Mheshimiwa Mtanda alitoa takwimu za wilaya yake tu peke yake, nilikuwa nahesabu hapa, ana upungufu wa walimu wasiopungua 400, Kilwa tuna upungufu wa walimu wasiopungua 500. Kuna shule nyingine unakuta mwalimu ni mmoja anaweza akawa ni mwalimu wa *arts* au wa sayansi, sasa masomo mengine yale ya michepuo mingine sijui yanafundishwaje!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri katika eneo hili, tuangalie vilevile ukubwa wa tatizo ili tuone ni lini tutamaliza hii changamoto, kwa sababu shule zimefunguliwa nyingi za msingi maradufu, lakini pia zimefunguliwa shule za sekondari nyingi vyuo vya kati vingi, vyuo vikuu vingi, lakini kasi ya ajira haiendani na idadi ya ongezeko la wanafunzi sambamba na shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba eneo hili liangaliwe, walimu waendelee kuajiriwa, na pia tuangalie maslahi ya walimu pamoja na wadhibiti ubora. Naishukuru Serikali kwa wadhibiti ubora ilisikia kilio ambacho mimi na baadhi ya Wabunge tulizungumza kwa miaka mitatu mfululizo. Wameweza kupewa ile

posho ya Madaraka, wameanza kupewa, lakini imetolewa kwa ubaguzi baguzi hivi. Wanataka lazima uwe na sifa sijui ya *Master's* ya *Education,* lakini tayari wameshapewa vyeo vile vya kuwa wadhibiti ubora wa wilaya, na wa mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningefikiri *criteria* iwe cheo alichotunukiwa. Kama ameshatunukiwa cheo, anastahili kupewa haki zake zote. Kwa hiyo, na wale walimu basi tuwaangalie nyumba, tuangalie na mazingira ya shule. Tumefungua shule mpya, zina vyoo vya kisasa, zina madarasa ya kisasa, lakini unakuta kuna baadhi ya maeneo hakuna maji. Huduma ya maji haipo. Tupeleke huduma kama hizo, tupeleke huduma kama za umeme ili hata wale wanafunzi ambao wanafundishwa TEHAMA waweze kujifunza kweli kweli, isiwe tu TEHAMA imeandikwa kwenye *theory* na kwenye mitaala yetu lakini *practically* haifanyiki. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hapo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Ndulane. Nilimtaja Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, na Mheshimiwa Nusrat Hanje, ajiandae.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kuweza kuijadili hoja hii. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa aliofanya katika sekta ya elimu, na pia kwa mapinduzi makubwa aliyoyafanya katika sera hii ya elimu. Hakika tunampongeza na tunaona dhamira yake ya dhati ya kuweza kumkomboa mtoto wa Kitanzania kuhakikisha anapata elimu iliyokuwa bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kujenga vyuo vya *VETA* katika wilaya zangu zote za Singida, lakini changamoto kubwa iliyoko vyuo hivi, bado havijakamilika ujenzi wake. Kwa mfano, Wilaya ya Iramba tuna chuo chetu kizuri kinachoendelea kujengwa, lakini bado hakijakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iweze kukamilisha chuo hiki kwa sababu mahitaji ni mkubwa sana. Hata hivyo, kiko chuo cha *VETA* Manyoni, nacho pia hakijakamilika. Naiomba Serikali iweze kuleta fedha za kutosha ili chuo hiki kikamilike kwa sababu kukamilika kwa chuo hiki ni mkombozi mkubwa sana kwa vijana wetu kujikomboa na kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa namna ambavyo wameendelea kusisitiza shule zetu za sekondari kusoma kwa njia ya *TEHAMA*, lakini changamoto kubwa ninayoiona katika shule hizi, kweli wameshaanza kusoma, lakini hakuna vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja ku-*wind* hapa, atuambie ni mkakati upi ambao amejipanga kuhakikisha kwamba vifaa vya *TEHAMA* vinapatikana katika shule zetu za sekondari, lakini pia katika vyuo vyetu vya *VETA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia tathmini iweze kufanyika kwa vyuo vya *VETA* kwa sababu vyuo hivi vipo, vimejengwa vizuri, lakini vina uhaba mkubwa wa walimu, vitendea kazi katika karakana zetu yakiwepo magari. Kwa mfano, Chuo cha *VETA* cha Ikungi kina changamoto kubwa sana ya uhaba wa vifaa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri tupate vifaa katika chuo hiki, chuo ni kizuri, chuo kinapendeza, lakini hakina vitendea kazi katika karakana na walimu wa kutosha hakuna. Kwa hiyo, naomba suala hilo lichukuliwe kwa kipaumbele kikubwa. *(Makofi)*

*Hapa, Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia, naomba Serikali ifanye tathmini ya vyuo vyote vya *VETA* nchini kwa maana ya ubora na mahitaji, kwa sababu kila Mbunge aliyesimama hapa amechangia uhaba wa walimu; kama siyo uhaba wa walimu, basi vitendea kazi. Kwa hiyo, maana ya uwepo wa vyuo hivi, ni vitendea kazi, walimu pamoja na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulichangia ni walimu waweze kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya mafunzo kazini ili sasa tuendane na teknolojia iliyopo. Kwa sababu walimu wengi wanafundisha, lakini changamoto kubwa wanakuwa wanafundisha kutokana na jambo la kipindi cha zamani. Ninaamini kwamba endapo watapata fedha za kutosha kwa ajili ya mafunzo, wataweza kwenda kufundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Yustina Rahhi, ajiandae Mheshimiwa Samweli.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa, kwa dhati ya moyo wangu naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa anayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeona ni Wizara pekee ambayo imeleta *reforms* nyingi sana na ni kwa ajili ya maboresho na maisha ya Watanzania, hongereni sana. Ndiyo maana utaona kwamba katika malengo ya *millennia* Tanzania tulifanya vizuri sana katika lengo la pili, kwa sababu kila mtoto aliyezaliwa Tanzania alipata haki ya kusoma elimu ya msingi na tumefanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakubaliana na watu kwamba Tanzania tunahitaji uwekezaji na bajeti ya kutosha katika Wizara ya Elimu. Kwa kuwa elimu, kusema ukweli ndiyo *key factor* katika kuleta mabadiliko, tunapambana na maadui watatu toka tumepata elimu, lakini tukiweza elimu vizuri, nafikiri ndiyo itakuwa rahisi kupambana na magonjwa na umaskini na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kuhusu shule za sekondari za kata na mchango wangu nauelekeza kuhusu ulazima au umuhimu wa sekondari za kata kuwa na mabweni au hosteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo yenye jiografia ngumu kabisa, kwa mfano Manyara. Manyara ukiangalia wilaya za Kiteto, na Simanjiro, kuna watoto ambao bado wanatembea kilomita 10 – 15 wakienda shuleni. Wanaamka usiku maeneo yale pori kwa pori hatari ya Wanyama, mvua ikinyesha ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imekuwa ni sababu ya watoto kutokufanya vizuri kwenye ufaulu na imekuwa ni sababu kubwa ya *dropout* ya wanafunzi wengine kutokumaliza shule. Kuna maeneo mengine ambapo *form four* na *form six* wanabaki jioni kwa ajili ya kipindi wanachoita *prep* ili wa-*discuss* na wenzao, wanabaki mpaka saa nne usiku na imekuwa adha kwa wazazi kuwasubiria na kuwafuata wanafunzi hawa usiku, ukizingatia maeneo mengine usafiri wana namna hiyo hakuna, na hakuna anayeweza kumudu kuwalipia pikipiki kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naipongeza Serikali na waasisi waliokuwepo kufikiria kuwa na shule za kata. Hizi shule za kata imekuwa ni sababu ya watoto wa Tanzania kupata elimu ya sekondari. Pengine zisingekuwepo na wasingepata elimu ya sekondari, na kwa sasa hivi tunaona kwamba kata kwa zaidi ya 98% zina sekondari na nyingine zina sekondari moja mpaka nne. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri mchango wangu ni kwamba, tunahitaji *quality* ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatufikirii tena kuwa na madarasa mengi, na kuwe na shule nyingi. Sasa ili tuwe na *quality* na kuongeza ufaulu; naomba kabisa kwenye hizi za kata kuliko kuendelea kuongeza shule, sasa hivi twende kwenye kujenga mabweni *(hostel)*. Kuna shule chache zimejenga *hostel* kwa ajili ya watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sahihi kabisa kum-*protect* mtoto wa kike kwa sababu madhara makubwa na mabaya yalikuwa yanabaki kwa mtoto wa kike. Kama ni mimba, *whatsoever* itaonekana kwa mtoto wa kike, hata kama ni ya mwanafunzi mwenzake au ni ya Mwalimu, lakini ukweli ni kwamba hata watoto wa kiume wanaharibika. Watoto wa kiume tunawategemea ndio Taifa la kesho, ndiyo wababa wa kesho na vichwa vya kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huku katikati watoto wanavuta bangi na kujifunza tabia nyingi mbaya. Kwa hiyo, tusibaki kusema kwamba *hostel* ni za watoto wa kike, wote wanastahili *hostel*. Naomba tu kabisa kwamba sasa hivi Tanzania tubadilishe mfumo wetu na maoni kuona tu kwamba ikishakuwa shule ya sekondari iwe *hostel* (bweni) ili watoto sasa twende kwenye *exposure*. Mtoto anasoma shule ya msingi hapo hapo, anakwenda sekondari, watu hao hao, anajifunza *exposure* ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bora sasa kama tuna *hostel,* mtoto wa wilaya moja anaweza kwenda wilaya nyingine, lakini kwenye shule hizi kuwe na maabara pia. Tunawashawishi watoto wetu wasome sayansi na sayansi ni vitendo. Hivi ni vitu gani kwa watoto wa Tanzania vinavyowavutia wasome sayansi?

Mheshimiwa Naibu Spika, maabara hamna, kuna vyumba vya madarasa vilivyobaki ndiyo tunasema hiki tutafanya maabara ya *Physics, Chemistry* na *Biology*. Wanasoma nini hakuna vifaa kule? Nafikiri sasa ni mabweni, tuongeze maabara, *library* na mabwalo ili sasa tuwe na elimu iliyo bora kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni juu ya shule za watoto wenye mahitaji maalum. Naipongeza sana Serikali kwa kujenga hizi shule za watoto wenye mahitaji maalum. Zamani ilikuwa tabia wazazi wanawaficha hawa watoto hawawezi kuwatoa. Sasa imeleta ahueni kubwa kwa sababu wanawapeleka hawa watoto kwenye hizi shule na ndiyo maana wanafunzi wanaosoma kwenye hizi shule za mahitaji maalum, shule ikifungwa wanalia kurudishwa nyumbani. Anajua akirudishwa nyumbani bado ataenda kufungiwa ndani ili mama aende kwenye ujasiriamali au shambani. Kwa hiyo, napongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiomba, wapatikane au waajiriwe walimu wenye uwezo mkubwa wanaoweza kukaa na hawa watoto kama walezi na walimu. Kingine ni hivi vifaa vya kuwasaidia hawa watoto. Wamechangia wenzangu kwamba hivi vifaa vinasambazwa na Serikali pamoja na taasisi zisizo za kiserikali, vipelekwe shuleni moja kwa moja. Pia, tumesikia gharama yake ni kubwa sana ndiyo maana tumeomba pengine unafuu wa kodi au kupewa ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na ushauri kwamba, tuna taasisi zetu za ndani; kuna *KMTC*, *SIDO* na *CAMARTEC,* hizi zina uwezo mkubwa sana wa kutengeneza hivi vifaa. Ndiyo maana tumeomba vitengenezwe hata vifaa vya hospitalini. Ni kwa nini tusijenge *internal capacity* tukawapa kazi hawa wakatengeneza hivi vifaa vya kuwasaidia watoto kusoma ili hata vijana wetu wanaomaliza shule za ufundi wapate ajira huku? Inakuwa *demand driven,* tunavihitaji hivi vitu na vijana wapate ajira na pengine vikapatikana kwa bei ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sana, *KMTC* ni wabunifu wazuri na wana uwezo mkubwa sana wa kuvitengeneza hivi vitu. Tuwape kazi watutengenezee kuliko tunavyo-*order* vingi vinatoka nje kama China na kwingine, na ni kwa gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine mchango wangu ni kuhusu vyuo vya kati na vyuo vikuu. Vyuo vya kati na vyuo vikuu kwa kweli vina uchakavu wa kutosha. Naipongeza Serikali, tumefanya ukarabati wa kutosha kwenye shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule nyingine za msingi na shule shikizi, ukiziona utafikiri ndiyo chuo kikuu, maana ina madarasa mazuri, yana *tiles, gypsum board* na vingine, lakini ukienda vyuo vya kati vimechakaa. Hata njia ya kwenda kwenye hivyo vyuo huwezi kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafikiri kwamba vile vyuo vina fedha zao za ndani za kuweza kukarabati, lakini vinazidiwa. Naomba Serikali iangalie hilo, iwasaidie. Nami kwa Mkoa wa Manyara, naomba Mheshimiwa Waziri atujengee chuo kikuu. Tulishatenga eneo la ujenzi wa chuo kikuu katika Wilaya ya Hanang, kwa hiyo, tunaomba sana, na Mkoa huo ni mpya uwe na chuo kikuu ili kwamba kwenye *chart* ya dunia watuone tu kwamba tunafanya vizuri, nami napendekeza kiwe chuo cha kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kuhusu kasi ya kuweka vyuo au shule za amali. Kusema ukweli kutokana na changamoto kubwa ya ajira ya vijana wetu tuliyonayo, mtazamo wa kuanzisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 89 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Waombeaji Taifa na Mheshimiwa Rais kutoka mikoa mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 109 na walimu watatu wa Shule ya Mfano Mtemi Mazengo kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa namwita tena Mheshimiwa Hhayuma na Mheshimiwa Nusrat ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwanza kwa kuweka msukumo mkubwa kwenye mapitio ya mitaala yetu ili mitaala iboreshwe iweze kuendana na hali halisi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha *Samia Scholarship* ambapo vijana waliofanya vizuri wanapata *scholarship* ya Mheshimiwa Rais, wanasoma bure na tunapata wataalamu. Vilevile, nampongeza kwa kuanzisha *Samia Innovation Fund* ambayo itatoa mikopo ya riba nafuu kwa watafiti ambao watazibiasharisha bidhaa zao ambazo zimetokana na utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Prof. Mkenda; Naibu Waziri, Mheshimiwa Kipanga; na Katibu Mkuu, Prof. Nombo, kwa kusimamia maono mapana ya Mheshimiwa Rais katika kuimarisha elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashukuru, niliomba sana kujengewa *VETA* pale kwangu Hanang, ujenzi umeanza. Pia, Mheshimiwa Waziri anakumbuka nilikwenda kwake nikilia kwamba idara ya ukaguzi haina usafiri (gari) na alinipatia lile gari. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya kushauri. Tumekuwa na hili suala la mitaala. Jana baadhi ya Wabunge walikuwa wakilalamika kwamba masomo gani watu wasome na masomo gani yasisomwe. Nafikiri yote haya tunahangaika na tuna watoto wengi ambao wamesoma na vijana wapo mtaani hawana

ajira, na ukiitisha tu nafasi kwa sasa hivi maelfu kwa maelfu ya watu wanajitokeza kwa sababu hawana kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri sasa ni wakati mwafaka kozi zetu tunazozifundisha na aina ya elimu tunayoitoa tuangalie mahitaji ya nchi, siyo tunatoa tu elimu. Tunao walimu wengi mtaani: wa Historia, na wa Jiografia ambapo wenye *degree* sasa wanapelekwa shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeandaa walimu, lakini hawana nafasi ya kuajiriwa. Hebu tuangalie kweli zile kozi tunazozitoa, vyuo vinachukua ada, sawa, wanajitengenezea kipato. Hao vijana tunaowapa elimu, wana sehemu ya kwenda kufanya kazi? Nafikiri hilo tuna sababu ya kuliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuwaelimishe Watanzania, tunapowaambia kutafuta taaluma au kutafuta *knowledge* tunamaanisha nini? Ili hatimaye kila mtu kwenye ndoto yake ndiyo atafute taaluma. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa sababu sasa tumeanza kuwekeza zaidi kwenye elimu ya ufundi na elimu ya amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kubwa ya watoto wetu kuacha shule. Amechangia Mheshimiwa Rahhi hapa sasa, kwamba kikubwa ambacho kinahitajika kwa sasa kwa shule tulizonazo, tujenge mabweni kwa sababu kinachowafanya watoto waache shule ni mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanatembea zaidi ya kilometa 18 kuifuata shule. Akihangaika hivyo mpaka aweze kutoboa, mwisho ataacha shule katikati. Watoto wa kike watapata ujauzito kwa sababu ya mazingira magumu na wengine wamepangisha geto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumejenga shule, tuangalie namna ambavyo tunaweza kuboresha mazingira ya watoto wetu kujifunza na mazingira ya watoto kusoma. Kingine badala ya

kujenga shule, inawezekana maeneo mengine tunafikiria kujenga shule mbili za kata. Tuangalie namna ya kuchanganya zile shule. Maeneo ya watoto ambao wanatoka mbali tuhakikishe angalau wanapata mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo kata sasa hivi unakuta kata moja inakimbilia kujenga shule tatu. Tuna changamoto ya walimu kukidhi mahitaji ya walimu kwa shule nyingi, hivyo ni ngumu. Kwa hiyo, ili angalau kuziba tofauti hiyo ya mahitaji ya walimu kwa kila shule ambayo inajitokeza, kwa sababu tukijenga shule nyingi tutahitaji walimu zaidi badala yake tuangalie namna ya kuboresha miundombinu iliyopo na namna ya kuwaweka watoto vizuri ili kuhakikisha kwamba wanasoma na wanapata elimu kwenye mazingira ambayo ni mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la elimu ya vyuo vikuu hasa kwenye eneo la mikopo. Wanafunzi wengi wa vijijini wana changamoto ya kupata mikopo ya elimu ya juu. Hii inatokana na utaratibu ambao tumejiwekea kwamba mtoto akisoma shule za binafsi, nafasi ya kukopeshwa inapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi wengi kwa mazingira ya elimu ilivyo sasa anapambana wakati mwingine wazazi wanauza mashamba kuhakikisha angalau mtoto wake anafaulu kwenye elimu za sekondari aweze kuingia chuo kikuu. Anapofika chuo kikuu, vigezo ambavyo vinaangaliwa vinawaacha watoto ambao wazazi wao wamehangaika kuhakikisha kwamba wanasoma kwa kuuza rasilimali za familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto hao sasa vigezo vinawatoa kwa sababu wao wamesoma shule binafsi. Hili eneo naomba liangaliwe kwa sababu anayeomba mkopo kama inawezekana akopeshwe na mazingira ambapo watoto hawa wamepita tuyaangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao watoto wengi wanakuja kwa Wabunge kwamba, "nimeomba mkopo nimekosa". Pia, wako

watoto ambao wamebaki nyumbani kwa sababu ya kukosa ada ya kulipa chuo kikuu. Tuangalie eneo hili tuweze kuliboresha. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa kuongeza fedha za kuwakopesha watoto wetu, lakini sasa vile vigezo tuviangalie. Kuna wengine wanakwama kwa sababu ya mazingira ambayo walipitia kabla ya kuomba mkopo wa chuo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nimejaribu kuangalia ni eneo la utafiti. Kitu kikubwa ambacho nilikuwa naangalia, ni kwamba kuna fedha kiasi gani kwenye eneo hilo. Nchi yetu ili tuweze kujitegemea na ili tuwe na teknolojia ambazo watu wetu watazipenda ni lazima ziwe zimetafitiwa na hatimaye ile *finishing* ya *products* zetu ziwavutie wanunuzi wa hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufikia huko, ni lazima tuweke fedha. Nimeangalia kwenye eneo hili la utafiti, fedha pekee niliyoona ni *Samia Innovation Fund* shilingi bilioni 2.3. Hizi ni fedha kidogo. Tukitaka kulitengeneza Taifa letu na tukitaka kuendeleza eneo la utafiti, hii itatufanya maprofesa wetu wahangaike kutafuta vyanzo vingine vya mapato ili waweze kuendesha maisha yao badala ya kubaki maabara, wafanye utafiti na hatimaye waweze kuja na teknolojia mbalimbali zitakazosaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, niseme naunga mkono hoja ili Mheshimiwa Prof. Mkenda akapambane na akaboreshe elimu yetu, ahakikishe kwamba elimu ya Watanzania inaendana na mazingira yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Nusrat, Mheshimiwa Sitta na Mheshimiwa Juwakali jiandaeni.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kuwapongeza Mawaziri pamoja na Katibu Mkuu Profesa Carolyne pamoja na

Mheshimiwa Profesa Mkenda na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kipanga kwa kazi ambayo wanaendelea kuifanya. Mimi ni Mjumbe wa Kamati na tumekuwa tunafanya nao kazi wakati wote na tunaona *willingness* yao kuhakikisha kwamba tunasogea katika upande wa elimu, tunafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia watumishi/watendaji wa Wizara tumekuwa nao kwenye kazi kipindi chote hiki tangu hii Kamati mpya, kwa sababu hii ni Kamati mpya, sasa hivi inashughulika na masuala ya elimu zaidi. Kwa hiyo, tumejadili mambo mengi kwa kina. Kuna mambo mengine ambayo wakati mwanzo haikuwepo hii Kamati, maana yake kuna vitu tulikuwa hatuvijui, lakini tangu imekuwepo, tumechakata mambo mengi sana kwa ukaribu, na kwa kina kwa muda wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia maeneo machache sana. Waheshimiwa Wabunge wamechangia, nami pia naunga mkono maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusiana na mambo kadhaa ambayo tumeyajadili. Yote ni sisi tumejadili na tumekubaliana kama Kamati kwa niaba ya Bunge, lakini mimi nitachangia upande wa ubora wa elimu kwa sababu katika vile vipaumbele, Serikali imeweka kipaumbele cha kuboresha elimu ya awali, msingi na sekondari pamoja na upande wa amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukizungumza ubora wa elimu, kuna vitu vingi ambavyo tunaviangalia na kwa sababu hii ndiyo bajeti ya mwisho kwa miaka hii mitano tangu tumeanza kujadili nitaomba niongee mambo kadhaa. Jambo la kwanza, tunapoizungumzia Tanzania, tunazungumza mambo matano ya msingi. Tunazungumza maeneo matano ya kisekta ya msingi ambapo mengine yanaingia humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiizungumzia Tanzania, sekta ya kwanza, tunazungumzia kilimo; tukiizungumzia Tanzania tunazungumzia *logistics;* tukiizungumzia Tanzania tunazungumzia *extractive industry* (sekta ya uziduaji); na pia tukiizungumzia Tanzania tunazungumzia utalii, vilevile tukiizungumzia Tanzania tunazungumzia

*trade and industry* (viwanda na biashara); na tukiizungumzia Tanzania kitu kingine ambacho kina-*cut across* hizo sekta zote ni *human capital development* (maendeleo ya watu).

Mheshimiwa Naibu Spika, walipata kuandika waandishi wa vitabu mahiri duniani wakieleza kwamba maendeleo ya nchi yoyote duniani ni lazima yawe *people centred development* (maendeleo ambayo yanafungamanishwa na watu). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiizungumzia *human capital development* unazungumzia elimu, afya na sekta nyingine. Hata hivyo, elimu kwa upekee wake, hizi sekta zote nilizozizungumza ambazo ndiyo ukiizungumza Tanzania unazizungumza, hizi sekta zote zinategemea kuwa *informed* na mfumo wa elimu kwenye nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huwezi kuzungumza sekta ya utalii kama unataka kuifanya vizuri bila kuwekeza kwenye elimu ya watu wake. Huwezi kuzungumza sekta ya uziduaji kwa mafanikio yake makubwa bila kuzungumza elimu ya watu wa nchi husika zote hizi nilizozitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba kama ni kweli tunazungumza lugha moja kwenye hiki, kuna vitu vinatakiwa viachwe. Mwisho ni mwaka huu tunaomaliza kwenda kwenye uchaguzi, kuna baadhi ya vitu ambavyo vinakwamisha elimu yetu kwenda mbele, vinatakiwa visiwepo kabisa kabisa katika *Hansard* za Bunge, na hotuba za Wizara. Kwa mfano, kuna mambo kadhaa nimeyaandika hapa na nimeyaona kwa sababu ili Mheshimiwa Waziri Wizara yake ifanye vizuri, lazima mfumo wake wa utoaji wa elimu, watu wote wapate elimu katika mazingira yaliyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapozungumza lugha ya alama, bado siyo somo. Yaani watoto wetu hawajifunzi lugha ya alama ili wawasiliane na watoto wengine wenye changamoto za mawasiliano, lakini pia hakuna walimu wa lugha ya alama kwenye shule zetu. Maana yake umeondoa kipengele muhimu cha mawasiliano katika utolewaji wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa natamani tukirudia tena bajeti ya mwakani tuwe tumeshapata ufumbuzi wa jambo linalohusu lugha ya alama kwa sababu ni *means of communication* kama tunavyozungumza Kiswahili na Kingereza. Sisi sote humu Bungeni tunatakiwa tujue kuzungumza kwa lugha ya alama kwa sababu hao watu wapo kwenye jamii, na sisi ni watumishi ambao tunatumikia watu kwenye majimbo yetu ambao wana changamoto za usikivu na kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima sisi sote tulitakiwa wakati tunapita huko shule tuwe tumesoma somo la lugha ya alama. Tunaweza kuwasiliana na wao wanaweza kuwasiliana na sisi na hilo ni jambo la kutoa tu mwongozo, Mheshimiwa Waziri anajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachotamani kisiwepo kabisa katika kukwamisha utolewaji wa elimu nchini, leo bado tunazungumza uhaba wa matundu ya vyoo shuleni. Yaani kitu kidogo kama choo bado tunajadili tujenge matundu mangapi ya vyoo? Natamani ufike muda tumalize. Tena viwe vyoo vya kisasa kwa sababu tuna teknolojia, mifumo, vipaumbele na tunafanya *planning*. Kwa nini tusimalize haya mambo? Yaani liishe tu iwe imebaki *maintenance* ya hizo *system?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine cha tatu, kuna kundi kubwa la watoto wa kike ambao wanakosa kuhudhuria masomo eti kwa sababu wamekosa taulo za kike. Yaani una Wizara ambayo ndani yake kuna *VETA* na *SIDO,* umesema unaenda kwenye mfumo wa amali na una karakana za nchi ambazo ziko kwenye vyuo, lakini bado umeshindwa kutatua hili? Nchi nyingine wanatushangaa, unaenda eti unatafuta mwekezaji ili akusaidie taulo za kike ukawapelekee watoto shuleni kama vile ni kitu tumekianza jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, enzi na enzi tunajua binti akifika umri fulani lazima ataingia kwenye hiyo hatua. Hivi kweli tumeshindwa kama nchi kutatua hili jambo? Mpaka leo bado tunazungumza kwamba, hakuna taulo za kike! sijui tuliondoa kodi, imeshindikana

kupunguza bei, hivi tumeshindwa kuwaambia *VETA* waje na *solution*?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna pamba kwenye nchi. Tunaweza ku-*import materials* tukatengeneza sisi, TAMISEMI wakatusaidia, vyuo vya *VETA* vikawa vimetatua kabisa hilo jambo likawa limeisha. Natamani lisiwepo kwa sababu, linakosesha watoto wetu kupata elimu. Kuna watu wengine ambao wako kwenye kaya maskini hawawezi ku-*afford,* ni gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni vifaa vya watu wenye ulemavu. Serikali imeweka mwongozo wa elimu jumuishi, lakini tuna changamoto kubwa ya vifaa vya watu wenye ulemavu, hasa wanafunzi. Tanzania tunazalisha asilimia tano tu ya vifaa ambavyo vinatolewa kwenye hii nchi, lakini 70% na zaidi vinatoka nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza pia Waheshimiwa wengine hapa, yaani tunashindwa kuelewa kwa sababu, *VETA* iko chini ya Wizara hiyo hiyo, hawa wanafunzi wanasoma Wizara hiyo hiyo, yaani tumeshindwa kufanya *roll call* kujua ni watoto wangapi wenye uhitaji, ili tutumie mifumo yetu ambayo tuna-*inject* fedha kule, ili tutatue hili jambo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anatakiwa ajue miongoni mwa vitu ambavyo vinasababisha elimu katika Wizara yake isitolewe katika mazingira yanayostahiki ni pamoja na upatikanaji wa vifaa vya watu wenye ulemavu. Kwanza kwenye ulemavu kuna unaoonekana na usioonekana. Hata watoto kutokuwa na utulivu darasani wakati wanafundishwa, wakaelewa kirahisi pia ni ulemavu usioonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna vituo 12 Tanzania vya kupima ulemavu usioonekana kabla watoto hawajaenda shuleni. Mwongozo wa elimu jumuishi unasema kwamba, kila halmashauri inatakiwa iwe na kituo. Labda hapa niongee taratibu, yaani watoto

kabla hawajaenda darasani kusoma wanatakiwa wapimwe ili waonekane wanasikia vizuri, wanaona vizuri au ni *ADHD*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, kuna watoto wengine wanachelewa kuelewa, kwa hiyo, huwezi kum-*treat* kama wengine. Ndiyo inasababisha unaweka *Form One A, Form One B, Form One C,* yaani wale C ndio wale wa mwisho kule, halafu hawa A ndio wenye akili, unaanza kuwabagua tangu kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri hivi vitu vinatakiwa viangaliwe ili kuhakikisha kwamba, elimu yetu inatupeleka mbele.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mengine mwandikie Mheshimiwa Waziri.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Sitta dakika tano, Mheshimiwa Latifa Juwakali dakika tano. Jiandae Naibu Waziri.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwa kifupi hoja iliyoko Mezani. Kwanza, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Daktari Samia na Serikali yake anayoiongoza, kwa jinsi ambavyo ametilia mkazo sana suala la elimu na maisha ni elimu, kila kitu ni elimu halafu mengine yote yanafuata. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa jinsi ambavyo

wameishika hii Wizara. Tunaamini kabisa elimu itaimarika nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda niliopata wa dakika tano, naomba nijikite zaidi kwanza, kwa niaba ya Wananchi wa Urambo, kuishukuru Serikali kwa kutupa *VETA*. Sisi wananchi wa Urambo tuliona mafunzo ya ufundi ni muhimu sana maishani, hasa vijana wetu, ili waweze kujikita katika maisha yao, wajiendeleze wenyewe kiuchumi kwa kupitia mafunzo ya ufundi. Ndiyo maana tukachelewa kungojea majengo mapya, tukatumia majengo yaliyokuwa kambi ya ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, tunaishukuru Serikali kwa kukubali ombi letu, lakini tunarudi kuiomba Serikali itusaidie kuongeza majengo zaidi ili tuongeze *study* zaidi kuliko zile tulizonazo kwa sababu, tuna upungufu wa karakana, mabweni na majengo mengine. Kwa hiyo, tutashukuru sana Serikali ikifikiria kutuongezea majengo pamoja na walimu, ili vijana wetu wa Urambo wapate mafunzo ya kuwasaidia maishani mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo haya yanayozungumziwa, ya ufundi ya amali, ni muhimu sana nchini kwetu, lakini unapozungumzia elimu yoyote, iwe ya ufundi, nadharia, jambo muhimu la kuwaza ni walimu. Kwa hiyo, tunaomba kwa heshima na taadhima kabisa Wizara itakapokuwa inakamilisha hotuba yake, basi ituelezee mpango mzima wa kupata walimu kwa sababu, ukisema tu elimu, lazima walimu namba moja na mengine yanafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kujua suala la kupata walimu na sasa hivi hili zoezi lililopita, la kupata walimu kwa kweli, naona kidogo Serikali ingeliangalia upya. Walimu hawa wamesoma miaka minne, miaka mitatu kule waliko pia, wakapitishwa kwenye mtihani. Naiomba Serikali ione kweli, kulikuwa na umuhimu wa kuwapitisha kwenye mitihani tena?

Mheshimiwa naibu spika, kwa hiyo, nafikiria watu waliohitimu tayari, bado wanarudishwa kwenye mitihani? Nafikiri ni jambo ambalo Serikali ingeliangalia kwamba, je, kuna umuhimu wa kuwapitisha tena walimu kwenye mitihani ile baada ya kukaa vyuoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nafikiria kwamba, kwa sababu hivi vyuo vya ufundi na amali, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, ni muhimu sana, naomba tuangalie kwamba, kutokana na mahitaji makubwa ya walimu, je, Serikali haiwezi kuja na mpango wa posho fulani, kama vile wanavyopata walimu wanapojitolea kwenye shule sasa hivi kabla hawajaajiriwa? Je, Serikali inaweza kufikiria mpango wa kupata posho ili walimu wale tunaowahitaji kwa sasa hivi wapate posho wanapojitolea?

Mheshimiwa Naibu Spika, watakapotangaza ajira, hawa walimu wanaojitolea ndio wawe wa kwanza kuajiriwa. Sasa tunaomba Serikali ione, kama je, iko tayari kupata posho kwa hawa walimu wanaojitolea?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la muhimu sana kutokana na mafunzo ya ufundi, kulikuwa kuna kitu kinaitwa *Skills Development Levy*. Je tunaitumiaje? Kwa sababu, *Skills Development Levy* ililetwa, kwa ajili ya kukuza mafunzo hayo. Ndiyo tunaitumiaje? Sheria ilivyosema ndivyo inavyotumika sasa hivi? Nafikiri ni jambo ambalo lingeangaliwa sana, je, tumewaandaa wenye viwanda wawe tayari kuwapa nafasi wanafunzi kufanya majaribio wakati vyuo vinapofungwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi nyingine wameweka sheria ya kuwataka wenye viwanda kutoa nafasi kwa vijana wanaojifunza mafunzo haya wafanye majaribio wakati wanapokuwa likizo. Kwa hiyo, nafikiri ni jambo la msingi sana kukubalika, kupewa nafasi ya majaribio kwenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana vyuo vya *VETA*, mafunzo yanayotolewa yalenge sana mahitaji ya maeneo. Kama

watu wanachimba dhahabu au nini, basi mafunzo ya *VETA* yalenge kupunguza changamoto za maeneo yanayohusika kutokana na ujuzi wanaoupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawapongeza sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi kubwa wanayofanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Latifa dakika tano, jiandae Naibu Waziri.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Elimu. Kwanza, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari Samia Suluhu Hassan, kwa mapinduzi na maboresho makubwa yanayoendelea kufanyika katika Wizara yetu hii ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nampongeza pia, Waziri wetu wa Elimu, Naibu Waziri wa Elimu, viongozi wote na watendaji wote wa Wizara ya Elimu. Kutokana na muda, mchango wangu naomba nijielekeze katika maeneo matatu. Eneo la kwanza litakuwa ni Mikopo ya Elimu ya Juu; eneo la pili ni Vyuo vya *VETA* na eneo la tatu ni Udhibiti wa Ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba Mheshimiwa Rais amefanya maboresho na mapinduzi makubwa katika miundombinu, ikiwemo kujenga shule mbalimbali na kujenga matundu ya vyoo. Nataka nizungumzie hili suala la mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuboresha upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wetu wa elimu ya juu. Tunajua kwamba, sasa hivi wanafunzi wetu wengi wanapata mikopo ya elimu ya juu tena kwa wakati unaostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba, nchi nyingine ambazo zimeendelea huko, elimu ni *service* na tunamshukuru Mheshimiwa Rais, mbali ya kuwa kunatolewa mikopo ya elimu ya juu, fedha zinakwenda, tunajua kwamba, kuna *Samia Scholarship*. Serikali waendelee kulichukua hili kwamba, kwa sababu tumefanya maboresho makubwa katika mikopo hii na ninaiona dira, ninaona mwelekeo na ninaona kiu ya Mheshimiwa Rais ya kuendelea kuwasaidia wananchi na vijana ambao ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo haja ya kuwasaidia hao wanafunzi wetu ambao wanatoka katika familia maskini, angalau basi wapatiwe hata elimu bure katika vyuo vikuu. Hii itaweza kuwasaidia wao, lakini kuwa wanafunzi wa mfano wa kuendelea kuisemea Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niendelee katika suala hili la vyuo vya *VETA*. Sisi tunafahamu kwamba, sasa hivi Serikali yetu inajiandaa katika kumalizia vituo vyetu hivi vya *VETA* katika nchi nzima. Nataka niipongeze Serikali kwa sababu, katika bajeti zilizopita tulilizungumzia sana katika Bunge lile lililopita, ili kuona tunafanya maboresho na marekebisho ya mitaala ya elimu. Kimoja ambacho tulikuwa tunakizungumzia, ni kuona kwamba, tunaboresha vituo vyetu vya *VETA* ili wanafunzi waweze kupata ujuzi, waweze kujiajiri na kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali yangu kwamba bora tuchelewe, lakini tufanye vitu kwa uhakika na ninaomba hili tulichukue. Tufanye vitu kwa uhakika, tumeshajenga *VETA*, tutafute hata vituo vya *VETA* 63 hata nusu ya vituo vya *VETA* tulivyovijenga, lakini tuhakikishe mahitaji ambayo yanahitajika katika vituo vile yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya maboresho makubwa na imetoa fedha nyingi sana. Haitapendeza kwamba, tunaenda katika vituo hivyo vya *VETA,* mwanafunzi anaenda kujifunza kutengeneza magari, lakini katika kituo hicho cha *VETA*

hakuna karakana. Naamini kwamba, tutakuwa bado hatujawasaidia na hatutaweza kufikia lengo tulilokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa haraka haraka, naomba nimalizie na hili suala la udhibiti ubora. Hawa wadhibiti ubora wanaajiriwa au wanasimamiwa na Wizara ya Elimu, lakini cha kushangaza hawa wanafanya kazi kwenye halmashauri. Huwezi kufanya kazi ipasavyo, kama mtu ambaye unamsimamia, ndio ambaye anakulipa au ndio anaku-*supervise*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara, hili walichukue. Hao wadhibiti ubora waendelee kuwasimamia wao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mengine utamwandikia Waziri.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** ...na ruzuku zao zitoke kwao wawapelekee moja kwa moja, ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na

wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua elimu katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miezi kumi ya mwaka wa 2024/2025, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na TAMISEMI, imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya elimu hasa kuboresha ufaulu na hata miundombinu ya madarasa na mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imeendelea kupitia kipindi kigumu cha changamoto za kuporomoka kutoka kuongoza kimkoa katika ufaulu wa elimu ya sekondari. Pia ufaulu kwa shule za msingi unapitia katika changamoto kubwa hasa kutokana na mazingira ya shule za vijijini ikiwemo upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja kuwa ni jukumu jumuishi kwa wazazi, bado kunahitaji uharaka wa kupitia sera ya elimu kuweza kuboresha taaluma kwa shule za vijijini ambazo kwa kiasi kikubwa hazifanyi vizuri ukilinganisha na shule za mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu bado wanaendelea kufanya kazi katika mazingira magumu kwa kukosa majengo ya nyumba za kuishi. Napendekeza Serikali kupitia TAMISEMI na Wizara ya Elimu kuendelea kushirikiana na wananchi katika ujenzi wa nyumba za walimu iende sambamba na ujenzi wa maboma na pia madawati kwa wanafunzi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kuhakikisha motisha kwa walimu ili kuboresha taaluma iwe ya kiushindani kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, *SADC* na hata Afrika. Napendekeza pia Serikali itoe kipaumbele kwa kulipa madai ya malimbikizo kwa walimu, ili kupunguza muda wa kufuatilia malipo yao na badala yake waelekeze muda zaidi kwenye kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na magonjwa yasiyo ya kuambukizwa yakiwemo magojwa ya

kansa, shinikizo la damu, figo, moyo na kadhalika, narudia tena kushauri Serikali kuweka kipaumbele cha kuboresha elimu ya afya, ikiwemo upanuzi wa ujenzi wa ndaki ya Sayansi ya Afya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(Mbeya College of Health and Allied Sciences (UDSM-MCHAS)*. Serikali itoe kipaumbele cha ujenzi wa chuo hiki kutoka kwa eneo la iliyokuwa *Tanganyika Packers Ltd.,* Mbalizi Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwezesha uwekezaji na uendelezwaji wa viwanda endelevu, Tanzania inahitaji kuzalisha watalaamu wengi na hasa ujasiriamali na taaluma ya ufundi ngazi za kati na chini ambapo mahitaji ni makubwa. Pamoja na kujiwekea malengo ya kuongeza viwanda, nashauri Serikali iweke mkazo suala la uwepo wa nguvu kazi (vijana kupata mafunzo ya ufundi na ujasiriamali) ya kutosha na itakayowezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko mbalimbali hasa ya kisayansi na kiteknolojia na hata kiuchumi, yanayoendelea duniani, napongeza hatua ya Serikali kwa kuchukua hatua za kuboresha mitaala ya elimu kuwa ya kisasa zaidi ili kuendana na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka kadhaa iliyopita Tanzania imeshuhudia mafundi mchundo wengi wakiongeza *(upgrade)* ngazi za utaalamu wao kwa kusomea kozi za uhandisi wakati idadi ya mafundi mchundo wanaofuzu masomo ya ufundi mchundo ikipungua huku mafundi wa kawaida *(artisans)* wanaoongeza utaalamu wao ikiwa haiongezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imepelekea kupungua kwa kasi idadi ya mafundi mchundo pamoja na mafundi wa kawaida na hivyo kuathiri utendaji wa viwanda na sekta nyingine kwa kuwa hawa ndio wanaotenda kazi kwa mikono. Ukizingatia kuongezeka kwa uwekezaji katika viwanda, hali hii inabidi irekebishwe haraka kwa kuongeza idadi ya mafundi husika ili kukidhi mahitaji ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa uwiano wa wahandisi/mafundi mchundo/mafundi wa kawaida upo chini sana na hautaweza kuisaidia Tanzania kufikia malengo tarajiwa. Hata ukilinganisha wataalamu wa juu wa stadi mbalimbali za Taifa na wenye stadi za kati na za chini uwiano wake siyo mzuri ukilenga uwezo wa kusimamia viwanda vya kisasa kiasi cha kuhitaji marekebisho ya uwiano kama Mpango wa Taifa wa Kuendeleza Stadi Unavyotegemea *(National Skills Development Strategy)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iongeze msukumo kwenye mafunzo ya amali, mafundi mchundo na mafundi wa kawaida na pia elimu yetu ilenge mafunzo ya ujasiriamali. Hii pia ishirikishe elimu ya kujitegemea toka elimu ya awali na hata kutumia watalaamu wetu wa kilimo, mifugo na uvuvi kuanzisha mashamba darasa mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Adolph Mkenda, Mbunge na Naibu wake Mheshimiwa Omari Kipanga, Mbunge na wataalamu wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kuhusu maboresho ya kimkakati yanayohitajika katika sekta ya elimu ya juu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora ni msingi wa maendeleo ya Taifa na Tanzania, inapaswa kufanywa juhudi za makusudi na kimkakati kukabiliana na changamoto zinazoikumba sekta ya elimu, ikiwemo elimu ya juu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti umeonesha kwamba elimu ya juu ndiyo inayotoa dira na mwelekeo wa kitaifa juu ya maendeleo. Hapa duniani, nchi nyingi zilizopiga hatua kubwa kwenye maendeleo ni nchi zilizofanya mapinduzi makubwa kwenye elimu ya

juu. Kwa mfano, nchi za Marekani, China, Canada, Japan, Uingereza, Australia, Urusi, Ujerumani ni nchi zenye uchumi mkubwa. Nchi hizi zina vyuo vikuu vyenye hadhi kubwa duniani vilivyo kwenye orodha bora kutokana na tafiti wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika hata katika Bara la Afrika, vyuo vikuu vyenye hadhi kubwa katika kumi bora vingi zaidi vinatokea Afrika Kusini ikifuatiwa na Misri, na haya ndiyo Mataifa yenye uchumi mkubwa Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upimaji wa ubora wa Vyuo Vya Elimu ya Juu vya Tanzania kwa kuzingatia vigezo vya Kimataifa, vyuo vyetu havijafanya vizuri. Kwenye Bara la Afrika, kwenye vyuo bora 100, Tanzania inashika nafasi ya 26 na ya 1,614 duniani (Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam) ikifuatiwa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine) ambacho kipo nafasi ya 53 Afrika na ya 2,634 duniani na Chuo Kikuu cha Afya cha Muhimbili ambacho kipo nafasi ya 95 Afrika na cha 3,667 duniani *(https://edurank.org/geo/af/)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii, nachelea kusema kwamba hali hii inaweza kufanana na kasi ya maendeleo ya Taifa letu. Hivyo basi, ili kulikwamua Taifa letu kama wenzetu wa nchi zilizoendelea walivyofanikiwa, ni vyema tukaangalia mahali pa kuanzia kwa kuwekeza kikamilifu na kimkakati ili kutatua changamoto zinazokabili vyuo vya elimu ya juu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, kuna uhusiano mkubwa sana kati ya elimu ya juu na maendeleo ya nchi. Nalisema hili kwa sababu gunduzi kubwa duniani zenye mchango mkubwa kwenye maendeleo ya dunia hii zinafanywa na taasisi za elimu ya juu. Ni kwa maana hiyo napenda nisisitize hapa kwamba nchi yetu isipowekeza kimkakati katika elimu ya juu, itabidi tusahau kabisa kuhusu maendeleo ya nchi yetu, kwani hatutaweza kutatua matatizo ya kawaida ya wananchi wetu katika nyanja za afya, kilimo, mifugo, uvuvi, maliasili (maji, madini, utalii, nishati), utalii, ujenzi, viwanda, biashara, mazingira, ardhi, ulinzi na mambo mengine muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kulinufaisha Taifa na elimu ya juu, naishauri Serikali ichambue haya mapendekezo ya kimkakati ili kuondoa baadhi ya changamoto zinazokwamisha maendeleo ya vyuo vya elimu ya juu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali ifanye maboresho ya Sera ya Elimu na Utafiti wa Vyuo Vya Elimu ya Juu nchini. Pia napendekeza kwamba Serikali iandae sera maalumu ya kuunganisha elimu ya juu na maendeleo ya Taifa letu kwa kuzingatia mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kuboresha Sera ya Elimu ya Juu, ni vyema wakashirikishwa wadau wote muhimu kama wanachuo walio vyuoni, waliohitimu, walio kwenye ajira katika sekta husika na wadau mbalimbali wa maendeleo. Kushirikisha wadau wote hawa kutapanua wigo wa kugundua changamoto mbalimbali zilizopo kwenye jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali ifanye mapitio na maboresho ya mitaala ya vyuo vya elimu ya juu nchini. Ushirikishwaji wa wahitimu walioko kazini pamoja na wakufunzi katika mapitio ya mtaala ni muhimu ili kuamua ni vipengele gani vibaki, viongezwe au viondolewe. Mapitio haya yalenge kufundisha vijana wetu vitu vitakavyosaidia kujenga Taifa lenye maarifa, ustadi na uwezo wa kushindana katika uchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba kimkakati vyuo vya elimu ya juu nchini viwe na ushirikiano wa moja kwa moja na Halmashauri za Serikali za Mitaa. Ni jambo la heri kuhusisha vyuo vikuu katika shughuli za maendeleo ya Halmashauri za Serikali za Mitaa. Kwa kufanya hivyo, watakuwa wanajihusisha moja kwa moja na maendeleo ya wananchi na changamoto ya tafiti za wanazuoni wetu kubakia makabatini itakuwa imetatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhuisha ari ya utumishi miongoni mwa wahadhiri wa vyuo vya elimu ya juu, Serikali ihakikishe kuwa katika bajeti zake zote madeni yote ya wanataaluma ya posho ya

pango kwa wanaostahili yanalipwa, posho za kujikimu wanapokuwa kwenye majukumu na mpango wa kuboresha mafao ya wahadhiri ya uzeeni unatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la azma hii ni kuwaondolea hofu ya maisha yao ya kila siku wanataaluma wetu ili waweze kujikita kweli katika kutoa elimu, kufanya utafiti kwa utulivu, na kutoa ushauri wa kitaalam ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto kubwa katika elimu ya juu ni uhaba wa wahadhiri wenye sifa stahiki ili kuendana na ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na vyuo kufanya tafiti na ubunifu. Taarifa mbalimbali zimeonesha kwamba vyuo vyetu vikuu vya umma nchini vina uhaba mkubwa sana wa maprofesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, ili kuendelea kufaidika na utaalamu na uzoefu wa maprofesa wetu hapa nchini, nashauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza umri wa maprofesa kustaafu kutoka miaka 65 ya sasa hadi 70, na kwa wale wenye uwezo wa kufundisha, waruhusiwe kupewa mikataba hadi wanapofikisha umri wa miaka 80. Hili liamuliwe na taasisi husika maadam wamejiridhisha kuwa profesa husika bado utaalamu wake anautumia kikamilifu na unahitajika kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikatoa fursa kwa vyuo vya elimu ya juu kujiendesha kiutawala na kitaaluma, bila kuingiliwa na mamlaka nyingine za Serikali. Hii iwe ni pamoja na uhuru wa kuajiri watumishi wa kada za elimu kwa vipimo walivyojiwekea bila kuingiliwa na mamlaka zisizo za kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali ifadhili kikamilifu tafiti za kimkakati, ubunifu na kuhakikisha kuwa matokeo ya tafiti hizo yanatumika katika kuanzisha viwanda hapa nchini. Ni vyema watafiti wa vyuo vya elimu ya juu wakajengewa mazingira bora na kupatiwa ufadhili wa fedha za kutosha kufanya tafiti na bunifu mbalimbali. Serikali ikiwekeza kikamilifu kwenye hili, bunifu za watafiti wetu zitaingia sokoni na kuliletea Taifa letu maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizi zinahitaji kushughulikiwa ili kufikia lengo la elimu yetu ya juu kuchangia katika maendeleo ya kijamii na uchumi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kujengwe shule za watoto wa kiume kama zile za watoto wa kike shule za mikoa za wasichana au katika shule zile zile za watoto wa kike ziongezwe na miundombinu kama ya mabweni kwa ajili ya watoto wa kiume. Hii ni kutokana na changamoto zilizopo za ukatili sasa zinakua kwa kasi hadi kwa watoto wa kiume.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ili kutoa elimu katika usawa, basi usawa huo upimwe hata kwa watoto kupata fursa sawa za mazingira yanayotolewa elimu, ikiwemo kupata miundombinu ya mabweni kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa suala la afya ya akili, basi ni muhimu kuanzisha klabu za afya ya akili ili kuwasaidia watoto kujitambua, kuzalisha kwa tija, kupambana na changamoto na kutoa mchango chanya kwenye jamii. Mambo hayo ni muhimu kwa kila ngazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika kusimamia ubora, basi Shule ya Msingi Nduli ihamishwe ndani ya uwanja wa ndege, na watoto wapate muda wa kupata mafunzo mengine ya dini.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha mazingara mazuri zaidi ya kujifunzia ili kuwaandaa Watanzania kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa. Napongeza pia kwa kuanzishwa shule za amali kila mkoa ambazo zinakwenda kuwa mkombozi wa ajira hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Wizara ni kama ifuatavyo:-

Kwanza Wizara ipeleke wataalamu wa fani mbalimbali kama kilimo, ushonaji, ujasiriamali na fani nyingine ambazo zitawaandaa wanafunzi kujiajiri na siyo kusubir ajira.

Pili, wanafunzi wajifunze zaidi kwa vitendo.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada anazozifanya ili kuhakikisha watoto wetu wanasoma kwenye mazingira mazuri, na walimu kuboreshewa mishahara na mafao yao mengine. Hongera sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana pia Mheshimiwa Waziri wa Elimu Profesa Mkenda, kwa kazi nzuri ya kuhakikisha Wizara ya Elimu inasimamiwa vilivyo ili kupata rasilimali watu walio bora kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu kwa Wizara ya Elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza Wizara kwa kuja na mwongozo wa utambuzi wa vipawa na vipaji kwa wanafunzi wa shule zetu. Ushauri wangu ni kuwa mwongozo huu uwe jumuishi kwa maana ya kwamba utambuzi usiishie kwa wanafunzi mashuleni tu, bali uende mbali mpaka kuwatambua watu wazima wanaofanya mambo kwa kutumia vipawa na vipaji vyao vya kubuni mambo au vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tuna watu wazima wana kipaji cha kutengeneza bunduki, sera na sheria zetu zinazuia ubunifu wa aina hii na watu hawa wakipatikana wanakamatwa na kuhukumiwa kufungwa kwamba wamevunja sheria zetu. Kwa nini tusifikirie kuwa na watu hawa kwenye kambi maalumu za ufundi na

kuendeleza vipaji vyao na kuwatumia hatimaye kufanya mambo makubwa baadaye?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwangu mimi naona ni wakati muafaka sasa kwa Wizara ya Elimu kuwa Wizara ya Muungano, kama ilivyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani, Mambo ya Nje na kadhalika. Hoja yangu ni kuwa tangu enzi za kupata uhuru elimu imetumika kama nguzo mojawapo iliyotuunganisha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wa Kanda ya Ziwa walisoma Kusini na Kaskazini na Watanzania wa Kusini walisoma Shule za Kanda ya Ziwa na Kaskazini mwa nchi, na hivyo hivyo wa Magharibi walisoma Mashariki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu likiwa jambo la Muungano litafanya Utanzania wetu kuwa na mshikamano na umoja zaidi na hivyo kufanya Taifa letu kuwa moja lenye watu wamoja. Kwa maana hiyo, Watanzania walioko Pemba au Unguja watakuja kusoma Bara na Watanzania wa Bara hivyo hivyo kwenda kusoma Zanzibar hasa kuanzia kidato cha tano na sita na vyuo vikuu, na hivyo kuwafanya Watanzania wa Bara na wa Visiwani kutokuwa na utofauti wowote, na hivyo ku-*cement* zaidi umoja wetu wa Kitaifa.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jana kwenye mchango wangu wa kuzungumza nilikatizwa na hivyo sikuweza kumalizia. Naomba kutoa na kusahihisha maneno yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu maombi ya ujenzi wa vyuo vya elimu ya juu katika Wilaya ya Mbozi na Jimbo la Vwawa wananchi wa Kata ya Ipunga wametenga eneo litakalotolewa bure kwa taasisi yoyote itakayokuwa tayari kujenga chuo cha elimu ya juu. Eneo lina ukubwa wa ekari 308. Tupo tayari kulitoa bure na lipo tayari. Naomba Mheshimiwa Waziri akubali kupokea eneo hilo ili atutafutie chuo chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye Kata za Nyimbili na Hasanga kuna eneo la zaidi ya ekari 700 linafaa sana kujenga vyuo vya elimu ya juu. Pia Ihanda kando kando ya Mlima Mazuri wa Ng'amba na Kata ya Hasanga pia kuna eneo. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutusaidia kupata vyuo ambavyo vitajengwa kwenye maeneo hayo ili kuchangia katika huduma za jamii na uchumi na maendeleo ya wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni kuhusu mitaala ya elimu ya juu kushindwa kukidhi mahitaji ya soko na mabadiliko mbalimbali. Naomba Serikali ichukue hatua za kuboresha mitaala ya vyuo vingi vya elimu ya juu ili iwe ni *competency based* kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu utafiti na machapisho ya vitabu na Makala, ni vizuri vyuo vyetu vikatilia mkazo wa kufanya utafiti na kuandika vitabu na machapisho mbalimbali. Hiyo itaboresha na kuinua hadhi ya vyuo vyetu nchini na duniani. Pia hatua hiyo itavutia wanafunzi wengi kutoka nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri yeye na timu yake na kuendelea kutilia mkazo maeneo ya sayansi, teknolojia na hesabu kwa maendeleo ya nchi. Nchi itaendelea kama elimu yetu itawaandaa vijana hao kwa kupata maarifa na ujuzi vitavyowaandaa vizuri kujitegemea.

**MHE. ZULFA MMAKA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali nianze kumshukuru Mungu kwa neema ya uzima. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa suala la watoto wanaopata ujauzito wakiwa shuleni. Suala hili limepatiwa suluhisho la watoto hao kurudi shuleni baada kujifungua, ila nahisi kwamba elimu juu suala hili bado inahitajika kwenye jamii, kwa sababu inaonekana bado watoto wengi hawajarudi shuleni kwa

hofu za wazazi jinsi gani jamii itawaangalia. Kwa hiyo, ombi langu suala hili litolewe elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kujenga madarasa mengi vijijini. Hili linaenda kuondoa msongamano wa wanafunzi wengi darasa moja, ila naomba kwa upande wa matundu ya vyoo, bado ni changamoto kwa watoto wa kike na watu wenye mahitaji maalumu. Naiomba sana Serikali walitupie jicho jambo hili kwa roho ya kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AMINA BAKAR YUSSUF:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wake mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, pamoja na kuleta mabadiliko makubwa katika sekta hii ya elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe na Spika wetu wa viwango kwa kutuongoza na kuliendesha vyema Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri na uthubutu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa utendaji wao mzuri wa kazi za Wizara katika kuwahudumia wananchi na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango/ushauri wangu katika Wizara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mtaala wa elimu ya msingi na sekondari uendane sambamba na mazingira ya maeneo husika ndani mikoa ili uindane na wakati uliopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaala wetu wa elimu kuanzia ngazi ya msingi hadi vyuo vya juu umwandae kijana kuweza kujiajiri na kujitegemea mara baada ya kumaliza masomo yao ili kupunguza ongezeko la vijana wasiokuwa na ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa iongeze jitihada zaidi katika kuboresha mazingira ya vyuo vya elimu ya kati/*VETA* pamoja na kujenga majengo ya *VETA* kila wilaya nchi nzima ili kuwasaidia vijana kuweza kupata elimu ya amali kwa urahisi zaidi, ili kupunguza wimbi kubwa la vijana mtaani na kuwaepusha na kujiingiza katika vikundi viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kuboresha mazingira rafiki ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia hasa masomo ya sayansi nchini ili wanafunzi waweze kupenda masomo ya sayansi zaidi bila ya kulazimishwa ili tuweze kuzalisha wataalamu na wasomi mahiri wa sayansi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara iandae mfumo/ mpango maalumu wa kutoa elimu ya umuhimu wa elimu ya *VETA* na maisha yao ili jamii ione umuhimu wa elimu inayotolewa *VETA,* maana kuna vijana wengi bado hawatambui umuhimu na kudharau na kuona haina tija kwao na maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote napenda kutumia fursa hii adhimu na adimu, kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetupa kibali cha kuweza kukutana siku ya leo mahali hapa katika muda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani ya pili, nimpelekee Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani yake ambayo ameendelea kunionesha, kuendelea kuniamini mimi na mwenzangu Mheshimiwa Prof. Mkenda kuweza kumsaidia kwenye eneo hili dogo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na ahadi yetu kwake kwamba, hatutamwangusha, tutahakikisha kwamba tunasimamia Wizara hii kwa uaminifu na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani nyingine ni ya kwako wewe Naibu Spika, Msheshimiwa Spika na Wenyeviti wetu wa Bunge kwa kusimamia vizuri Bunge letu hili. Shukrani nyingine ni kwa Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo kwa maelekezo, miongozo na maoni yao, ambayo kila mara wameendelea kutushauri juu ya namna gani tunaweza kuisimamia Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nitoe shukrani nyingi sana kwa Wabunge wenzangu ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa kwenye Hoja ya Wizara ya Elimu. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, lakini tunaomba tu tuwaambie kwamba, maoni na ushauri wenu wote tumeupokea na sisi, kama wasimamizi wakuu, tutaenda kuhakikisha kwamba yale maoni tunakwenda kuyafanyia kazi sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nitoe shukrani sana kwa Mheshimiwa Waziri, amekuwa ni mwalimu, amekuwa ni kiongozi, tumekuwa tukishirikiana kwa karibu sana. Pale Wizarani, Mheshimiwa Waziri ana msemo wake unaosema kwamba, ukitaka kwenda haraka nenda peke yako, lakini ukitaka kwenda mbali twende kwa pamoja. Kwa hiyo, ametengeneza *sense of ownership,* vilevile *sense* ya kufanya kazi kama *team work.* Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru Katibu Mkuu, Prof. Nombo na Manaibu Wakuu wote wawili, Prof. Mushi pamoja na Daktari Mahela; Wakuu wa Idara, Vitengo na Wafanyakazi wote wa

Wizara ya Elimu kwa ushirikiano ambao wanatupa katika kipindi hiki chote ambacho tunasimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa niwashukuru sana wananchi wa Mafia kwa kuniamini na kuendelea kunipa ushirikiano katika kipindi chote ambacho tunatekeleza majukumu ya Kiserikali. Niwaahidi tu wananchi wa Mafia, kwa namna yoyote ile sitawaangusha, tuendelee kushirikiana na kushikamana kuwa kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba niishukuru sana familia yangu kwa ushirikiano na uvumilivu katika kipindi hiki chote wakati tunatekeleza majukumu ya Kiserikali. Baada ya utangulizi huo naomba sasa nijikite kuchangia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naongeza muda kidogo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo dogo ambalo Waheshimiwa Wabunge wameleta ushauri, pamoja na hoja zao mbalimbali, eneo la kwanza ni kwenye Ujenzi wa Vyuo vyetu vya *VETA,* vile 64 vya wilaya na kile kimoja cha mkoa, ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba, twende tukajenge vyuo vya *VETA* katika maeneo yote katika wilaya zote ambazo zilikuwa hazina *VETA* hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmechangia hoja hii kwamba, sisi kama Wizara, tutasimamia kwa karibu au tumeendelea kusimamia kwa karibu na mpaka hivi leo naomba niwahakikishie tu kwamba, zaidi ya shilingi bilioni 72 zimeshatoka, zile za awamu ya kwanza kati ya zile shilingi bilioni 100 na ujenzi kule umefikia asilimia 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matamanio yetu kwamba utakapofika mwezi wa Kumi mwaka huu 2025 ile awamu ya kwanza

ya majengo tisa tuwe tumeweza kuikamilisha, ili basi mafunzo yale ya muda mfupi utakapofika mwezi Novemba au Disemba, mwaka huu 2025 yaanze kutolewa na itakapofika Januari mwakani, 2026 kwa awamu hii ya kwanza, basi vyuo hivi viweze kuanza kutoa mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ujenzi wa vyuo hivi 64 unaenda sambamba na ununuaji wa vifaa. Kama mnavyofahamu, tulianza ujenzi wa vyuo vya awali kabisa, vyuo 25 vile vya wilaya vinne, vile vya mikoa na vyuo, hivi vyote vinahitaji vifaa kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwathibitishie kwamba, katika bajeti yetu ya 2023/2024 tulitenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 2.1, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa. Vilevile tulitenga fedha, kwa ajili ya ununuzi wa vitabu katika mwaka huo huo, zaidi ya shilingi milioni 345. Vifaa hivi kwa mwaka huu, ambapo kwa fedha hizi tulizotenga, vilikuwa vimenunuliwa kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 7.2. Tayari wazabuni wamepatikana kwa ajili ya usambazaji wa vifaa hivi. Vimeshanunuliwa na hivi sasa wazabuni wako tayari kwa ajili ya kuvipeleka kwenye maeneo mbalimbali ambayo tayari vyuo vimekamilika na vifaa hivi vinahitajika. Kwa hiyo, wale Wabunge wenzangu wa Ikungi, ambao walizungumza hapa habari ya zile *VETA* 25, vifaa vyake viko tayari na hivi sasa tunavipeleka kuhakikisha kwamba, huduma ya elimu kule inatolewa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 tumetenga fedha katika bajeti yetu zaidi ya shilingi bilioni 2.5, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Pia, tuna mradi mkubwa wa *ESPJ* ambao una fedha zaidi ya shilingi bilioni 286, fedha hizi zinaenda kutumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa katika vyuo vile vya zamani 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, vyuo 34 ambavyo tayari ujenzi wake umekamilika vilevile vitasaidia kununua vifaa katika hizi *VETA* 64 za wilaya na kile kimoja cha Mkoa wa Songwe, ambavyo tunakadiria kufika mwezi wa Kumi ujenzi utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, vyuo 34 ambavyo tayari ujenzi wake umekamilika vilevile vitasaidia kununua vifaa katika hizi *VETA* 64 za wilaya na kile kimoja cha Mkoa wa Songwe, ambavyo tunakadiria kufika mwezi wa Kumi ujenzi utakuwa umekamilika. Kwa maana hiyo, vifaa vitakuwa vinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tayari tumeshajipanga vizuri, bajeti yetu hii ambayo tutaipitisha hapa leo, itakapofika mwezi wa Saba tutakapoanza kutumia kipaumbele cha kwanza tutakipeleka kwenye ununuzi wa vifaa kwa ajili ya *VETA* zetu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna vyuo vyetu 54 vya *FDC,* navyo vilevile vitakuwa *covered* kwenye hii shilingi bilioni 286. Kwa hiyo, niwaondoe hofu kwenye eneo hili la ununuzi wa vifaa kwa ajili ya vyuo vyetu vya *VETA,* vile vilivyokamilika na hivi tunavyoendelea kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ununuzi wa vifaa, tumeendelea kutoa ajira kwa walimu wa ufundi ambapo zaidi ya walimu 465 tayari wameshaajiriwa kwenye eneo hili. Kwa hiyo, kazi hii tunaendeleanayo Waheshimiwa Wabunge na tutaendelea kuifanya kwa uadilifu na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili lililozungumzwa hapa ni eneo la wadhibiti ubora. Tunafahamu kuwa tulifanya mabadiliko kidogo ya muundo wa Wizara kwa kuwaingiza wadhibiti ubora kuwa kama ni maafisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba wadhibiti ubora katika wilaya zote 164 walipandishwa daraja, na hivi sasa tunavyozungumza wako kwenye muundo mpya kistahiki na maslahi yao yote. Kwa hiyo zile

stahiki na maslahi yao yote yamezingatiwa kwenye muundo huu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Wizara au Serikali imeweza kujenga ofisi mpya za wadhibiti ubora katika wilaya 165. Vilevile tumefanya ukarabati wa ofisi zile za zamani kwenye zaidi ya wilaya 30. Sambamba na hiyo, tumepeleka vifaa vya ofisi, kwa maana ya *laptop, printer* takribani ofisi hizo zote ninazozizungumzia. Kwa hiyo, mazingira yale ya kufanya kazi kwa maana ya wadhibiti ubora tumeyaaminisha kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumenunua magari kwa ajili ya kufanyia kazi wadhibiti ubora katika wilaya karibu zote 164…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** … kwa hiyo, wilaya zetu karibu zote za udhibiti ubora tayari zina magari kwa ajili ya matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nami naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii ya kuhitimisha hoja. Jumla ya Wabunge 36 wamechangia moja kwa moja Bungeni, na tumepata michango mingine kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wote kwa pamoja wamezungumza mambo mengi ambayo napenda kuhakikishia kwamba tunayabeba. Mengi ni ushauri ambao tutauzingatia. Kwa

hiyo, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu, nawahakikishia kwamba tutazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Husna Sekiboko, na Makamu, Mheshimiwa Mussa Sima nao wametoa taarifa yao ambayo kwa ujumla wake kwa kweli hatuna la kubisha, wala kupingananao. Ni suala ambalo tutalichukua na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo tunawashukuru sana Kamati yetu kwa sababu pamoja na kwamba wakati mwingine wamekuwa wakali kidogo wakati wa kutusimamia, lakini siku zote wamefanya hivyo kwa lengo la kujenga, kuendelea mbele. Kwa kweli kama kuna mahali tumefanya vizuri sana, itakuwa ni kwa sababu ya mchango mkubwa wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Husna Sekiboko na Makamu wake. Naomba niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nielezee kwamba katika michango yote hii tuliyoisikia, kila Mbunge aliyeongea hapa pamoja na Kamati wamempongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wamempongeza kwa mengi; kwa mageuzi makubwa ya elimu ya kihistoria kwa namna fulani ukiacha yale mageuzi yaliyofanyika miaka ya 1960, sasa hivi ni mageuzi ya pili makubwa na huenda yakawa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamempongeza kwa ongezeko la bajeti katika Wizara ya Elimu na katika sekta ya elimu kwa ujumla. Pia wamempongeza kwa kuongeza mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na hata vyuo vya kati. Pongezi kwa ujenzi wa vyuo vya *VETA*, vyuo 64 jumlisha moja, wamempongeza Rais wetu kwa ujenzi wa shule za amali, wamempongeza Rais wetu kwa kuendelea kujenga kampasi mpya za vyuo vikuu katika mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, na ninajua Mheshimiwa hapa alizungumza Manyara ni mojawapo ya mikoa ambayo

imepata kampasi ya chuo kikuu, kampasi ya taasisi ya elimu na juu. Mtwara kwa mara ya kwanza sasa watakuwa na *university college,* Kagera wanapata *university college,* Kigoma, Lindi, Tanga, Njombe, na mikoa mingine ya Singida, Tabora, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga na mikoa mingine yote ambayo ilikuwa haina kampasi ya chuo kikuu. Sasa hivi tutabaki na Mkoa wa Pwani tu ambao na wenyewe mkakati wake unafanywa. Kwa hiyo, wote wamempongeza Mheshimiwa Rais kwa haya yote na mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wote kumpongeza sana Rais wetu kwa uongozi wake makini na ujasiri wake mkubwa wa kusimamia sekta ya elimu na kuruhusu mageuzi makubwa haya yafanyike, jambo ambalo ni rahisi sana kulikwepa na kukimbilia katika miradi mingine ya majengo, madaraja, reli na kadhalika ambayo inaonekana kwa macho kuliko mageuzi ya mfumo ambao matokeo yake yanachukua muda mrefu kuonekana. Tunamshukuru na kumpongeza sana Rais wetu kwa maelekezo yake, uongozi wake na jinsi ambavyo anapeleka Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais ambaye anamsaidia Rais na katika kutusimamia sisi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri wetu Mkuu ambaye vilevile anatusimamia katika utekelezaji wa kazi siku hadi siku; na Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko ambaye naye anasaidia katika Ofisi ya Waziri Mkuu katika uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika Wizara ya Elimu, Elimu ya Juu tunafanya pamoja mpaka upande wa pili wa Muungano na hata katika elimu nyingine hii tunashirikiana sana. Kweli na nimewahi kutembelea Ikulu ya Zanzibar takribani mara tatu katika masuala ya elimu. Namshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kutoa shukrani nyingi sana kwa Spika wetu, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa

uongozi wake wa Bunge letu, wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa uongozi wako jasiri na mahiri sana, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kutuongoza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika yote yaliyozungumzwa, nitazungumza machache kwa dondoo. Moja, ni mageuzi na hasa suala la amali ambalo limezungumzwa hapa, kukubali kwamba inabidi tuendelee kuyasema haya mambo zaidi ili watu waweze kuyaelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ngoja nieleze kidogo katika mageuzi ya elimu, katika suala la kuwa na mkondo wa elimu jumla na elimu ya amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mageuzi yetu yanatusababisha sasa sekondari ya *O' Level* iwe na mikondo miwili; mkondo wa elimu jumla na mkondo wa elimu amali. Nitazungumzia mkondo wa elimu amali. Elimu amali ni kile tunachokiita ufundi na ufundi stadi. Kwa Kiingereza *it is technical and vocational training*. Ni *technical and vocational training.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, amali siyo fundi tu, lakini ufundi ni amali na ufundi stadi ni amali ingawa ufundi stadi siyo ufundi. Kwa hiyo, ule ufundi wa kihandisi ni *sub-component* ya ufundi ya mafunzo ya amali kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, zile shule alizozungumzia Mheshimiwa Maige hapa, kwa mfano *Moshi Technical School, Ifunda Technical School, Tanga Technical School* ni shule za amali ufundi. Kilosa shule ya kilimo ilikuwa ni shule, na kwa kweli haikuendeshwa kama shule ya amali kwa sababu ilikuwa bado ni elimu jumla sana na mashamba makubwa, lakini ni shule ambayo inaweza ikawa ni shule ya ufundi stadi; amali na ufundi stadi, siyo ufundi. Kwa hiyo, yenyewe inaweza ikazingatia masuala ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hivi shule nyingi ambazo tumejaribu kuzifufua hasa hizi tisa ni zile shule za ufundi, amali ufundi. Pia tutakuwa na shule za amali kilimo, amali ukarimu, amali michezo na kadhalika na kadhalika. Hilo suala ni muhimu sana kulielewa. Katika shule za amali, sekondari za amali, baada ya kumaliza *form four* unapata cheti chako cha *NACTVET* na cheti cha *form four*. Ukitaka kwenda *high school* ya amali, iwe ni ufundi ama ufundi stadi, unakwenda *high school* kwa miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ngoja nizungumzie *high school* ya ufundi, kama ambavyo alikuwa anaeleza Mheshimiwa Maige. Ukienda *high school* ya ufundi, unakwenda kwenye *Polytechnique* kama ilivyokuwa *Dar Tech*. Tunarudisha tena hapa Tanzania *Polytechinical Schools.* Tunajenga moja Mwanza, tunajenga nyingine Kigoma, tunajenga nyingine Mtwara, tunajenga nyingine Morogoro, tunajenga nyingine Zanzibar na tayari tuna Chuo cha Ufundi hapa Dodoma kimekamilika, na sasa hivi kimeunganishwa na Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam, lakini nacho kitakuwa kama *Polytechniques*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa wale wanaosomea elimu ya ufundi, siyo ufundi stadi, wakienda *high school* wakuwa miaka mitatu watapata *diploma* na cheti cha *form six,* lakini ili kuondoa tatizo lililosababisha *Dar Tech* ibadilike iwe taasisi ya elimu ya juu, wale wakiamua kwenda chuo kikuu kusoma *engineering* watasoma miaka mitatu badala ya kusoma miaka minne. Kwa hiyo, hawatopoteza tena mwaka mmoja kama ilivyokuwa wakati ule. Kwa hiyo, hii ni hatua kubwa sana, tunamshukuru Rais wetu kwa ilivyo. Narudia tena, mafunzo ya amali ni seti yenye ufundi na ufundi stadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa ni kuhusu kuweka vifaa katika shule hizi. Ni kweli kabisa, tungetamani sasa hivi tuwe na takribani nusu ya sekondari zote ziwe shule za mafunzo ya amali, lakini kwa makusudi tumeamua twende hatua kwa hatua. Shule ikiwa ni shule amali lazima iwe na

uwekezaji wa kutosha. Tusipeleke shule ikawa shule ya amali halafu baadaye wazazi wakaona kwamba tunapoteza muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi moja tu tuliitembelea tuliona ilianza mageuzi kama haya yaka-*collapse* kwa sababu wazazi walihisi kwamba wanadanganywa. Kwa hiyo, shule hizi nyingi, pamoja na *Moshi Tech* na *Tanga Tech,* vifaa vinanunuliwa ili kuhakikisha kwamba kuna vifaa. Karakana zile zilizokuwepo zamani, nyingi sasa hivi zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulimtuma Katibu Mkuu kwenda India, ametembelea kule, tutakwenda China, *South Korea,* tumezungumza na Ujerumani na Switzerland kwa ajili ya kupata vifaa vya kisasa zaidi vya elimu ya ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya ufundi wakati mwingine siyo lazima utumie *material* na kuyamaliza. Sasa hivi unaweza ukatumia *virtual training* kwanza. Kama ni *welding,* unatumia kwanza kwa *simulation* halafu baadaye ndipo unakwenda kufanya *actual activity.* Sisi pia tunalenga kwenda huko, kwa sababu bila ya hivyo, *of course* itakuwa ni gharama sana kuendesha shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi shule tunazozijenga za amali tulizonazo sasa hivi hazitaanza kufanya kazi bila kuwa na vifaa na wakufunzi wa kutosha. Tuko tayari kwa yale maeneo ambayo hatuna wakufunzi hapa nchini, kutafuta wakufunzi kutoka nje waje kwa muda ili tuweze kuinua viwango vya elimu ambayo tutavitoa hapa nchini, ndiyo maana tunakwenda taratibu. Wako wengine wanasema tunaenda taratibu sana, wengine wanasema tunaenda haraka sana, lakini ukweli ni kwamba, ni lazima twende kwa makini vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *high school* nyingine za mafunzo ya amali ambazo siyo ufundi, tuna vyuo vya kilimo hapa nchini, vyuo vya mifugo, vyuo vya utalii na kadhalika. Tutavi-*align* vitoe fursa ya *high school education,* kupata *diploma* na kupata cheti cha *form six*

*at the same time,* na baada ya hapo akitaka kuendelea wataenda chuo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba nilizungumze, limezungumzwa vizuri sana kwa ufasaha na Mheshimiwa Prof. Muhongo, Mheshimiwa Prof. Manya na baadhi ya wachangiaji wengine. Hili ningependa nilielezee, kwanza tayari tumeanza kutoa *scholarship,* tumeanza kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wanaofanya *master's degree*. Tuna wanafunzi takribani 80 ambao wanafanya *master's* chini ya Bodi ya Mikopo katika Taasisi yetu ya Sayansi na Teknolojia, Nelson Mandela pale Arusha, kwa sababu tunataka kile Chuo kibaki kuwa ni *graduates' university,* kisichanganye kuwa na *undergraduate,* bali ki-*focus* kwenye *research* na kufundisha watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kweli kuwa kuna wakati tuliacha tu tunaletewa *scholarship,* tunapeleka watu bila ku-*define* tunataka nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumebadilika. Kwa mfano, kwenye Tume yetu ya Atomi tumeangalia, hatuna wataalamu wa kutosha hapa Tanzania. Tulikuwa tunatafuta Mtendaji Mkuu tena hata hawapo, wengine wameshastaafu, walikuwa Makamu wa Rais, hapa alikuwa ni mtalamu wa kule. Kwa hiyo, sasa hivi tumeamua kwamba tunapeleka Watanzania kwenda kusoma nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, uwe mtumishi wa Tume, la sivyo mfanyakazi wa chuo kikuu, la sivyo Mtanzania, *passport* yako iwe ni ya Kitanzania. Tunawapeleka watano kwenda kufanya *master's* katika masuala ya Atomi kwa sababu ni muhimu sana katika uchumi wetu. Hiyo inaitwa *Samia Extended*. Kwa hiyo, tunawapeleka nje kwenda kufanya *post graduate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kuliko yote, ukisikiliza vizuri mazungumzo ya maendeleo ya sayansi na teknolojia, wanakwambia *the future is uncertain, technological development is going to be destructive,* ita-*cause dislocation* kwenye *labour market.*

Kuna watakao-*gain* na watakao-*lose*. Ambao hawajajiandaa wata-*lose*. Hata katika kujitawala sisi wenyewe, tunapokwenda katika akili-unde, yaani unde ni akili iliyoundwa; pengine hata neno *artificial intelligence* lingekuwa *constructed, intelligence* ingekuwa *appropriate* zaidi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akili-unde inakotupeleka sasa hivi itatukimbiza kwa kasi ambayo hatujapata kuona. Wanasema *the future is so uncertain,* lakini *the future is already here*. Sasa sisi tunafanyaje? Tayari tumeandaa kwenye bajeti hii, tumetenga shilingi bilioni tano na *potentiality* zitaongezeka kwa ajili ya kuwapeleka Watanzania kwenda kusoma nje masuala ya *data science* katika vyuo tutakavyovichagua sisi. Watakwenda kusoma *first-degree* na baada ya hapo wanaweza wakaendelea. Huko wasome akili-unde, wasome *machine learning,* wasome *internet of things* na kadhalika na kadhalika. Tujiandae na *future*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, tutafanyaje katika suala hili? Kwanza, wanafunzi wa sayansi ambao wanamaliza mtihani wa *form six* sasa hivi, matokeo yatakapotoka huwa tuna-*shortlist* wale wote ambao wana-*qualify* kwa *Samia Scholarship*. Mara nyingi wanakuwa ni kuanzia mwanafunzi wa kwanza kwa *performance* mpaka mwanafunzi wa 640 mpaka 700. Wale tutawatangaza kama kawaida, halafu tutawaambia wanaotaka kwenda kusoma nje ya nchi *first degree* waombe, tutawa-*shortlist*. Pengine watakuwa kati ya wanafunzi 50 hadi 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti yake ni kwamba hawataingia chuo kikuu mara moja. Tutawachukua tutawapeleka *Nelson Mandela African Institute of Science and Technology* pale Arusha ambako watafanya *boot camping*. Watakaa kwenye kambi pale, watafundishwa uzalendo, watafundishwa maadili, na watafundishwa *digital literacy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukawa na *first class* ya *PCM* lakini hujagusagusa kompyuta. Utafundishwa namna usije na *cultural shock* ukienda kusoma nje. Kuwaandaa wawe tayari, na baada ya

takribani miezi kumi tutawapeleka kwenda kusoma kwenye vyuo tutakavyochagua kwenye masomo ya *computer science in related allied science's,* lakini *mostly* kwa ku-*aim* mambo ya *artificial intelligence*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kambi tunawapelekaje? Kwanza tunazo *Scholarships* nyingi ambazo hatuzitumii vizuri hapa Tanzania. Juzi nimetoka Saudi Arabia na Katibu Mkuu, tuna *Scholarships* hatuzitumii. Tutawaambia Saudi Arabia zile *Scholarships,* tunataka *scholarship* 10 hizo au 100 ziende kwa wanafunzi hawa kwa masomo tuliyochagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *scholarships* nyingine tunapata kutoka Hungary, *scholarships* nyingine tunapata kutoka China, tutasema hizi *scholarship* tunazichukua lakini tunataka wakasome masomo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumaliza zile nafasi ambazo tunazipata kama *scholarships* tunawatumia Watanzania *diaspora* na tunawanaunganisha, watuunganishe katika vyuo ambavyo wanafanya kazi ili mradi tu hatutapeleka mwanafunzi aliyemaliza *form six* mmoja mmoja tu. Tutahakikisha kwamba tunawapeleka kwa *batch* ili wasiende wakapata shida kuji-*adjust;* waende walau watano au kumi kwenye chuo kimoja ili washirikiane, wajenge umoja, wakakaa tu wana-*adjust* kwa ajili ya kusoma vile. Wanaobaki wengine watasomeshwa na pesa za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tunazungumza na wadau ili hizi bilioni tano ambazo huenda tuna-*negotiates* ziongezeke, wadau wengine, na niwataje kabisa, *CRDB, NMB, Tanzania Commercial Bank,* wamekuja wamesema wataangalia namna ya kuungana na sisi. Hii nayo ni *Samia Scholarship Extended* lakini ita-*focus* kwenye *data science*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuanzia sasa hivi wanaomaliza *form six* na waisikie Serikali inasema wale watoto wa mkulima ambaye hakusoma *International School* kama wengine,

kwamba sasa hawezi kuomba *scholarships,* tutakapomweka Nelson Mandela pale tutamsaidia na kuomba hizo *scholarship,* tutawa-*guide* ili Watanzania nao waanze kuchukua hizi *scholarship* ambazo zinakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, vijana wetu hawawezi kuziomba, wanaoomba wengi ni wale waliosoma *international school,* watoto wa wakulima na wafugaji wataenda lini kupata hizi fursa wakati na wenyewe wana uwezo? Kwa hiyo, tunalifungua hilo suala moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda lingine niliseme haraka haraka, limezungumzwa hapa kuhusu vyuo vya elimu tiba kuwa na hospitali ya kufundishia. Naomba niseme kwamba hakuna chuo kikuu cha elimu tiba hapa Tanzania ambacho hakina hospitali ya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugomvi uliopo ni umiliki wa hospitali, kwamba usipomiliki pengine uratibu unaweza ukawa na shida, kwamba wewe una chuo, ni cha Serikali, humiliki hospitali ambayo una mkataba nayo halafu hospitali ikiamua kuleta wanafunzi kutoka nje, labda wametoka Sudan, ukajaza nafasi ambazo wale wanafunzi wa chuo kikuu walitakiwa wakitumie kwa ajili ya kujifunzia, inaleta utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa duniani, siyo vyuo vyote vya elimu-tiba vinamiliki hospitali. Kuna muundo wa hospitali na chuo kikuu kuwa chini ya *entity* moja na bado kuna muundo. Hata Marekani na nchi nyingine, chuo kikuu na hospitali huwa na makubaliano ya namna ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaendelea na mazungumzo hasa pale Mloganzila ili kuona cha kufanya. Kwa sababu Mloganzila sasa hivi, na jana nimepata taarifa nzuri, *two more centers of excellence in East Africa* vimeanzishwa pale Mloganzila. Sasa na wenyewe wanauliza, hii hospitali tunaimiliki vipi? Kwa sababu hizo *centers of excellence* ni pamoja na tiba. Kama zinafanya utabibu,

hata bajeti yao watapitisha wapi? Watapitisha Wizara ya Elimu au Wizara ya Afya? Hilo najua linafanyiwa kazi, tutajaribu kulitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile *tension* zinazo-*exist* kati ya vyuo vikuu na hospitali za kufundishia tunazifanyia kazi, lakini kwa asilimia kubwa sana mambo yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimetoka kuzindua Chuo Kikuu cha *KCMC*. Hakimiliki Hospitali ya *KCMC* ingawa sasa chuo kikuu kile na hospitali ya *KCMC* vinamilikiwa na taasisi moja. Sasa, na sisi hospitali zetu na vyuo vyetu vinamilikiwa na Serikali moja. Kwa hiyo, naamini kama ni uratibu, tutafanya uratibu unaotakiwa, na pale ambapo tunahisi inabidi kabisa chuo kikuu kimiliki hospitali, tutazungumza, halafu tujue bajeti ya afya ile itapitia Wizara gani? Ndiyo utata mdogo ambao uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kuwahakikishia Watanzania wasije wakaelewa vibaya kwamba suala hilo ni umiliki, siyo matumizi, kwa sababu tayari yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Kanyasu na hili niliseme vizuri. Juzi hapa nimekutana na kijana anafanya kazi Guinea Conakry amesoma *VETA* ya Moshi ya mambo ya *mining* kwa sababu tu *VETA* ya Moshi ina *industrial link* na *GGM*. Tulifanya mapema sana na tuliandika barua Wizara ya Madini, tumemwomba Mkuu wa Mkoa na Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba, Chuo cha *VETA* pale Geita kiwe ni chuo cha kufundisha masuala ya madini kwa kushirikiana na migodi iliyopo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuongea na wenzetu wa madini watusaidie tufanye vile. Nilishangaa na kufurahi kuona vijana wa *VETA* ambao wamesoma mambo ya madini pale Moshi wanafanya kazi Mauritania, nchi inayoongea Kifaransa na Kiarabu, wanafanya kazi Ghana, Guinea Conakry na Namibia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, fursa hii ya ajira ni kubwa endapo tutajenga *industrial link*. Kuna maelekezo mahususi tumewapatia *VETA* na tunawapima kwamba, lazima wa-*establish industrial link,* siyo tu na migodi, lakini pia na wanaoshona nguo na suti. Tumefanya nao vikao wale watengeneza *furniture* na shughuli nyingine zote za uzalishaji, ili ufundishaji unaofanyika kwenye *VETA* ulandane na mahitaji ya *industry* yanavyokwenda na tutawapima wenzentu wa *VETA* wamefikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Mheshimiwa Mulugo alizungumza hapa, nilizungumze kidogo. Mheshimiwa Rais wetu wakati anazindua Sera ya Elimu na Mafunzo alilisema, *PPP* kwenye elimu, tunapoelekea tunahitaji kuwa na *transition* ya watoto wote wanaomaliza darasa la sita kwenda sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawekeza miundombinu, tunaongeza uwekezaji, sisi na TAMISEMI tunafanya kazi pamoja. Tumetengeneza *booklet,* tunaendelea ku-*update geographical distance* ya *households* na shule kuhakikisha kwamba, tunaweka miundombinu ya kutosha na *inshallah* tutapata na walimu wa kutosha kuhakikisha kwamba, kweli wanafunzi wote wanaomaliza watasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kwa maelekezo kwamba tuangalie fursa ya *PPP,* tunaangalia na sekta binafsi utusikie kwamba, tunaweza ikibidi tutafute namna ya kuingia makubaliano ya muda fulani ambayo wewe umejenga Sekondari hasa ya Amali, Serikali ku-*guarantee* ni kwa muda gani itakuwa ikileta wanafunzi na kuwalipia katika shule yako ili kuhakikisha kwamba tunachukua wanafunzi wote waendelee kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukiona *speed* haiendi vizuri, nadhani sekta binafsi ina-*role to play*. Kwa hiyo, natoa wito kwa sekta binafsi ambao wameonekana kuchangamkia sana Elimu ya Amali kwamba, huenda kutakuwa na fursa na tutaanza majadiliano hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwekeza vizuri kwa viwango vinavyotakiwa, na walimu wanaofaa, usipoweka *fees* ambazo ni *exorbitant* zitakazozuia watu wasiende, Serikali iangalie uwezekano kwamba, wanafunzi waliobaki, hawa tunawa-*allocate* katika shule inayoendeshwa na watu binafsi, ili waendelee kusoma. Kama ni mkataba wa miaka mitano au 10, hayo tutaamua pamoja na Hazina ambao wanasimamia utaratibu wa *PPP,* lakini tunaweza tukawahitaji sana sekta binafsi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunavuka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lugha ya alama, ni kweli imezungumzwa hapa vizuri, kuna Mheshimiwa Mbunge hapa alizungumza hoja yake yote ilikuwa ni kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Namshukuru sana, ninadhani tutamwita tukae naye, ana uelewa mpana sana. Kwenye Sera yetu ya Elimu, lugha ya alama itakuwa ni *mandatory* kwa watu wanaosomea ualimu kwa sababu kama unafundisha shuleni ni lazima uweze ku-*communicate* na wanafunzi wa aina zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tuna Shule Maalum lakini tungependa zaidi Shule Mchanganyiko, ili hawa wasionekane kama wanatengwa na jamii, wanaenda kwenye shule zao wao wenyewe. Hilo lipo katika sera kwa sababu tulizungumza wote tukashirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kidogo kabla sijatoa shukrani, mwongozo wa walimu wa kujitolea tupo tayari kuendelea kupokea maoni nimeyasikiliza, lakini mpaka sasa hivi kuna walimu 23,405 wameweza kukamilisha kupitia mwongozo huu. Mwongozo huu unamtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ashirikishwe, Kamati ya Shule ishirikishwe na taratibu zipo, lakini tunasema kila kitu kina nafasi ya kuboresha. Tutakaa na wenzetu kuona kama kuna nafasi ya kuboresha ili tupate wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa shukrani. Nimshukuru kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Kipanga kweli kwa kuwa mwenzangu katika uongozi wa Wizara na kuwa mwepesi

sana tunapopeana majukumu. Amesababisha kazi yetu iwe rahisi sana. Mheshimiwa Kipanga nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Katibu wetu Mkuu Prof. Carolyne Nombo na Naibu wake Prof. Mushi na Dkt. Mahera, kwa kuwa ni wachapakazi wanaosababisha kazi yetu iwe nyepesi sana na kuweza kutimiza majukumu tuliyopewa na Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Wakurugenzi na watumishi wote na taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa sababu kwa kweli wanafanya kazi *round the clock.* Naomba wapokee shukrani zangu za dhati hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 – Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………………..Sh. 9,707,804,145

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hatuna hoja za Mshahara wa Waziri, tunaingia kwenye *guillotine*. *(Makofi)*

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 46 – Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………....Sh. 9,707,804,145
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……......Sh.1,565,565,501
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…...............Sh. 2,234,401,500
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…........................Sh. 1,279,644,200
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*........Sh. 814,771,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*….Sh. 643,783,000
Kifungu 1007 – *Legal Unit*………………….……………Sh. 653,808,000
Kifungu 1008 – *Information, Communication, Technology and E-learning*………….Sh. 920,370,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*…….Sh.1,275,637,499
Kifungu 2001 – *Basic Education Development Office*..............................................Sh.95,676,056,504
Kifungu 2002 – *School Quality Assurance*………....Sh. 59,719,870,659
Kifungu 7001 – *Higher Education*……....................Sh. 371,688,153,808
Kifungu 7002 – *Technical and Vocational Training Division*……………………............Sh. 77,338,759,179
Kifungu 8001 – *Science, Technology and Innovation*……………….……….Sh. 65,095,609,005

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 18 – Tume ya Taifa ya *UNESCO***

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 3,240,288,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………………Sh. 1,931,842,077
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.............Sh. 2,585,395,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...............Shs. 87,072,550,417
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……......................Sh. 1,460,241,190
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*..Sh.1,312,108,685
Kifungu 1007 – *Legal Unit*………………………………Sh. 1,357,715,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*……Sh. 7,462,516,810
Kifungu 2001 – *Basic Education Development Office*……………………….........Sh. 219,556,889,106
Kifungu 2002 – *School Quality Assurance*…………Sh. 10,234,563,190
Kifungu 7001 – *Higher Education*………………..Sh. 1,136,726,296,411
Kifungu 7002 – *Technical and Vocational Training Division*…………….………………Sh. 260,078,314,76
Kifungu 8001 – *Science, Technology and Innovation*…………..………..……………Sh. 18,035,738,345

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 123 (3) (a) na (b), naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Bunge kwamba sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2025/2026 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, jana nilikupongeza, na kawaida yetu huwa tunapongeza wakati bajeti ikishapita, lakini kutokana na kazi nzuri na

maelekezo ya Mheshimiwa Rais ulivyoyapokea na kuyatendea haki, hongera sana wewe, Naibu wako na timu yako ya wataalamu. *(Makofi)*

Pia niwashukuru Wabunge kwa michango mizuri. Hii hoja ya walimu wanaojitolea, kwa kweli mnawaonea. Mheshimiwa Waziri hawa watu wanajitolea wengine zaidi ya miaka saba, lakini anakuja mtu ghafla tu anaingia, huyu anaonewa. Hili mlitazame kwa umakini sana. Nawaomba sana muwape kipaumbele. Ni *experienced,* wana uwezo na wana uzalendo mkubwa kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Baada ya maneno haya, ninawashukuru tena. Tunaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.09 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 14 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*